**8 MEI, 2026**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA TATU

### Kikao cha Ishirini na Tano – Tarehe 8 Mei, 2026

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mkutano wa Tatu, Kikao cha Ishirini na Tano, leo tarehe 8 Mei, 2026.

Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

### HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Katibu tuendelee.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na maswali Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Ado Shaibu Ado, Mbunge wa Tunduru Kaskazini, aulize swali lake.

Waheshimiwa Wabunge, ninawakumbusha kwamba, mkifika tu asubuhi mfungue vishikwambi vyenu hivyo vya kusemea ili muweze kuonekana nyote mpo, kwa sababu utakapofungua baadaye inaweza kuwa ni shida. Kwa hiyo, mkifika tu muweze kufungua mapema, yaani m-*login* ili tuweze kuelewana. Mheshimiwa Ado.

Na. 277

**Fao la Kujitoa kwa Watumishi**

**MHE. ADO S. ADO** aliuliza:-

Je, ipi kauli ya Serikali juu ya fao la kujitoa kwa waajiriwa na lini Serikali inafikiria kuanzisha fao hilo?

**MWENYEKITI**: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA MAHUSIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninaomba nimshukuru Mungu mwingi wa rehema kwa kunijalia uhai afya njema na neema ya kusimama kwa mara ya kwanza katika Bunge hili Tukufu, nikiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Mahusiano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa moyo wa unyenyekevu kabisa na shukurani za dhati, ninapenda kutumia nafasi hii hii, kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa imani kubwa aliyoionesha na kunipa dhamana hii adhimu ya kulitumikia Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatambua kwa kina kwamba uteuzi huu siyo heshima ya cheo, bali ni wito wa kazi, nidhamu na matokeo. Kwa hiyo, mbele ya Bunge hili Tukufu na mbele ya Watanzania wote, ninamwahidi Mheshimiwa Rais kwamba, nitafanya kazi kwa uaminifu kwa bidii, kwa uadilifu, weledi na uzalendo. Nitakuwa mnyenyekevu katika kujifunza, shupavu sana katika kutekeleza wajibu wangu na nitakuwa mwaminifu maeneo ya kazi, nikisimamia maslahi ya wananchi, hususani maeneo ya kazi, ajira na mahusiano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kubwa ninakishukuru Chama changu cha *NCCR*-MAGEUZI kwa kuniamini na kuniruhusu kutumika katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa maslahi ya Watanzania wote. Hatua hii ninaomba itukumbushe kwamba Taifa letu ni kubwa kuliko tofauti zetu zozote tunazoziona na pale maslahi ya wananchi yanapotangulizwa mbele basi Tanzania inashinda. Nina hakika, tumemshinda adui. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo, ninaomba nijielekeze kwenye swali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Mahusiano, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Ado Shaibu Ado, Mbunge wa Tunduru Kaskazini:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ado, ni kaka yangu ninaweza kusema ni wa damu, tumetoka mbalimbali kisiasa amekuwa akiniusia sana juu ya siasa safi. Kwa hiyo, ninatambua mchango wake kwenye siasa safi na pia ninatambua mchango wake katika kuwatetea wafanyakazi wa Taifa hili, hususani watu wake wa Tunduru. Hata hapa nilipo wosia wake umefanya kazi sana. Kwa hiyo, ninamshukuru pia Mheshimiwa Ado, kaka yangu wa damu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mafao ya mifuko ya hifadhi ya jamii hakuna fao la kujitoa mwanachama anapopoteza ajira bali kuna fao la kukosa ajira. Mwaka 2025 Serikali ilifanya maboresho ya kanuni za ulipaji wa mafao katika mifuko ya hifadhi ya jamii kwa kuboresha fao la kukosa ajira ili kumpa mtumishi uwezo wa kuamua kulipwa mkupuo maalum *(special lumpsum)* au 33.3% ya mshahara

wake kwa kipindi cha miezi sita ili kutopoteza sifa za kulipwa pensheni kipindi atakachostaafu. Kwa sasa, Serikali inaona kuwa utaratibu huu unakidhi matakwa ya watumishi wanaopoteza ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ado Shaibu Ado.

**MHE. ADO S. ADO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiri kwamba kinachoendelea ni fumbo la kisiasa katika siasa za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambapo Mbunge wa upinzani unasimama kumuuliza swali Naibu Waziri ambaye naye anatoka katika upinzani. Mtu ambaye siku chache zilizopita kikanuni alikuwa anahesabika kuwa ni Mbunge wa 12 katika kambi ya walio wachache. Kwa hiyo fumbo ambalo litapaswa kuendelea kutafakariwa katika siasa zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu dogo moja la nyongeza; kwa kuwa kinachoitwa fao la kukosa ajira halitoi manufaa yote ambayo yalikuwa yanapatikana katika fao la kujitoa; Serikali kwa kuendeleza msimamo wa kutorejesha fao la kujitoa haioni kwamba inawanyima haki, kuwanyonya na kuwadhulumu wafanyakazi ambao walikuwa wanapata manufaa katika fao la kujitoa; hasa wale ambao wanakosa ajira na ambao wana ajira za vipindi vifupi vifupi?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA MAHUSIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu kwenye swali langu la msingi; lakini pia baada ya kusikiliza maoni ya wadau mbalimbali na kwa usikivu wake uliotukuka uweledi na uelewa mkubwa alionao Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri, Kazi, Ajira na Mahusiano, mwaka jana mwezi Desemba alisaini kanuni; ambapo kama mwajiriwa anapoteza ajira anaweza kuchukua mafao yake ya jumla ndani ya siku 90. Hii ni kwa mkupuo na hii ni *special unemployment lumpsum*. Kanuni hii aliisaini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikwambie ukweli, hili suala lilipokelewa kwa nderemo na vifijo na shangwe kubwa kwa wadau wetu wote wa Mfuko huu. Ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana, Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu hayo ya Mheshimiwa Mbunge.

Tunaendelea na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI; Mheshimiwa Dougras Didas Massaburi.

Na. 278

**Kukamilisha Ujenzi wa Barabara na Madaraja Pugu – Msongola kwa Kiwango cha Lami**

**MHE. DOUGRAS D. MASSABURI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa barabara na madaraja kutokea Pugu – Majohe, Viwege hadi Mbondole na Msongola kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Dougras Didas Massaburi, Mbunge wa Jimbo la Kivule, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Pugu – Majohe Viwege hadi Mbondole, Msongola yenye urefu wa jumla ya kilometa 12.47. Serikali ilikwishaanza kujenga barabara hii kwa tabaka la lami nzito na zege, ambapo katika mwaka wa fedha 2022/2023 kiasi cha shilingi milioni 555.27, fedha za mapato ya ndani ya Halmashauri ya Ilala kilitumika kujenga kipande cha barabara hiyo chenye urefu wa kilometa 0.4 kwa kiwango cha tabaka la lami nzito *(asphalt concrete)*. Aidha, katika mwaka wa fedha 2023/2024, jumla ya shilingi milioni

917.84 zilitumika kujenga kipande cha barabara hiyo chenye urefu wa kilometa 0.4 kwa tabaka la zege kwa kutumia mapato ya ndani ya halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la Serikali ni kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami; ambapo kwa sasa Serikali imemwajiri Mhandisi Mshauri *M/s* Mhandisi *Consultancy Limited* anayesimamia Mradi wa *DMDP II,* Wilaya ya Ilala kufanya mapitio ya usanifu huo, ikiwa na lengo la kupata gharama halisi za utekelezaji wa ujenzi wa barabara hiyo kwa tabaka la lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutenga fedha ili kuhakikisha kuwa ujenzi wa Barabara ya Pugu – Majohe – Viwege hadi Mbondole, Msongola unakamilika kwa kiwango cha lami kwa lengo la kuboresha miundombinu ya usafiri na usafirishaji kwa wananchi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dougras Didas Massaburi.

**MHE. DOUGRAS D. MASSABURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa majibu mazuri ya Serikali. Wananchi wa Jimbo la Kivule hakika leo wamefarijika kusikia Serikali yetu Tukufu sasa imeingiza kwenye mpango barabara hiyo yenye zaidi ya kilometa 12 kwa ujenzi wa kiwango cha lami. Ninampongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo, ninao uzoefu fulani kwa miaka 10 katika Jiji la Ilala, pamoja na Unaibu Meya miaka nane. Barabara nyingi za *DMDP* ambazo tumesaini mikataba ni moja pekee yake ndiyo tayari imekwishapata fedha; Barabara ya Banana – Kitunda – Fremu Kumi mpaka Msongola. Hata hivyo, nayo bado inasuasua kwa sababu ya ulipwaji wa fedha. Ninamshukuru Mheshimiwa Rais, juzi wameingiza zaidi za shilingi 4,000,000,000 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa Barabara ile ya Banana – Kitunda mpaka Msongola.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, ziko barabara nyingine ambazo ziko kwenye 70% iliyobaki ya *DMDP;* Barabara ya Moshi *Bar* kwenda Kwa Mpolemba, Barabara ya Moshi *Bar* kwenda Bombambili kupitia kwa Diwani mpaka kwa Osama, Barabara ya

Kitunda – Mwanagati mpaka Buza Kwa Mpalange, pamoja na Barabara ya Kitunda kupitia Kibeberu kuelekea Magore na Nyangasa. Barabara nyingine ni ile Barabara ya Kitunda – Kivule – Msongola ambayo nimekwishaitaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; je, Serikali ina kauli gani kwa barabara hizi ambazo zimebakia ambazo nazo zipo kwenye mpango wa 70% ya *DMPD phase II?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; je, Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI yuko tayari kuongozana nami Jimboni kwetu Kivule ili kusudi tukafanye mkutano wa wananchi ambao Ofisi yake ya TAMISEMI ilitembelea pale kwenye Barabara ya Banana – Kitunda mpaka Msongola na kupitia njia nne na Serikali ikaahidi kufikia tarehe Mosi Aprili, barabara ile itakuwa imekwishakabidhiwa watu wanaitumia kwa kiwango cha lami, lakini leo tunapozungumza tayari tarehe takribani 8 Mei, sasa Serikali yangu Tukufu Mheshimiwa Naibu Waziri aniahidi hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, yuko tayari twende tukafanye mkutano na wananchi na kupata sasa tarehe mpya na kuwaambia wananchi kwamba tarehe Fulani, mradi huu utakuwa umekwishakamilika ili kusudi wananchi wetu waweze kufanya shughuli zao za uchumi pamoja na shughuli za kijamii.

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nimpomngeze sana Mheshimiwa Dougras Didas Massaburi, Mbunge wa Kivule; amekuwa msemaji na mwakilishi bora sana wa wananchi wa Jimbo la Kivule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge alishaleta hoja hizi Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI. Jambo ambalo limefanyika kwanza, kwa Barabara ya Banana – Kitunda – Msongola ambayo

ilikuwa na mkandarasi alisimama kwa muda lakini ameshalipwa zaidi ya shilingi 4,000,000,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa ninapoongea ameelekezwa kurejea *site,* kuhakikisha anatekeleza mradi wa barabara hii ili ikamilike mapema iwezekanavyo ili wananchi waendelee kutumia huduma bora ya barabara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutafuatilia ukamilishaji wa Barabara ya Banana – Kitunda - Msongola ambayo inajengwa kwa mpango wa *DMDP II* ili ikamilike mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, ni kweli tunazo barabara ambazo Mheshimiwa Mbunge amezitaja ambazo ziko kwenye ile 70% ya *DMDP*. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inaendelea kutekeleza Mradi wa *DMDP II* katika Wilaya ya Ilala katika Jimbo la Kivule. Tunaendelea kuweka taratibu za kifedha kuhakikisha kwamba barabara hizi alizozitaja tunakwenda kuzijenga kwa awamu ili barabara ziweze kupitika vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, niko tayari, tutapanga na mimi Mheshimiwa Mbunge, siku ambayo itapatikana twende Kivule, tufanye mikutano ya hadhara, tupite kukagua barabara zetu na kuhakikisha kwamba wananchi wananufaika na matunda ya Serikali yao hii sikivu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mariam Kisangi, Mheshimiwa Asia Halamga ajiandae; maswali mafupi ya nyongeza.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa changamoto inayolikuta Jimbo la Kivule inafanana kabisa na ile iliyopo kwenye Jimbo la Temeke katika barabara inayotoka Mashine ya Maji. Pamoja na juhudi za Serikali, ninaipongeza sana, hali ilikuwa mbaya; tumeanza kujengewa barabara ya zege. Je, ni lini Serikali itakamilisha kipande cha kutoka Mtoni Unguja kwenda Mashine ya Maji mpaka kwa Mama Kibonge?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatekeleza Mradi wa *DMDP* katika Halmashauri ya Temeke, katika Jimbo la Temeke. Nimhakikishie mama yangu, Mheshimiwa Mariam Kisangi, kwamba, kama alivyosema Serikali kwa kutambua umuhimu wa barabara hiyo imekwishaanza utekelezaji wa barabara hiyo na ujenzi umekuwa ukiendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie tu kwamba tutaendelea kuhakikisha kwamba maeneo hayo yote ambayo hayajakamilishwa wakandarasi wanaopewa kazi hizo wanazikamilisha kwa wakati. Nielekeze kwa Meneja wa *TARURA* wa Wilaya ya Temeke pamoja na Meneja wa *TARURA,* Mkoa wa Dar es Salaam kuendelea kusimamia wakandarasi walioko *site* ili waweze kutimiza majukumu yao kwa wakati na kuhakikisha kwamba hizo barabara zinakamilika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asia Halamga, Mheshimiwa Sara Ally ajiandae; maswali mafupi ninaomba.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Barabara ya Dirma – Simbay – Sirop yenye kilometa 23.6 ambayo ipo kwenye Ilani ya Uchaguzi kutokana na hali ya mvua imekuwa chakavu sana. Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara hii?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Dirma - Simbay – Sirop katika Jimbo la Hanang, Mheshimiwa Mbunge wa jimbo hilo, Mheshimiwa Asia Halamga amewasilisha mara kadhaa. Serikali hii kwa kujali na kutathmini ustawi wa wananchi wa Hanang tayari katika mwaka ujao wa fedha imetenga shilingi milioni 250 kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo kiwango cha changarawe kilometa 10 na kilometa nyingine

zinazobaki tutaendelea kutenga fedha kwa awamu kuhakikisha kwamba barabara hii inajengwa na kupitika vizuri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sara Ally.

**MHE. SARA M. ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Ni ahadi ya Serikali kujenga daraja lililovunjika ndani ya Jimbo la Mvomero, Kata ya Lubungo. Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa daraja hilo na madaraja mengine yaliyovunjika kwa ajili ya mvua?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, yako madaraja yaliyoharibika na kuvunjika kufuatia mvua nyingi ambazo zimenyesha mwaka huu. Serikali imeendelea kufanya tathmini; kwanza ya uharibifu; lakini pili ya gharama ya fedha inayohitajika kwa ajili ya matengenezo ya madarasa hayo; lakini tatu, kwa sababu maeneo mengi bado mvua zinaendelea kunyesha na katika maeneo ambayo uharibifu ni mkubwa siyo rahisi kuanza ujenzi wakati maji bado ni mengi yanatiririka katika mito hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, hilo daraja alilolitaja katika Jimbo la Mvomero na madaraja mengine katika jimbo hilo na katika majimbo yote kote nchini tumeweka mpango madhubuti kuhakikisha kwamba tunapeleka fedha mara baada ya hali ya hewa kukaa sawa ili kuendelea na ujenzi wa madaraja hayo kwa awamu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abubakari Asenga.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Nimesimama hapa kwa hali ya dharura kutokana na wakati huu ndiyo tunaelekea kuvuna mpunga. Halmashauri ya Mji wa Ifakara, kata 19 barabara zote zinazotoka mashambani hazipitiki. Nini mpango wa dharura wa Serikali wa kuhakikisha kwamba wanarekebisha barabara hizi ili kupunguza gharama ya mkulima

kufikisha mpunga wake katika maghala na mwananchi aweze kupata mchele na ubwabwa kwa bei rahisi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Ifakara ni jimbo lenye wakulima bora sana wa zao la mpunga na mazao mengine. Kwa kweli barabara ni nyenzo muhimu sana katika usafirishaji wa mazao kutoka mashambani kwenda kwenye maeneo ya majumbani na kwenye maeneo ya masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Asenga amelifuatilia mara kadhaa suala hili. Tayari kupitia Meneja wa *TARURA* wa Wilaya na Mkoa wa Morogoro, tumeshapata tathmini ya mahitaji ya matengenezo ya dharura ya barabara hizo. Nimhakikishie kwamba, tutakwenda kuhakikisha kwamba tunapata fedha angalau kurekebisha yale maeneo korofi ili barabara ziweze kupitika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirejee kuwasisitiza Mameneja wa *TARURA* wa Wilaya na Mkoa, yale maeneo ambayo yapo ndani ya uwezo wao, wanaweza wakafanya marekebisho kuwezesha wananchi angalau kuendelea kupitisha bidhaa zao kwa kipindi hiki wafanye haraka iwezekanavyo ili wananchi waendelee kupita wakati Serikali inaendelea na mpango ule wa kwenda kufanya marekebisho ya kudumu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Paschal Chinyele.

**MHE. PASCHAL I. CHINYELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kufuatia mvua zilizonesha katika maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Dodoma, barabara nyingi hasa katikati ya jiji zimeharibika na wananchi na yakiwemo magari ya kawaida yanashindwa kupita hasahasa barabara ya kutoka stendi ya Chang'ombe Juu kupitia Mnadani kwenda Ndachi haipitiki kabisa. Je, ni lini Serikali

itatengeneza barabara hiyo ukizingatia kwamba mvua sasa zimekoma?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge katika maeneo ambayo Serikali imeweka kipaumbele kikubwa sana katika Jiji la Dodoma, kwa sababu ya kuwa makao makuu ya nchi na taswira ya Taifa letu ni katika eneo la Sekta ya Barabara. Kwa hiyo sisi eneo la *TARURA* tumehakikisha kwamba tuna mpango wa *TACTIC* kuboresha barabara za Jiji la Dodoma. Tuna vile vile ule mpango wa ku-*transform* barabara za Jiji la Dodoma, lakini pia tuna mpango wa kawaida wa *TARURA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, barabara hiyo ya Mnadani - Chang'ombe Juu na maeneo mengine yote ni moja ya barabara ambazo tayari zipo kwenye mpango. Serikali inafanya utaratibu wa kupata fedha ili tuhakikishe barabara hizo zinajengwa mapema na kuwezesha usafiri kwa wananchi wa Jiji la Dodoma na Jimbo la Dodoma Mjini.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Jesca David Kishoa, Mbunge wa Iramba Mashariki.

Na. 279

**Kugawanya Kata ya Mwangeza – Iramba**

**MHE. JESCA D. KISHOA** aliuliza:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuigawa Kata ya Mwangeza ili kusogeza huduma za kijamii na kiutawala karibu na wananchi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**8 MEI, 2026**

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Jesca David Kishoa, Mbunge wa Jimbo la Iramba Mashariki kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, uanzishaji wa maeneo ya utawala katika Mamlaka za Serikali za Mitaa hufanyika kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), Sura 287 na (Mamlaka za Miji), Sura 288 pamoja na Mwongozo wa Uanzishwaji wa Maeneo ya Utawala wa Mwaka 2025 ambao umeainisha vigezo na taratibu zinazopaswa kufuatwa ili kugawanya na kuanzisha maeneo mapya. Kusudio hupita katika ngazi ya msingi (Vijiji au Mitaa), Kata, Wilaya na Mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muijibu wa mwongozo wa uanzishaji wa kata mpya wa Mwaka 2025, kata mpya inayoanzishwa inatakiwa kuwa na idadi ya watu wasiopungua 25,000 na kata mama inatakiwa kuwa na watu wasiopungua 25,000. Kata ya Mwangeza iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama haijakidhi kigezo hiki ikiwa zitagawanywa kata mbili. Kwa kuzingatia takwimu za Sensa ya mwaka 2022, Kata ya Mwangeza ina jumla ya watu 32,520, hivyo haitimizi kigezo hicho cha kugawanywa, kwani kuna upungufu wa takribani watu 24,519 ili kufikia kiwango kinachohitajika kwa uanzishaji wa kata mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kigezo cha uwezo wa halmashauri kujitegemea kupitia mapato ya ndani kwa angalau kwa 20%, halmashauri ya Wilaya ya Mkalama bado haijafikia kigezo hicho. Katika mwaka wa fedha 2021/2022 ilifanyiwa tathmini kuwa uwezo wa 13%, mwaka wa fedha 2022/2023 ulikuwa 12% na mwaka wa fedha 2023/2024 ulikuwa 13%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama inashauriwa kuwasilisha maombi hayo kwa kadri ya mwongozo husika ili tathmini ya vigezo iweze kufanyika kwa maamuzi zaidi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jesca David Kishoa.

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Kwanza kabisa nianze kwa kuipongeza Serikali kwa ngazi ya wilaya kupitia vikao vya *DCC* na ngazi ya mkoa kupitia vikao vya *RCC* kwa kuchakata suala hili kwa ajili ya kugawanya kata hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na majibu ya Serikali, ninaomba kujua kwa sababu wameainisha vigezo viwili, lakini kwenye mwongozo kuna vigezo zaidi ya hivi. Hamwoni haja sasa Serikali wakatazama vigezo vingine vya ziada kama shughuli za kijamii, shughuli za kiuchumi, pamoja na suala la kijiografia kwa sababu wananchi wa kata hii wanapata adha kubwa sana kufika maeneo ya kupata huduma zao kwenye ngazi ya kata?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba majibu kwa Serikali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge amesema. Kigezo kikubwa ni idadi ya watu na uwezo wa halmashauri kujiendesha kimapato, lakini kuna vigezo vingine kwa maana ya hali ya kijiografia, umbali kutoka makao makuu ya tarafa au ya wilaya, vyote ni vigezo ambavyo wakati wa maamuzi vinatiliwa mkazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana tumeishauri halmashauri pamoja na kwamba kuna vigezo hivi viwili havijatimia lakini walete maombi yale, Serikali iendelee kufanya tathmini kwa kutumia vile vigezo vingine ili ikifaa na ikipendeza tuweze kuona namna ya kushauri mamlaka husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa sasa imeendelea kuweka kipaumbele kikubwa zaidi kuendeleza miundombinu kwenye maeneo ya utawala yaliyopo. Tuna maeneo mengi, kata nyingi hazina ofisi za kata, hazina vituo vya afya, hazina zahanati, hazina barabara na changamoto nyingi. Kwa hiyo Serikali iliona ni busara, kwa sababu

kupanga ni kuchagua, lazima tuchague jambo moja, ajenda ifike mwisho, tuje na ajenda nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Serikali iliona ni busara, kwanza kuboresha miundombinu kwenye maeneo au kata za kiutawala zilizopo sasa na baadaye tuendelee kuona uwezekano wa kuanzisha mamlaka nyingine kwa kadri itakavyowezekana. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Subira Mgalu.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo ilipata hadhi ya kuwa halmashauri ya mji na ndani ya halmashauri hiyo kuna Kata ya Mapinga ina wananchi takribani 42,543 kwa mujibu wa sensa 2022; na kwa vigezo ambavyo amesema Mheshimiwa Naibu Waziri; je, Serikali ipo tayari wakati tukisubiri hati ya kuwa rasmi halmashauri ya mji na kuelekea kufanya uchaguzi wa mitaa, kufanya mapitio ya kata hii na kuweza kuigawanya kuwa kata mbili kwa sababu ina wananchi wengi na vigezo vimekamilika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa dada yangu Subira Mgalu, Mbunge wa Jimbo la Bagamoyo kwamba zipo baadhi ya kata ambazo zinatimiza vigezo vya mwongozo wa ugawaji wa maeneo ya utawala 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala ambalo Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI tumeendelea kushauri na kusisitiza Wakurugenzi wa Halmashauri na Makatibu Tawala wa Mikoa ni kupitia taratibu hizi za kuanza vikao vya ngazi ya msingi, kwa maana ya vikao ngazi ya vijiji, kuridhia ngazi ya mitaa, ngazi ya kata, *DCC*, *RCC* na hatimaye kuwasilisha Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI ili tathmini iweze kufanyika

na kuona uwezekano wa kuelekea kwenye hatua hiyo ya kupata mamlaka mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba nimshauri tu Mheshimiwa Mgalu kwamba, Halmashauri ya Bagamoyo ianze utaratibu na iwasilishe Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mbunge wa Mlalo.

Na. 280

**Kugawanya Kata ya Manolo – Mlalo**

**MHE. RASHID A. SHANGAZI** aliuliza:-

Je, lini Kata ya Manolo yenye idadi ya Wakazi 26,000 itagawanywa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mbunge wa Jimbo la Mlalo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, uanzishwaji wa maeneo ya utawala katika Mamlaka za Serikali za Mitaa hufanyika kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), Sura 287 na (Mamlaka za Miji), Sura 288 pamoja na Mwongozo wa Uanzishwaji wa Maeneo ya Utawala wa Mwaka 2025 ambao umeainisha vigezo na taratibu zinazopaswa kufuatwa ili kugawanya na kuanzisha maeneo mapya. Kusudio hupita katika vikao ngazi ya msingi, Wilaya na Mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa mwongozo wa uanzishaji kata mpya wa mwaka 2025, kata mpya inayoanzishwa inatakiwa kuwa na idadi ya watu wasiopungua 25,000 na kata mama inatakiwa kuwa na watu wasiopungua 25,000. Kata ya Manolo iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto haijakidhi kigezo hiki ikiwa zitagawanywa kata mbili. Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi 2022, kuna jumla ya watu 25,519 hivyo kuna upungufu wa watu 24,519 ili kuunda kata mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na vigezo hivyo, kigezo kingine ni uwezo wa Halmashauri ya wilaya kujitegemea kutokana na mapato ya ndani angalau kwa 20%. Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto haijafikia kigezo hiki pia. Katika mwaka wa fedha 2021/2022, uwezo wa kujitegemea ulikuwa 19%, mwaka wa fedha 2022/2023 ulikuwa 17% na mwaka wa fedha 2023/2024 ulikuwa 15%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto inashauriwa kuwasilisha maombi hayo kwa kadri ya mwongozo husika ili tathmini ya vigezo iweze kufanyika kwa maamuzi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rashid Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na majibu haya ya Serikali, lakini ni vizuri pia wakatazama kwa kina hiki kinachoitwa kigezo cha mapato. Kwa sababu sijajua ni tathmini kiasi gani imefanyika, ile halmashauri ni miongoni mwa halmashauri tajiri kabisa yenye uwezo wa kujiendesha bila tatizo lolote, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; tunapotaka maeneo hayo ya utawala yagawanywe hatuangalii tu sababu za kiuchumi, jiografia, utawala, lakini pia tunazingatia eneo zima la utawala bora. Sasa kwa mfano, Kata hii ya Manolo ina shule za msingi tisa, ina shule za sekondari nne ndani ya kata moja ambazo kwa kweli ni mzigo mkubwa sana kwa wataalam wetu kuweza kuzisimamia. Je, Serikali haioni haja ya kutazama vigezo hivi kwa umakini zaidi ili tuweze kupata ufanisi katika eneo zima la utawala bora?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; tunalo ombi ambalo lipo Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI la kupatiwa halmashauri ya Mlalo na vigezo wakati ule wakati tunafanyiwa tathmini tulikuwa zaidi ya 67%. Sasa ninapenda kujua katika utaratibu uleule wa kurahisisha dhana nzima ya utawala bora katika halmashauri yenye shule zaidi ya 200 za msingi, shule 80 za sekondari kuigawa ili tupate Halmashauri ya Mlalo na Lushoto wabaki kuwa halmashauri ya Lushoto. Ni lini watalifanyia kazi pendekezo letu hili lililopo ofisini kwao?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nimpongeze sana Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mbunge wa Jimbo la Mlalo amefuatilia suala hili, mara kadhaa kuhitaji kuona uwezekano wa kugawa Kata hii ya Manolo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba dhamira ya Serikali, kwanza ni kuhakikisha kwamba inasogeza huduma za kijamii karibu zaidi na wananchi. Moja ya hatua ambayo inaweza kusaidia kufikisha kusudio hilo ni pamoja na kusogeza maeneo mapya ya utawala katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya vigezo ambavyo ni muhimu vizingatiwe ni ile idadi ya watu, lakini pia uwezo wa halmashauri kujiendesha. Kwa sababu kadri unavyoongeza mamlaka za utawala, unaongeza gharama za uendeshaji wa halmashauri husika. Pamoja na vigezo hivi ni kweli kwamba tuna vigezo vingine kama hali ya kijiografia, lakini pia umbali na mambo mengine na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali iko tayari kuendelea kuifanyia *assessment* Kata hii na kuona uwezekano wa kuipa mamlaka hiyo. Kama nilivyosema waendelee kuwasilisha maombi hayo ili tuweze kuona uwezekano wa kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala la pili, Wilaya ya Lushoto ni wilaya kubwa kama Mheshimiwa Mbunge alivyosema na tunafahamu kwamba dhamira ya halmashauri ya Wilaya ya Lushoto ni kupata halmashauri mbili, halmashauri ya Lushoto na halmashauri nyingine mpya. Kwa hiyo ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tunafahamu walishawasilisha maombi Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI na tunaendelea na tathmini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na tathmini ambazo zinaendelea nirejee kusema kwamba dhamira ya Serikali kwa sasa ni kuboresha kwanza maeneo ya utawala yaliyopo, lakini hapo baadaye tutaendelea na taratibu nyingine za kuona uwezekano wa kupata mamlaka mpya za wilaya ikiwepo katika Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Selemani Kakoso.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ugawaji wa madaraka kwenye maeneo ya Wilaya ya Tanganyika ni muhimu sana. Kata ya Tongwe ina wakazi 48,000, Kata ya Sibwesa ina wakazi 40,000 na Kata ya Mwese ina watu wapatao 35,000. Hao wote wanashindwa kuhudumiwa kwa sababu ya kushindwa kupata mgawanyo wa madaraka. Mheshimiwa Naibu Waziri, ni shahidi alifika kwenye Kata ya Sibwesa ambayo ina rekodi ya watoto 15 wanaozaliwa kila siku. Je, ni lini Serikali itazigawanya hizo kata ili ziweze kupata huduma inayotakiwa? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Mbunge kaka yangu Mheshimiwa Kakoso, Mbunge wa Jimbo la Katavi ambayo ni maarufu Tanganyika, kwamba tunafahamu kata hizi zina uhitaji wa kupata kata mpya ndani ya kata hizi. Pia, tunafahamu Mheshimiwa Kakoso amelifuatilia suala hili mara kadhaa, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaendelea kushauri kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika waanze utaratibu huo wa kupitia kwenye vikao vya vijiji, ngazi ya kata, ngazi ya halmashauri, Wilaya (*DCC*) na *RCC* na hatimaye wawasilishe maombi hayo Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI ili tathmini iweze kufanyika na waone uwezekano wa kupata mamlaka mpya katika maeneo hayo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Agnesta Lambert.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kuniona. Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya 2022, Kata ya Kipawa ina wakazi 72,577 na Kata ya Tabata ina wakazi 60,000 na kata hizi zote mbili kijiografia ni *very scattered*. Kwa kuwa Jiji letu la Dar es Salaam tuko vizuri kwa upande wa mapato, swali langu kwa Serikali, je, wako tayari kugawanya hizi kata mbili? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI kumwelekeza na kumsisitiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kwa maana ya Ilala, lakini pamoja na Katibu Tawala wa Mkoa wa Dar es Salaam, kuchukua hatua stahiki kwa kufuata mwongozo huu wa kuomba kupata maeneo mapya ya utawala katika kata ambazo Mheshimiwa Mbunge amezitaja ili Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI ifanye tathmini na kushauri mamlaka husika kwa kadri itakavyowezekana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cecilia Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Katika Wilaya ya Karatu na sisi tuna mahitaji ya ugawanywaji wa kata mbalimbali kulingana na ukubwa wa kata husika. Tumeshafuata mwongozo kwa maana ya Baraza la Madiwani limepitisha, vikao vya *DCC* na vikao vya *RCC* vimepitisha. Je, ni lini Serikali itafanyia kazi maombi haya ya wananchi wa Karatu ili kugawa

kata hizo kwa kuwa kugawa hizo kata ndivyo ambavyo tunarahisisha upatikanaji wa huduma kwa wananchi wetu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Cecilia Paresso, Wilaya ya Karatu ni moja ya wilaya yenye kata kubwa na ambazo ziko mbali. Ninakumbuka tumefanya ziara pale kwenye kata moja kama ninakumbuka vizuri Mbuga Nyekundu na maeneo mengine ambayo kwa kweli umbali ulikuwa ni mkubwa sana kutoka Makao Makuu ya Halmashauri ya Karatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Serikali inatambua kwamba, ziko kata ambazo zina sifa ya kupata mamlaka mpya kwa maana ya kuzalisha kata nyingine. Niwapongeze Mkoa wa Arusha na Wilaya ya Karatu kwa kufanya vikao kwa mujibu wa taratibu hizo na kuwasilisha Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutaendelea kufanyia tathmini vigezo hivyo na ikiwa inakidhi vigezo tutaendelea na hatua nyingine kwa kadri ya utaratibu uliowekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la msingi ambalo ningependa kulisisitiza ni kwamba tunafahamu, kote nchini kuna uhitaji mkubwa wa kugawa maeneo mapya ya utawala (vijiji, mitaa, kata, tarafa mikoa na kadhalika). Hata hivyo, kupanga ni kuchagua, Serikali iliona ni budi na ni vyema tuanze kwanza na kuboresha miundombinu iliyopo kwa sababu tuna upungufu mkubwa sana wa miundombinu katika mamlaka za tawala zilizopo sasa na baadaye twende na hatua sasa za kuendelea kugawa maeneo hayo. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaendelea kufanya maamuzi kwenye eneo hilo kwa kadri itakavyowezekana.

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea sasa Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana, Mheshimiwa Lucy Edward Mwakyembe, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na 281

**Mitaji na Mafunzo ya Biashara kwa Vijana**

**MHE. LUCY EDWARD MWAKYEMBE** aliuliza:-

Je, Serikali inaboresha vipi upatikanaji wa mitaji na mafunzo ya biashara kwa vijana?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAENDELEO YA VIJANA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Lucy Edward Mwakyembe, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuwawezesha vijana kiuchumi kupitia maboresho ya mifumo ya utoaji wa mikopo, mafunzo ya ujasiriamali na huduma za maendeleo ya biashara. Katika kufanikisha hilo, Serikali imefanya mapitio ya miongozo na taratibu zinazosimamia utoaji wa mikopo kwa vijana ili kuhakikisha zinakuwa rafiki, jumuishi na zinazoendana na mahitaji halisi ya vijana katika mazingira ya sasa ya kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, Serikali imeongeza kiwango cha fedha kinachotengwa kwa ajili ya mikopo kupitia Mifuko na Programu mbalimbali za Uwezeshaji ili kupanua fursa za vijana kushiriki katika shughuli za uzalishaji na kujiajiri. Aidha, Serikali imeimarisha uratibu kati ya taasisi zinazohusika na uwezeshaji wa vijana kwa lengo la kuongeza ufanisi, uwazi na matumizi bora ya rasilimali zinazotengwa kwa ajili ya maendeleo ya vijana. Hatua hiyo imewezesha kupunguza urudufu wa majukumu na kuhakikisha

huduma pamoja na fursa mbalimbali zinawafikia walengwa kwa wakati na kwa tija inayokusudiwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lucy Mwakyembe.

**MHE. LUCY EDWARD MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana ndugu yangu Hamis Mwinjuma kwa majibu mazuri ya Serikali katika kuratibu na kufanya miongozo katika upatikanaji wa mikopo kwa ajili ya vijana, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kwa kuwa Serikali imewekeza na kuhakikisha taratibu na miongozo katika utoaji wa mikopo inafanikiwa. Je, imejipangaje kusaidia upatikanaji wa masoko ndani na nje ya nchi kwa ajili ya vijana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, tunatambua Serikali imefanya tathmini ya mafunzo na upatikanaji wa mikopo hiyo. Je, Serikali imewafikia vijana waliobakia katika ngazi za mikoa na wilaya ili vijana hao kupokea tabasamu ambalo Mheshimiwa Rais ameliahidi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAENDELEO YA VIJANA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa maswali mawili mazuri ya nyongeza kutoka kwa Mheshimiwa Mbunge, Lucy Mwakyembe, ninaendelea kumtia moyo aendelee kuwapigania vijana wa Kitanzania, anafanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijielekeza kwenye maswali yake mawili ya nyongeza, la kwanza lilikuwa kuhusiana na suala la masoko ndani na nje ya nchi. Vijana wengi waliopata mikopo hii wamekuwa wakipatiwa tenda na Serikali kupitia halmashauri zao kupitia mfumo wa *NeST*. Mfano, vijana kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi kule ambao wana kiwanda cha chaki, wao wanasambaza chaki karibu nchi nzima. Vilevile, wako ambao wanasambaza madawati, wako wanaosambaza matofali na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaendelea kukusanya maoni na kuhakikisha kwamba masoko kwa vijana ambao wanapatiwa fedha hizi zilizotolewa na Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, hayawi tatizo na hayawi kikwazo kuhakikisha kwamba lengo la Mheshimiwa Rais linafikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye masoko ya kimataifa, Serikali iko katika hatua za mwisho za kutengeneza mfumo, *Youth Empowerment System (YES)*, ambayo yenyewe itakuwa inaunganisha wizara zote za kisekta na mashirika yasiyo ya Kiserikali ambayo yatakuwa na fursa zinazowahusu vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo huu utakapokamilika, utawaunganisha vijana wote ambao watakuwa wamejisajili na fursa zote zitakazokuwa zinapatikana kupitia Serikalini ama Mashirika Yasiyo ya Kiserikali zitakuwa zinapatikana kwenye mfumo huu, iwe ni fursa za masoko ya kimataifa ama ya kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili, lilikuwa tathmini kuhusu kama zinafika wilayani na mikoani. Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana, limekuwa ni zoezi linaloendelea. Kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wote watakuwa wameona kwamba uboreshaji wa suala la utoaji wa mikopo kwa vijana unafanyika kila wakati. Mathalani, kutokana na tathmini ambazo zimekuwa zikifanyika wilayani na mikoani, unaona sasa riba ya mikopo hii imepungua mpaka asilimia tano. Kile kipindi cha neema kutoka miezi mitatu mpaka sita, lakini kwenye miradi maalum ya kimkakati, kwa mfano, ufugaji na uvuvi kinakwenda mpaka asilimia nane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiasi cha fedha ambacho kinatolewa Mheshimiwa Rais alikiongeza mpaka kufikia shilingi 200,000,000,000, lakini wanufaika sasa hivi wamekuwa mpaka mtu mmoja mmoja badala ya kutilia mkazo kwenye vikundi kama ilivyokuwa awali na maboresho mengi mengine yamefanyika. Hii inaonyesha kwamba Serikali inaendelea kufanya tathmini kwenye ngazi za chini kabisa kwenye wanufaika ili kuhakikisha kwamba mikopo hii inakwenda kuleta tija.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko na Mheshimiwa Dkt. Regina Malima, maswali mafupi ya nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwenye shilingi 200,000,000,000 za Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa siku 100, Serikali ilitoa tangazo la vijana kuomba mikopo na ikaweka ukomo wa umri wa miaka 18 mpaka 35.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukizingatia takwimu za mwaka 2024 zinaonesha kwamba vijana kati ya umri wa miaka 35 mpaka 40 ni takriban 4,000,000 na kundi hili ni kundi muhimu sana ambalo limejiajiri kwenye sekta isiyo rasmi na ujasiriamali mdogo mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninataka kujua Serikali ilifanya tathmini gani ya kiuchumi na kijamii ambayo ilisababisha kuweka huu ukomo badala ya kutanua ukomo mpaka umri wa miaka 40 ambapo hata taasisi mbalimbali ikiwemo *IPU*, kwetu Chama Cha Mapinduzi kimeongeza umri mpaka miaka 40 ili wanufaika waweze kupata wigo mkubwa kuongeza ajira na tija kwa Watanzania? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru, swali zuri la Mheshimiwa Esther Matiko. Ni ukweli kwamba Serikali imepokea maoni mengi kuhusiana na ukomo wa umri ambao unastahili kunufaika na mikopo hii ya vijana na tunaendelea kulifanyia kazi jambo hili. Maoni yamekuwa mengi na inaonekana kundi la miaka 35 mpaka 40 linapaswa kuhusishwa kwenye mikopo hii na tunafanyia kazi jambo hili.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Regina Malima.

**MHE. DKT. REGINA C. MALIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa vijana wengi wanaomaliza vyuo na vyuo vikuu huwa na mawazo bunifu lakini mara zote hukosa mitaji. Je, Serikali iko tayari kutengeneza

mfumo wa kuwasaidia vijana hawa wenye mawazo bunifu kuwapatia mitaji ili waweze kujiajiri? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nilisema wakati ninajibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Lucy Mwakyembe, Serikali iko katika hatua za mwisho za kukamilisha *a one-stop center*, mfumo unaoitwa *Youth Empowerment System* ambao pamoja na mambo mengine itakuwa ni hii ya kuhakikisha kwamba vijana ambao wana mawazo mazuri ya ubunifu wanapatiwa mitaji na kuweza kuyafanya mawazo hayo kwa vitendo na kuhakikisha kwamba Serikali inawaletea tabasamu kama ambavyo Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, ameelekeza Serikali yake ifanye. Ninakushukuru.

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge kutoka Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana.

Tunaendelea sasa na Wizara ya Uchukuzi, Mheshimiwa Dkt. Damas Daniel Ndumbaro, Mbunge wa Songea Mjini, aulize swali lake.

Na. 282

**Ujenzi wa Jengo la Abiria Uwanja wa Ndege Songea**

**MHE. DKT. DAMAS D. NDUMBARO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa jengo la abiria Uwanja wa Ndege wa Songea?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Damas Daniel Ndumbaro, Mbunge wa Songea Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ipo katika hatua za mwisho za kufanya maboresho ya jengo lililokuwa likitumiwa na mkandarasi ili liweze kutumika kwa muda kama jengo la abiria, hatua itakayosaidia kuimarisha utoaji wa huduma za usafiri wa anga wakati maandalizi ya utekelezaji wa miundombinu ya kudumu yakiendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali inaendelea na taratibu za upatikanaji wa fedha kwa ajili ya ujenzi wa jengo jipya la abiria kwa lengo la kuongeza uwezo wa kuhudumia abiria, kuboresha ubora wa huduma na kukuza mchango wa sekta ya usafiri wa anga katika maendeleo ya uchumi ya eneo husika na Taifa kwa ujumla.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro.

**MHE. DKT. DAMAS D. NDUMBARO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninampongeza Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri yenye kuleta moyo kwa Wanasongea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maswali mawili ya nyongeza; swali la kwanza, kwa kuwa Songea ni mbali kutoka Dar es Salaam na maeneo mengine. Ni lini sasa Serikali itaweka huduma ya mafuta ya ndege pale uwanjani pamoja na usafirishaji wa mizigo ya wakulima? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa uwanja ule unahudumia nchi za jirani pamoja na mikoa ya jirani; ni lini sasa Serikali itaongeza miruko ya ndege kutoka mitatu kwa wiki kwenda mitano kwa wiki? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tunakubaliana na Mheshimiwa Ndumbaro, kwamba kwa uwanja ule na kwa *traffic* inavyongezeka, iko haja ya kujenga mifumo ya mafuta

kwa ajili ya kuhudumia ndege. Kwa kulitambua hilo, tayari *(TAA)* imeanza kufanya mchakato wa kupata mwekezaji ama mkandarasi ambaye atafanya kazi hiyo ya kujenga mifumo ya mafuta ya ndege. Kazi hiyo itachukua kati ya miezi sita mpaka miezi nane kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kama alivyosema Mheshimiwa Ndumbaro ni kweli kwa sasa mpaka wiki iliyopita *Air Tanzania* ilikuwa inafanya *frequency* tatu au miruko mitatu kwa wiki. Jumapili iliyopita tulianzisha *frequency* ya nne ambayo sasa tunafanya *route* nne kwa wiki na bahati nzuri sana hii *route* ya Jumapili imeonyesha matokeo makubwa kwani mara baada ya kuanzishwa *load capacity*, yaani ujazo wa ndege umeongezeka hadi kufikia 56%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikawaida haitokei hivyo, *route* ya kwanza huwa inachukua muda mrefu ku-*peak,* lakini hii imefanya vizuri. Kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Ndumbaro na wananchi wote kwamba tutaendelea kuisoma hii kwa muda wa miezi miwili, ikiwa itaendelea kufanya vizuri tutaongeza *route* ya tano kwa njia ile. Ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tinnar Chenge, swali fupi la nyongeza.

**MHE. TINNAR A. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kuniona. Kwa kuwa ni muda mrefu sasa wananchi wa Kijiji cha Igegu, Bariadi, wameachia maeneo yao kupisha ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Mkoa wa Simiyu na kwa kuwa hawaruhusiwi kuyaendeleza maeneo hayo. Je, ni lini Serikali itaanza kujenga uwanja huu muhimu kwa uchumi na utalii wa Mikoa ya Kanda ya Ziwa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli wananchi wa Simiyu pamoja na Bariadi wametoa baadhi ya maeneo kwa ajili ya kujenga kiwanja cha ndege. Kwa sasa Serikali tunafanya *feasibility study* ili kuona jinsi gani tutaweza kuujenga kiwanja hicho na kiwanja

chenyewe kiwe na ukubwa gani. Baada ya hapo tutatafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa kiwanja hicho.

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana Mheshimiwa Waziri, Wizara ya Uchukuzi, kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Kilimo. Mheshimiwa *Engineer* Ramadhani Hamza Singano, Mbunge wa Bumbuli, aulize swali lake.

Na. 283

**Utafiti wa Fursa za Kilimo cha Umwagiliaji – Bumbuli**

**MHE. RAMADHANI H. SINGANO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kitafiti wa kuhakikisha fursa ya kilimo cha umwagiliaji inapewa kipaumbele kwa kata za Bumbuli?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inaendelea kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa Mradi wa Kwanguruwe wenye ukubwa wa hekta 520. Mradi huu unajumuisha *scheme* ndogo saba ambazo ni Mkumbulu A, Mkumbulu B, Kwambogolo, Kwambuguni, Mwamba, Kigunga na Makunguu ambapo utekelezaji wake umefikia wastani wa 80%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kukamilika kwa usanifu mradi huu utajumuishwa kwenye mpango wa ujenzi wa miradi ya umwagiliaji na unatarajiwa kunufaisha wakulima zaidi ya 2,000 baada ya kukamilika kwake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imetambua maeneo ya Bumbuli, Mbokoi, Manga, Galamba, Tanda, Kwemhafa, Nkamai, Kweminyasa, Mahange,

Mponde, Ngugui, Mayo, Dule, Malomboi, Mgwashi, Sagala pamoja na Baga kwa ajili ya kuendeleza kilimo cha umwagiliaji katika Halmashauri ya Bumbuli.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Engineer* Ramadhani Singano, swali la nyongeza.

**MHE. RAMADHANI H. SINGANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nipongeze majibu mazuri ya Serikali; majibu ambayo yanaleta tabasamu kwa wananchi wa Bumbuli ambao saa hizi wanasikiliza Bunge la Tanzania, lakini nina swali moja la nyongeza na ushauri mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti Mabonde ya Kwabulu na Kwakongo Kata ya Milingano ni mabonde yenye mito ya uhakika ambayo hufika mahali na kuharibu miundombinu ya barabara. Je, Serikali haioni ni muda muafaka sasa kujenga mabwawa kwa ajili ya kunufaika na kilimo cha umwagiliaji, lakini pia kuzuia uharibifu huu wa miundombinu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu, Kata ya Usambara kuna maeneo pia ya Kiviricha na Kwampunda, lakini katika Kata ya Makanya, Jimbo la Lushoto, kuna maeneo ya Kijiji cha Mdando, Bonde la Muheza, lakini Kitivo na Kwemsaa, Kijiji cha Bombo. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, swali moja.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimthibitishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba katika maelekezo ambayo Mheshimiwa Rais alitupatia, kuhakikisha maeneo yote yanayofaa kwa kilimo; Wizara ya Kilimo kupitia tume tunayafikia na kuhakikisha kwamba tunatafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa miradi katika maeneo hayo. Kwa hiyo, hata haya maeneo ya Kwampuli na hilo lingine ambalo Mbunge ameliainisha hapa ni maeneo ambayo yapo katika mpango wetu ambapo yanakwenda kujengwa mabwawa kwa ajili ya kunufaisha wakulima katika muda wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, jukumu letu sisi kama Wizara ni kuhakikisha sasa miradi yote inatekelezeka baada ya kuwa na fedha za uhakika ambazo sasa zitakwenda kufanya kazi hii ambayo Mheshimiwa Rais ametuelekeza. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami ninakushukuru niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Mheshimiwa Waziri, Wakala wa Mbegu wa *ASA* wana hekta 17,000, ni hekta 3,785 pekee yake ndiyo zina mtandao wa umwagiliaji. Ni lini sasa Serikali itahakikisha hekta zote 17,000 zinapata umwagiliaji ili wakala wa mbegu wa Serikali awe na uhakika wa kuzalisha mbegu kwa wingi kwa kuzalisha kwa msimu mara mbili? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda nimpongeze Mheshimiwa Ester Bulaya, Mbunge wa Bunda Mjini, kwa swali zuri na la msingi na kama mwekezaji katika mashamba ya *ASA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo moja tu ambalo ninamhakikishia, Serikali inafanya kazi kwa hatua na katika hatua ya kwanza ndiyo tumeanza katika hizi hekta 3,785. Tunamhakikishia kwamba tutamaliza hekta zote zilizobakia karibu hekta 13,000 na kitu kwa sababu zote zipo katika mpango. Tuna miradi mingi juu ya utekelezaji wa mradi huu ikiwemo miradi ambayo haipo kwenye bajeti, lakini vile vile katika miradi ambayo tunapata fedha kutoka nje. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwita Getere, swali fupi la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru, katika Wilaya ya Bunda tuna *schemes* za umwagiliaji mbili, kuna *Scheme* ya Maliwanda na *Scheme* ya Kisangwa. Hizi *schemes* zimeshawekewa bajeti kwenye Wizara ya Kilimo na mwaka jana tuliambiwa hii kazi ya ujenzi wa hizi *schemes* mbili ungeanza. Je, Waziri yuko tayari tukutane leo na wataalam wake wa umwagiliaji

tukiwa na Mbunge wa Bunda Mjini ili tuweze kuhakiki kwamba hiyo *project* inaendelea au imeshakufa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na swali lake la msingi, tuko tayari, shughuli hiyo ya kukutana mimi pamoja na tume tutaifanya leo mchana baada ya Bunge lako Tukufu kuahirishwa. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Asha Omar Rashid, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 284

**Upatikanaji wa Nishati ya Gesi Vijijini**

**MHE. ASHA OMAR RASHID** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha upatikanaji wa nishati ya gesi vijijini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

MheshimiwaMwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Asha Omar Rashid Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha nishati ya gesi inawafikia na kuwanufaisha Watanzania wengi zaidi, Serikali kupitia Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania *(TPDC)* inaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya usambazaji gesi asilia ambapo hadi kufikia Aprili, 2026, jumla ya nyumba 2,512 zimeunganishwa na

miundombinu ya gesi asilia katika Mikoa ya Mtwara ambapo kuna nyumba 425 Mkoa wa Lindi 677, Pwani 530 na Dar es Salaam 880.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini *(REA)* inaendelea kutekeleza Mradi wa Kusambaza Mitungi 452,445 ya gesi oevu (*LPG)* ya kilogram sita kwa bei ya ruzuku ya 50% ili kuendelea kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia maeneo ya vijijini na vijiji-miji. Vilevile, Serikali inaendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika miundombinu ya kusambaza gesi ya *LPG* maeneo ya vijijini na vijiji-miji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na miradi hiyo inayotekelezwa bado Serikali inaendelea kufanya tafiti katika maeneo ya mijini na vijijini ili kubaini aina sahihi ya miundombinu inayohitajika kwa ajili ya kufikisha na kusambaza gesi asilia kwa ufanisi zaidi. Matokeo ya tafiti hizo yatawezesha kubainisha njia bora za usambazaji wa gesi asilia katika maeneo husika, kulingana na kiwango cha mahitaji. Vilevile, utafiti huo utaibua fursa ya kuanzishwa kwa miradi mingine ya usambazi wa gesi asilia itakayotekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi ili kuhakikisha nishati hiyo inawafikia na kuwanufaisha Watanzania wengi zaidi mijini na vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asha Omar Rashid.

**MHE. ASHA OMAR RASHID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini ninayo maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; pamoja na kuweka ruzuku kwenye gesi inayouzwa kwenye mitungi, lakini bado bei ya gesi ni ghali kiasi ambacho mwananchi mwenye kipato cha chini hawezi kumudu huduma hii. Je, Serikali ina mpango gani wa kufanya utafiti zaidi ili kuja na suluhisho la bei yenye unafuu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; je, Serikali ni lini itaongeza vituo vya kujaza gesi karibu na wananchi badala ya kusubiri mitungi kuletwa madukani? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Asha anawawakilisha vizuri wananchi wa Mkoa wa Kaskazini na wapigakura wake wa Mkoa wa Kaskazini Pemba na Mheshimiwa Asha amekuwa pamoja na sisi katika kuhakikisha tunatatua changamoto ya matumizi ya nishati ambayo siyo rafiki kwa mazingira na afya za wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kupunguza gharama za gesi majumbani na kuwezesha upatikanaji wake kwa wananchi wengi zaidi. Serikali imeondoa kodi ya ongezeko la thamani (*VAT)* kwenye gesi ya *LPG* na mitungi ya gesi pamoja na kuondoa kodi ya ushuru wa forodha pia kwa baadhi ya vifaa vya *LPG*. Hata hivyo, tumeendelea kuwahamasisha wadau mbalimbali waweze kusambaza gesi. Nichukue fursa hii kuwahamasisha vijana kuchukua kama fursa wajiunge kwenye vikundi ili kuweza kuwafikia wananchi kwa karibu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye swali lake la pili, Serikali inachukua mikakati mbalimbali kuhakikisha kwamba tunawafikia wananchi wasitembee umbali mrefu kupata gesi na kwa kufanya hivyo mpaka sasa Serikali imeweza kusambaza mitungi ya gesi zaidi ya 500,000 na imeweza kusambaza majiko banifu zaidi ya 300,000. Hizi ni jitihada mbalimbali ambazo Mheshimiwa Rais amehamasisha akiwa kama kinara wa wa nishati safi ya kupikia nchini Afrika na duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zainab Kawawa.

**MHE. ZAINAB R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Mikoa ya Lindi na Mtwara ndiyo ipo karibu sana na nishati ya gesi inakopatikana, lakini kinachoshangaza gharama ya gesi hasa ya kwenye mitungi haina tofauti na gharama ya maeneo mengine ambayo ni ya mbali. Sasa katika mikakati yenu ya kuhakikisha kwamba bei inapungua ya gesi kwa nini tusipunguze kwanza bei kulingana na umbali wa mahali ambapo gesi

inapatikana? Kwa sababu imekuwa tatizo hasa kwa akina mama, Serikali imewapa mitungi ya gesi mingi, lakini akishatumia gesi mara moja ikiisha hawezi tena kununua gesi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Zainab Kawawa kwa swali zuri na nimhakikishie kwamba, bei ambayo wananchi wananunua mitungi ya gesi imepungua kwa zaidi ya 50% kwa sababu Serikali imeweka ruzuku katika mitungi hiyo ya gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingesema inunuliwe kwa bei halisia ya uagizaji wa gesi ingekuwa ni changamoto na tusingefikia lengo letu la kuhakikisha tunawafikia zaidi ya 80% ya wananchi itapofika mwaka 2030. Pia, nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kwa Mikoa ya Lindi na Mtwara ili kuwapa nafuu kwa sababu bomba la gesi linatoka kule tunajitahidi kuunganisha gesi majumbani kwa kutumia bomba la gesi. Hiyo itawafanya wananchi wengi wa Lindi na Mtwara waweze kunufaika kwa kutumia gesi ya bei nafuu ambayo inatokana na bomba la gesi na pengine wasipate athari kubwa ya kuendelea kutumia gesi ya mitungi. Ninakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ninakushukuru sana kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, swali la Mheshimiwa Joshua Samwel Nassari, Mbunge wa Arumeru Mashariki litaulizwa na Mheshimiwa Isack Joseph, Mbunge wa Monduli.

Na. 285

**Ujenzi wa Barabara ya *By Pass* Tengeru – Mererani**

**MHE. ISACK J. COPRIANO K.n.y. MHE. JOSHUA S. NASSARI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani mahsusi wa kutengeneza Barabara ya *Bypass* Tengeru - Mererani Mkoani Arusha?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Joshua Samwel Nassari, Mbunge wa Arumeru Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa Barabara ya Mchepuo ya kutoka Tengeru hadi Mererani yenye urefu wa kilometa 28 inayounganisha Mikoa ya Arusha na Manyara ambayo ni njia mbadala ya Barabara ya Arusha – Moshi na kiungo muhimu kuelekea Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro. Tayari Serikali imekamilisha kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya kuijenga barabara hii kwa kiwango cha lami na barabara hiyo imeingizwa katika mpango wa bajeti ya mwaka wa fedha 2026/2027 kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Isack Joseph.

**MHE. ISACK J. COPRIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa tunajua fika wote kwamba 2027 tutakuwa na mashindano hayo makubwa na ukizingatia barabara ile ya kutoka Bomang'ombe kwenda Arusha ina njia ambayo kimsingi inatumiwa na watalii na tutakuwa na *route* nyingi ambazo zitakuwa na wachezaji na kadhalika. Je, mpaka sasa ni nini kinazuia barabara hiyo isitangazwe ili ujenzi huo uanze kama Mheshimiwa Waziri Mkuu alivyotoa maelekezo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niungane na Mheshimiwa Mbunge kuhusu suala hilo na sisi katika mipango ya kawaida tumeipanga kwenye bajeti ijayo. Ninakumbuka katika ziara pia aliyofanya Mheshimiwa Waziri Mkuu katika Mkoa wa Arusha ilikuwa ni moja ya maagizo ambayo aliagiza Serikali kuijenga hiyo barabara ambayo inaweza kuwa msaada mkubwa kama njia

mbadala kipindi cha *AFCON* ili tuwe na njia mbili kwa maana hiyo ya *KIA* - Mererani kwenda Tengeru pamoja na hiyo Barabara ya kutoka Bomang'ombe - USA kwenda Arusha Mjini ili iweze kuwa rahisi kipindi cha *AFCON*. Kwa hiyo, hiyo kazi inafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishe pia Mheshimiwa Mbunge kwamba pamoja na hizo barabara tuna barabara ambazo ziko katikati ya mji ambazo tayari tumeshaanza zingine tumetangaza na zingine tayari ujenzi umeshaanza ili kurahisisha usafiri katika Mji wa Arusha wakati wa *AFCON*.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali Mheshimiwa Dkt. Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijini.

Na. 286

**Ujenzi wa Barabara ya Kyetema – Katoro – Kyaka**

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA** aliuliza:-

Je, lini ujenzi wa Barabara ya Kyetema – Kanazi – Ibwera - Katoro hadi Kyaka ambayo ipo kwenye Ilani ya CCM kwa mara ya pili utaanza?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Kyetema – Kanazi – Ibwera – Katoro hadi Kyaka yenye urefu wa kilometa 60.7 ni barabara ya mkoa inayohudumiwa na Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)*. Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami umekamilika. Aidha, Serikali imeanza na kazi ya kujenga Daraja la Kalebe lenye urefu wa meta 60

ambalo lilikuwa kikwazo kikubwa katika barabara hiyo ambapo utekelezaji wake umefikia 90%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya Kanazi – Kalonge kilometa 10 zinaendelea kwa sehemu zilizobaki, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara hiyo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Jasson Rweikiza. Jaribu kuwasha na kuzima.

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi niulize maswali ya nyongeza. Swali la kwanza; ninapenda kujua iwapo Serikali inafahamu umuhimu wa barabara hii? Kwamba ni barabara ya ulinzi inaunganisha mpaka Uganda na Rwanda hata vita ya mwaka 1972 na 1978 ilipigwa kupitia barabara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; upembuzi yakinifu na usanifu wa kina umefanyika na kukamilika miaka mingi iliyopita sasa kwa gharama kubwa sana mabilioni kadhaa ya shilingi, lakini barabara hii imekuwepo kwenye Ilani ya CCM mwaka 2015, mwaka 2020 na mwaka wa jana 2025 dalili za kujenga hata chembe hakuna. Ninafahamu CCM haidanganyi watu, Serikali haiwezi kudanganya watu. Tatizo ni nini kwa nini barabara hii haijengwi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba Mheshimiwa Mbunge arudie swali lile la kwanza maana sikulipata vizuri ili niweze kumjibu vizuri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Jasson kwa ufupi. Mheshimiwa Naibu Waziri hukuelewa vizuri?

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Swali la kwanza nimesema, je, Serikali inafahamu umuhimu wa

barabara hii kwamba huko inakoelekea inaunganisha na Nchi ya Uganda na Nchi ya Rwanda na hata vita ambako mwaka 1972 Vita ya Iddi Amini na 1978 ilipigwa kupitia barabara hii?

**MWENYEKITI:** Swali lako?

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA:** Swali la pili …

**MWENYEKITI:** Umemwelewa Mheshimiwa Waziri? Uliza swali ili akuelewe maana maelezo ukiuliza swali anashindwa kuelewa, uliza swali.

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali inafahamu umuhimu wa barabara hii?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu maswali mawili kwa pamoja ya Mheshimiwa Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaelewa sana umuhimu wa barabara hii na ndiyo maana ipo na inahudumiwa na ndiyo maana hata tumeifanyia usanifu na tunatambua kwamba hii barabara kama itakamilishwa itakuwa kwanza ni njia ambayo itasaidia watu wanaokwenda Karagwe ama kwenda Mtukula, ni njia ya mkato na ndiyo maana hata katika jibu letu la msingi tulikuwa na daraja ambalo ni kikwazo sana Mheshimiwa anajua tumejenga kwa awamu, tunalikamilisha tukijua kwamba hiyo barabara ni ya muhimu sana. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge barabara hii ni muhimu, ndiyo maana hata tumetenga bajeti kuanza kuijenga kwa awamu hizo kilometa 10 kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali ya Mheshimiwa Shaffin Ahmedali Sumar, Mbunge wa Uyui.

Na. 287

**Ujenzi wa Barabara ya Tabora Mjini – Ibiri – Usagali – Ulyankulu**

**MHE. SHAFFIN A. SUMAR** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Barabara ya Tabora Mjini – Ibiri – Usagali hadi Wilaya ya Ulyankulu kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Shaffin Ahmedali Sumar, Mbunge wa Uyui, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa Barabara ya Tabora Mjini – Ibiri – Usagali hadi Ulyankulu yenye urefu wa kilometa 90. Baada ya usanifu kukamilika na gharama za ujenzi kujulikana, Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya ujenzi. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shaffin Ahmedali Sumar.

**MHE. SHAFFIN A. SUMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Ninaomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa Serikali imeshapanga kufanya usanifu wa barabara hii; je, ni kiasi gani cha fedha kimepangwa katika bajeti ambayo tunaitegemea kuipitisha ya mwaka wa fedha 2026/2027? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa ahadi ya Mheshimiwa Rais ni maelekezo kwa Serikali na kwa kuwa Mheshimiwa Rais wetu mpendwa, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alishatuahidi sisi Wanatabora hasa Wilaya ya Uyui kwamba atatujengea barabara ambayo inaanzia Magiri kupitia Nsimbo na kuelekea Kigwa na kwa kuwa barabara hii ni kilometa 27 tu na kwa kuwa barabara hii inapunguza mzunguko wa wasafiri kutoka Kigwa

kuelekea Tabora kwa ajili ya kwenda Nzega ambayo ni kilometa 70 na kwa kuwa barabara hii iko chini ya *TARURA* kwa sababu kuna ahadi ya Serikali, Wizara haioni umuhimu wa kuichukua barabara hii na kuitekeleza ili kulinda heshima ya Mheshimiwa Rais?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mheshimiwa Shaffin Ahmedali Sumar, Mbunge wa Uyui, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba hii barabara ambayo ya kwanza bado hatujakamilisha usanifu wake, usanifu unaendelea na tukishakamilisha ndiyo tunaweza tukajua gharama halisi ya hiyo barabara ambayo pia itahusisha uthamini wa mali kwa watu ambao watapisha na ndiyo bado baada ya hapo tunaweza tukaja sasa na gharama na tutakavyoanza kuitengeneza hiyo barabara. Kwa hiyo, tuko tunakamilisha hiyo barabara na kwenye bajeti ataiona hiyo barabara tumeitengea nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili, ninaomba nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba sasa hivi ni kweli kwamba wananchi wengi na magari mengi ambayo yanakwenda Kanda ya Ziwa tumeona yanapita sana kutokea Manyoni kwenda Tabora na kumekuwa na msongamano mkubwa sana katika Mji wa Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa sasa ni kwamba tumekuwa tukitoa maelezo kwamba sasa hivi kupunguza misongamano katika miji ni kutengeneza barabara za michepuko. Wabunge watakubaliana na mimi hata hapa Dodoma hii leo baada ya magari kuanza kupita barabara ya mzunguko, malori sasa hivi hayaonekani hapa mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishe Mheshimiwa Mbunge tulishapokea kama Wizara maombi ya Mkoa wa Tabora kuanza kuisanifu, lakini ninaomba kwanza ipandishwe hadhi kwa sababu inahudumiwa na wenzetu wa *TARURA*, kupandishwa hadhi na

utaratibu ni kwamba timu itakwenda ikajiridhishe na kumshauri Mheshimiwa Waziri namna ya kuipandisha na itaanzia wapi kwenda wapi ili iweze sasa kusanishiwa na kupandishwa hadhi ikiwa kama njia ya mkato ama *bypass* kwa Mji wa Tabora kwa magari yanayotoka Manyoni kwenda Tabora lakini ambayo yanaelekea Kanda ya Ziwa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa tulishapokea hayo maombi na liko linafanyiwa kazi. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ninashukuru sana kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Mheshimiwa *Engineer* Amosy William Maganga, Mbunge wa Sikonge, aulize swali lake.

Na. 288

**Ujenzi wa Ofisi Mpya ya Polisi – Sikonge**

**MHE. ENG. AMOSY W. MAGANGA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Ofisi mpya ya Polisi Wilaya ya Sikonge?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ninapenda kujibu swali namba 288 la Mheshimiwa *Engineer* Amosy William Maganga, Mbunge wa Sikonge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mpango wa kujenga Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Sikonge, kwenye kiwanja kitalu namba 817 chenye ukubwa wa meta za mraba 12,329 kilichopo katika eneo la Isungilunde. Fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho zinatarajiwa kutengwa kwenye bajeti ya Serikali ya mwaka wa fedha 2027/2028.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Engineer* Amosy William Maganga.

**MHE. ENG. AMOSY W. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. kwanza nimshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini pamoja na shukurani hizo nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; katika Kata yetu ya Kiloleli na hususani kwenye Kijiji hicho hicho cha Kiloleli, shughuli za kiuchumi na kijamii zinakuwa kwa kasi sana na hivyo kuvutia wafanyabiashara wengi pamoja na mitaji yao kwenda katika eneo hilo, lakini kata hii imekuwa haina Kituo Kidogo cha Polisi. Je, Serikali haioni kwamba, kuna haja sasa ya kujenga Kituo Kidogo cha Polisi katika kata hiyo, ambacho vilevile kitaweza kuhudumia kwenye Kata jirani tatu za Ngoywa, Usunga pamoja na Kipanga? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; Wilaya yetu ya Sikonge ina tarafa mbili, kuna Tarafa ya Sikonge na e Tarafa ya Kiwele. Tunacho Kituo Kidogo cha Tarafa ya Kiwele ambacho kipo umbali wa takribani kilometa 200 kwenda kwenye kituo kilichopo Sikonge, lakini kwa bahati mbaya sana kituo hiki hakina usafiri. Je, Serikali haioni haja ya kupeleka angalau gari moja, ili kusudi askari wetu kule waweze kufanya kazi kwa ufanisi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninaomba nimpongeze sana Mbunge, Mheshimiwa Amosy, kwa kuunganisha dhana ya maendeleo ya watu na uchumi, lakini pia, usalama wa maendeleo, ambayo yanatekelezwa katika jimbo lako na utayari wa kuwatetea wananchi, ili wawe salama pamoja na mali zao. Ninakushukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa zaidi tunaelewa kuwa, mpango wa Serikali ambao ni wa miaka mitano tumeanza, unaishia mwaka 2030 wa kujenga vituo katika ngazi ya kata 698 na pia, tunamalizia kujenga vituo vya *Grade B* katika ngazi ya wilaya 75, lakini katika mikoa mitano iliyobaki tutajenga Ofisi tano za Polisi *Grade A*. Tunamhakikishia kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI na pia, halmashauri yake, Mkurugenzi na wadau waliopo kwa kuona umuhimu wa kituo hiki tunamhakikishia tutakwenda kujenga kwa uharaka, ili tulete amani, utulivu na usalama wa mali za watu pamoja na watu wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa swali la pili; tunafahamu una kata mbili na tumewiwa na umbali alioutaja wa kilometa 200 kutoka makao makuu ya wilaya mpaka kwenye Tarafa hii ya Kiwele. Ninaomba nimhakikishie, nitapeleka ushauri huu na maombi haya kwa Waziri aweze kushughulikia, tutafanya mawasiliano naye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Othman Maulid Suleiman, Mbunge wa Mahonda.

Na. 289

**Kuweka Namba ya *NIDA* Kwenye Cheti cha Kuzaliwa**

**MHE. OTHMAN MAULID SULEIMAN** aliuliza:-

Je, Serikali haioni haja ya kuweka Namba ya *NIDA* kwenye Cheti cha Kuzaliwa kuliko kusubiri mtu mpaka atimize miaka 18?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ninapenda kujibu Swali Namba 289, la Mheshimiwa

Othman Maulid Suleiman, Mbunge wa Jimbo la Mahonda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa kuwa na namba moja ya utambulisho kwa wananchi wote kuanzia umri wa kuzaliwa hadi kufa, ili kuimarisha utambuzi pamoja na kuwa rejesta ya taarifa za matukio muhimu ya binadamu. Maelekezo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa *NIDA* ni kutoa Namba ya Utambuzi wa Kipekee kwa watu wote wanaoishi nchini kuanzia umri wa kuzaliwa, ambayo itawekwa katika Cheti cha Kuzaliwa na itatumika katika utambulisho wa wananchi katika kupata huduma mbalimbali za kiuchumi na kijamii kwa Taasisi za Umma na Binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na taratibu za kufanya marekebisho ya Sheria ya Usajili na Utambuzi wa Watu, Sura 36, katika Kifungu cha 7(1), ili kuwezesha usajili na utambuzi wa watu kuanzia umri wa kuzaliwa na hivyo kutoa namba ya utambulisho ya kipekee, ambayo itawekwa katika Cheti cha Kuzaliwa. Aidha, Serikali imeandaa mpango wa majaribio ya usajili na utambuzi wa watoto, kwa ajili ya kutoa Jamii Namba katika Wilaya ya Rungwe, Mbeya, Kilolo, Iringa na Kusini Unguja, ambao utaanza kutekelezwa baada ya marekebisho ya Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha mpango wa utoaji wa Jamii Namba unakuwa endelevu, Serikali ina mpango wa kuunganisha majukumu ya usajili wa matukio muhimu ya binadamu ya Wakala wa Usajili, Udhamini na Ufilisi *(RITA)* na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa *(NIDA),* ili kuwezesha majukumu ya usajili, utambuzi wa watu na majukumu ya usajili wa matukio muhimu ya kibinadamu kutekelezwa chini ya taasisi moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo lake ni kuongeza ufanisi na kupunguza usumbufu kwa wananchi wa kutafuta huduma zinazofanana katika taasisi mbili tofauti. Aidha, uamuzi huo utawezesha utekelezaji wa mpango wa kuweka Jamii Namba katika Cheti cha Kuzaliwa cha mtoto na hivyo, kuongeza tija na ufanisi katika usajili na utambuzi wa watu wote wanaoishi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Othman Maulid Suleiman.

**MHE. OTHMAN MAULID SULEIMAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali langu la kwanza; kwa kuwa, mpango huu ni mzuri sana kwa Taifa letu. Je, ni lini unatarajiwa kukamilika kwa manufaa mapana ya wananchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; Tanzania yetu ni nchi kubwa sana. Je, mpango huu umo katika Bajeti ya Serikali? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; mpango huu utaanza kutekelezwa mara baada ya mabadiliko ya Sheria, ambayo nimeyaeleza kwenye swali langu la msingi yatakavyokamilika. Kama tunavyofahamu Vitambulisho vya *NIDA* kwa Sheria yetu ya sasa hutolewa kwa watu wenye umri wa miaka 18 na kuendelea na vizazi na vifo maana yake ni kuanzia umri wa sifuri. Hivyo, mara baada ya kupokea majukumu haya kutoka Wizara ya Katiba na Sheria tutafanya mabadiliko madogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuunganisha na swali la pili, je, ipo katika bajeti; ni ukweli Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2026/2027 imezingatia mabadiliko haya na shughuli hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Maji. Mheshimiwa Charles Jacob Sungura, Mbunge wa Handeni, aulize swali lake.

Na. 290

**Kukamilisha Mradi wa Maji Segera – Kabuku**

**MHE. DKT. CHARLES J. SUNGURA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Mradi wa Maji wa Segera – Kabuku wenye thamani ya shilingi bilioni 25?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Charles Jacob Sungura, Mbunge wa Jimbo la Handeni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na utekelezaji wa Mradi wa Maji wa Segera – Kabuku uliopo Wilaya ya Handeni, Mkoani Tanga, kwa gharama ya shilingi bilioni 25.5. Mradi huo unahusisha ujenzi wa dakio lenye uwezo wa kuzalisha maji lita milioni 5.9 kwa siku, ujenzi wa mtambo wa kutibu maji (*treatment plant*) wenye uwezo wa kutibu maji lita milioni 5.78 kwa siku, ujenzi wa tanki lenye ujazo wa lita 2,000,000 sanjari na ulazaji wa mabomba umbali wa kilometa 80.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huo umefikia wastani wa 55% za utekelezaji na unatarajiwa kukamilika ndani ya Mwaka wa Fedha 2026/2027, kadri fedha zinavyopatikana. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Charles Jacob Sungura.

**MHE. DKT. CHARLES J. SUNGURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini ninaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kwa kuwa, Mradi huu wa Segera – Kabuku, ambao Waziri ameujibia sasa mabomba yanakwama na yamezuiwa kupita kwenye eneo la Shamba la Askofu

Mwingira kwa kigezo cha Askofu huyu kudai fidia, jambo ambalo linachelewesha haki ya maelfu ya wananchi kupata huduma ya maji. Je, Serikali ipo tayari sasa kutumia Sheria ya Ardhi na Mamlaka ya Waziri wa Maji, kuketi na Askofu huyu, ili mabomba yasikwame, yapite. ili mradi uweze kukamilika kwa wakati?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; ni kwamba, kwa kuwa, wananchi wengi wanaishi mbali kidogo na bomba kuu la ule Mradi wa Miji 28, bomba lile linalotoka Korogwe kuja Handeni. Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kufanya *extension,* ili maji haya yaweze kuwafikia wananchi wengi, mara tu mradi ule utakapokamilika? Ninashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu maswali madogo ya nyongeza ya Mheshimiwa Charles Jacob Sungura, Mbunge wa Handeni. Ninaanza kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Charles Jacob kwa kazi nzuri anayoifanya kwa wananchi wake wa Handeni, lakini pia, kwa kuendelea kuwasemea na kuwasilisha changamoto katika Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza. Mradi huu wa Segera – Kabuku hauna fidia. Ninatumia fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wake wa Handeni kwa kukubali kuupokea mradi na kutoa maeneo yao bure kabisa, ili waweze kufaidika na maji, lakini ninamtoa hofu kuhusiana na suala la Askofu Mwingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Maji inaendelea kum-*engage,* ili atambue mradi huo hauna fidia yoyote, lakini pia, atambue kwamba, mradi huu ni kwa maslahi mapana ya wananchi zaidi ya laki moja na kitu wanaoishi katika maeneo ambayo yatanufaika na haya maji. Tunatambua kwamba, mashamba yake nayo ni ya muhimu sana, lakini tutaendelea kuhakikisha anapata uelewa wa kutosha, ili tu aweze kutoa ushirikiano kwa Serikali, ili iendelee kutekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, hasa katika kumtua mama ndoo kichwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaendelea kuhakikisha kwamba, hilo linawezekana bila ya kuwa na changamoto, neno kutoka Serikalini ni kwamba, mabomba ambayo yamefika, wananchi wasiwe na wasiwasi, yatapitishwa na watakwenda kupata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao Mradi wa Miji 28. Mradi huu ni *package* ya wilaya nne; Wilaya ya Handeni, Pangani, Korogwe pamoja na Muheza. *Package* hii ina zaidi ya gharama ya shilingi bilioni 172 ambao ni uwekezaji mkubwa sana wa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Wanufaika katika mradi huu ni zaidi ya wakazi 870,000 katika wilaya hizi tatu, wakiwemo wananchi wa Handeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejipanga pia, baada ya kupokea maombi ya Mheshimiwa Mbunge kwamba, kuna wananchi wake ambao wapo mbali na bomba kuu. Mheshimiwa Waziri wa Maji amekubali kuhakikisha kwamba, mradi utakapokamilika tutaandaa *extension* ya kilometa 60 katika maeneo ya wananchi wake ambao watakuwa wanahitaji huduma ya maji safi na salama. Ninamtoa hofu, tupo vizuri na hilo litatekelezwa bila ya kuwa na changamoto yoyote. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea. Mheshimiwa Mary Daniel Surati, Mbunge wa Serengeti.

Na. 291

**Kuongeza Bajeti ya Huduma ya Maji, Serengeti**

**MHE. MARY D. SURATI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaongeza Bajeti ya Huduma za Maji Wilaya ya Serengeti?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Mary Daniel Surati, Mbunge wa Jimbo la Serengeti, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipaumbele cha Serikali ni kukamilisha miradi inayoendelea kwa kutenga bajeti kila mwaka, ili kuhakikisha inaboresha upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama kote nchini, ikiwemo Wilaya ya Serengeti, Mkoani Mara. Katika kutimiza azma hiyo, Serikali katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 imetoa jumla ya shilingi bilioni 1.339 katika Wilaya ya Serengeti na kuwezesha ukamilishaji wa utekelezaji wa miradi mitano ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, hadi kufikia Mwezi Machi, 2026 jumla ya shilingi bilioni 1.568 zimetolewa, ambapo zimewezesha kukamilisha miradi sita katika Wilaya ya Serengeti, wakati miradi saba ikiendelea, ukiwemo Mradi wa Miji 28 wa Mji wa Mugumu kwa gharama ya shilingi bilioni 23.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kuongeza bajeti sambamba na kupeleka fedha za utekelezaji wa miradi katika Wilaya ya Serengeti kadri ya mahitaji na upatikanaji wa fedha, ili kuimarisha zaidi upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mary Daniel Surati.

**MHE. MARY D. SURATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na ninampongeza Naibu Waziri kwa majibu mazuri na yenye kutia moyo. Pia, ninatumia fursa hii kumshukuru kwamba, alifika Wilayani kwetu Serengeti na kuufuatilia Mradi huo wa Miji 28.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu moja tu, la nyongeza, kwake. Je, ni lini sasa Mradi huu wa Miji 28 utakamilika Wilayani Serengeti, ukizingatia Serengeti inahudumia wananchi pamoja na watalii? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali moja dogo la Mheshimiwa Mary Daniel Surati, Mbunge mahiri wa vijana kwa kazi kubwa anayofanya kuliongoza Jimbo la Serengeti, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa nimefanya ziara Mugumu, Serengeti na nikajionea hali ya upatikanaji wa maji na mwenendo wa utekelezaji wa huu Mradi wa Miji 28 ambao unagharimu zaidi ya shilingi 23,000,000,000, ambapo Serikali ya Chama Cha Mapinduzi imewekeza. Ni mradi ambao unaenda kunufaisha wakazi wa Mheshimiwa Mbunge zaidi ya 150,000 utakapokamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama Serengeti ni 63%, mradi huu utakapokamilika tunaenda ku-*shoot* mpaka kufikia 95%. tunatambua kwamba, Mheshimiwa Mbunge ametusaidia sana kutoa elimu kwa wananchi wake kutambua umuhimu wa mradi huu na pia, hauna fidia. Mbunge amekuwa mstari wa mbele kuhakikisha kwamba, anatusaidia sana Serikali, tunampongeza kwa hilo na tunahakikisha kwamba, tutaendelea kushirikiana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu unatarajiwa kukamilika Desemba 2026. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge na muda wetu wa maswali umeshakwisha.

Waheshimiwa Wabunge, ni muhimu tukaendelea kujifunza kanuni zetu na kuzifuata, kwa ajili ya utekelezaji bora wa shughuli zetu Bungeni. Kanuni ya 52(2) inaonesha jinsi ya kuuliza swali unaposimama, huna haja ya kuongeza maneno ya ziada, unajulikana wewe ni Mbunge wa jimbo fulani, unajulikana wewe ni Mbunge unayewakilisha fulani. Kwa hiyo, unaposimama unatakiwa useme tu ninaomba swali langu namba fulani lipatiwe majibu, ni hivyo tu. Ukiendelea kuongea mengine muda unakwisha. Tunasema hivyo kwa sababu, kanuni ya 53 inaeleza kuhusu muda wa maswali.

Wakati wa mikutano ya kawaida tuna dakika 90, saa moja na nusu, lakini wakati wa Bunge la Bajeti tuna dakika 60 tu, saa moja. Kwa hiyo, mtaona muda ambao umepita, ndiyo maana tunahimiza maswali ya nyongeza yawe mafupi, ili wengi wapate kuuliza. Siyo vyema wala siyo uungwana unapoanza kushauri mimi nikakukatisha nikakwambia kwamba, uliza swali. Hatutakiwi kushauri sasa hivi, utaonekana kanuni huzielewi. Kwa hiyo, ushauri ni wakati ambapo tunachangia na wakati wa maswali ni wakati wa maswali. Ninaomba sana tuzingatie kanuni ili Bunge letu liwe na staha yake. *(Makofi)*

Ninakumbusha pia wakati tunapowasha visemeo vyetu, tunapokuwa tume-*log in*. Unapokuwa umebonyeza na wakati wengine wanaendelea kuuliza ikiwa ipo wazi maneno yako yanasikika kwenye *Hansard* kwa hiyo, mkiwa mmewasha basi mpumzike kidogo kuongea au mzime halafu ndiyo mwongee kwa sababu, kwenye *Hansard* maneno yenu yanasikika. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo, sasa nitatangaza wageni ambao wapo Bungeni kwa asubuhi hii ya leo:-

Tuna wageni wa Mheshimiwa Spika. Mgeni wa Mheshimiwa Spika ni Ndugu Monica Masaburi. Karibu sana. *(Makofi)*

Pia, tuna wageni wengine ambao wamekaa kwenye Jukwaa la Mheshimiwa Spika; kuna wageni wa Mheshimiwa Profesa Adolf Faustine Mkenda, Waziri wetu wa Elimu, Sayansi na Teknolojia. Hawa ni Ndugu Fadhili Rajabu Maganya, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi Taifa; Ndugu Kilumbe Ng'enda, Naibu Katibu Mkuu, Jumuiya ya Wazazi Bara; na Ndugu Yusufu Nzoa, Katibu Tawala Mkoa wa Kilimanjaro. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Profesa Mkenda, ambao hawa ni marafiki zake kutoka Wilaya ya Rombo, Mkoani Kilimanjaro. Karibuni sana. *(Makofi)*

Yupo pia mgeni wa Mheshimiwa Wanu Hafidh Ameir ambaye ni Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Linda Mhando, Mshauri wa Mwanamke *Initiative Foundation (MIF)*. Karibu sana. *(Makofi)*

Wageni 24 wa Mheshimiwa Christina Solomon Mndeme ambao ni marafiki zake aliosoma nao Shule ya Wasichana *Tabora Girls*. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna pia wageni wa Waheshimiwa Wabunge: Tuna mgeni wa Mheshimiwa Amour Seif Abdalla, ambaye ni mfanyabiashara kutoka Zanzibar. Karibu sana. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Bonnah Ladislaus Kamoli, ambao ni rafiki zake kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 56 wa Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza, ambao ni Wenyeviti wa Serikali za mitaa, CCM kutoka Jimbo la Segerea, Dar es Salaam. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tuna wageni 13 wa Mheshimiwa Suleiman Mohamed Rashid, ambao ni viongozi wa Chama cha Walimu kutoka Mkoa wa Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Edward Olelekaita Kisau, ambao ni wanafunzi aliosoma nao shule ya *Agape Lutheran Junior Seminary*. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Fagason Aron Nkingwa, ambao ni Ndugu Esther Lwesagula, mke wa Mheshimiwa kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibu sana. *(Makofi)*

Tuna wageni 94 wa Mheshimiwa Sarah Msafiri Ally, ni wanafunzi 87 na walimu saba wa Shule ya Sekondari ya Melela kutoka Mvomero, Morogoro. Karibuni sana wanafunzi wetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia tuna wanafunzi wengine ambao wametembelea Bungeni hapa kwa ajili ya mafunzo; wanafunzi 121 na walimu sita kutoka Shule ya Msingi *King's Modern* kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana wanafunzi wetu. Wageni wote mnakaribishwa katika Bunge letu, karibuni sana. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano yetu kwenye Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. Tutaanza na Mheshimiwa Nassriya Nassir Ali, Mheshimiwa Mariam Ditopile Mzuzuri, Mheshimiwa Nyamizi Simon Mhoja ajiandae.

*(Hapa Mhe. Nassriya Nassir Ali alichangia kupitia mtaalamu wa lugha ya alama)*

**MHE. NASSRIYA NASSIR ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kabla ya yote, nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, lakini pia nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi hii na sitachoka kusimama nitaendelea kuuliza na kutoa hoja zangu kadri nitakavyoweza kwa sababu hapa nipo kwa kuwakilisha watu wenye ulemavu kwenye nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niipongeze Wizara ya Elimu na nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo amekuwa akiifanya ndani ya Wizara ya Elimu kuhakikisha kwamba anajenga shule lakini pia kuhakikisha kwamba anajenga shule jumuishi kwa ajili ya watoto wetu wenye ulemavu. Pia, kuna shule ya wasichana mpya

nimepata kuisikia jumuishi kwa ajili ya watu wenye ulemavu, nipongeze kwa hilo pia na niwapongeze sana Wizara ya Elimu kwa kazi yao kubwa na nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina furaha kubwa kuona kwamba kuna miongozo tisa ndani ya Wizara ya Elimu ambayo imehusisha ujumuishaji kwa watu wenye ulemavu, ninawapongeza sana. Niseme wamenitia nguvu kwa sababu hii itakwenda kurahisisha utoaji wa elimu kwa watoto wenye ulemavu ndani ya nchi hii na masuala yanayohusiana na elimu, tunaambiwa elimu ni ufunguo wa maisha, bila elimu maana yake hakuna kitu ambacho unaweza ukafanya na ukaeleweka unafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, nimshukuru sana Profesa Adolf Mkenda kwa kazi yake kubwa na dada yangu Mheshimiwa Naibu Waziri Wanu, nina imani nao na ninaamini nao watakuwa mabalozi wazuri kwa ajili ya wanafunzi na watoto wetu wenye ulemavu. Ninaamini pia watasimamia vizuri hii miongozo na kazi hizi ziende vizuri ili watu wenye ulemavu waweze kujumuishwa vizuri kwenye shule zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichangie mambo kadha wa kadha kama matatu hivi. Kwanza ninarudia tena kuomba sana Serikali, Serikali yetu iweze kujenga shule kila Mkoa, shule jumuishi kila Mkoa ili kuweza kusaidia wazazi wa watoto wenye ulemavu kuwapunguzia ule mzigo wa kuwapeleka watoto wao mashuleni na umbali ambao wanajikuta wanakwenda katika hali ya umbali. Ni vizuri kujenga shule hizi ili kupunguza gharama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano hai, nilikuwa ninaishi Zanzibar, lakini fikiria nilikuwa ninasoma Tanzania Bara na hapo hapo shule ya msingi sisi tunasoma miaka 10 na hapo hapo unatakiwa ujiunge na sekondari, umri unakuwa umekwenda. Kwa hiyo ni changamoto, ukiacha tu kupunguza gharama pia tunapoteza muda mrefu. Kwa hiyo, niombe sana kwa heshima kubwa na kwa unyenyekevu, hizi shule ziweze kujengwa katika kila mkoa na kila wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine kuhusiana na suala zima la lugha ya alama, ningeiomba sana Mheshimiwa Waziri lugha ya alama iweze kufundishwa kama lugha rasmi shuleni kuanzia shule ya awali, msingi, sekondari mpaka vyuo vikuu, iwe kama somo rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaweza kusema ninashangaa wakati mwingine tunakuwa na wakufunzi, tunakuwa na walimu, lakini sasa ninajiuliza wanafanya kazi gani kama wanataka kuwajumuisha watu wenye ulemavu wakati huo huo hawawezi kuwafundisha kwa njia ipasayo. Kwa hiyo ninatamani sana kuwe na ujumuishaji kwa maana walimu wapo, wakufunzi wapo, lakini kuna umuhimu sana wa kuwawezesha hawa ili waweze kuwafundisha watoto wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Serikali na nirudie tena kwa unyenyekevu tena, ninafahamu kwamba kuna Wakurugenzi Wizara ya Elimu, lakini kuna Kitengo cha Watu Wenye Ulemavu, ningeiomba sana Ofisi ya Mkurugenzi ya Elimu Maalum katika Wizara ya Elimu iweze kutupatia ushirikiano wa hali ya kutosha kwa sababu hawawezi kufanya peke yao, lazima tushirikiane na watu wenye ulemavu ili kupata mawazo na kuwasaidia wap kujua ni namna gani wanaweza kuboresha mifumo ya elimu hapa Tanzania; kuna umuhimu sana wa kutushirikisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kuhusiana na mitaala ya elimu. Kwanza ninapongeza kwa kuweka mitaala ya elimu mipya, ni hatua kubwa, lakini niseme kwamba watu wenye ulemavu, kuna vyama 12 kama sikosei au vyama 13 ambavyo kuna ulemavu wa aina tofauti tofauti, hii siyo rahisi, kwa nini? Ninarudia tena, viziwi sisi tunasoma miaka 10 shule ya msingi, fikiria watu wenye ulemavu wengine hali yao inakuwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tunasoma hivyo kutokana na uhitaji na utofauti wa ulemavu wetu. Kwa hiyo wakati mwingine inatuwia nguvu sana kuweza kukamilisha elimu zetu kwa ufasaha kwa sababu tu ya uhitaji na changamoto zetu. Niseme sisi kundi la viziwi tuna hali ngumu shuleni, kwa hiyo wakati wanaboresha mitaala, wakati huo huo waboreshe namna ya usahihishaji kwa ajili ya watoto wetu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo tunahitaji kuiangalia vizuri zaidi kwa sababu sisi viziwi kuna namna Kiswahili chetu hakijanyooka, kwa hiyo tunapoboresha, tuboreshe na namna ya usahihishaji wetu. Ninaomba sana tunaposhirikiana na wadau wa elimu wakati wa kuandaa hii miongozo au programu mbalimbali za elimu ni vizuri tuweze kushirikishwa kwa sababu sisi ndiyo tunajua viatu vinatubana wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesafiri mikoa kadha wa kadha, nimefanya ziara na kuona shule kadhaa za watu wenye ulemavu, ni Mungu tu atusaidie, nimeona namna ambavyo mama amejitahidi kujenga shule nzuri ambazo ni jumuishi na ana upendo na watoto wenye ulemavu, kwa hiyo, niombe sana kwenye maeneo ambayo miundombinu bado haijakaa vizuri iweze kuboreshwa ili watoto wetu waweze kusoma vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tupo pia kwenye mpango wa bima ya afya kwa wote, ni vizuri watoto wetu wenye ulemavu waweze kupatiwa hizi bima wakiwa shuleni kwa sababu wana uhitaji mbalimbali. Niombe sana Wizara ya Elimu pamoja na Wizara ya Afya wakishirikiana na TAMISEMI waweze kuliona hii kwa utofauti, hususan tuna watoto wetu ambao wako huko *boarding* wanahitaji sana hizi bima za afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna shule moja ipo Katumba, ni *Katumba Primary School* ipo Tukuyu, Mbeya, hii ni shule jumuishi lakini hali yake ni mbaya, walimu ni wachache, hawajitoshelezi kuweza kufundisha watoto wetu wenye ulemavu. Kwa hiyo nimeona, nipo tayari kutumika, nipo tayari ninaweza kusema nipo tayari kuwa mtumwa, wanitume tuweze kusaidiana kuboresha elimu yetu hapa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaongea hivi kwa sababu kiatu kinanibana mimi mwenyewe, ninafahamu na wakati mwingine ninakosa usingizi, ninajiuliza watoto wetu wenye ulemavu wana hatma gani huko mbele. Kwa hiyo, tunapofikiria haya mambo tuyachukulie *in a simple way*. Ni vizuri sana tuwe na *data* kamili ya watoto wetu wenye ulemavu hapa Tanzania wa aina tofauti tofauti ili tuweze kwenda vizuri; bila hivyo hatuwezi kwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni sawa tuna vifaa saidizi nimesikia hapa kwenye hotuba kuna vifaa saidizi, lakini hivi vifaa saidizi tuna uhakika gani vinawafikia watoto mbalimbali kwenye mikoa tofauti tofauti? Ni vizuri tusiishie tu kusema watu wenye ulemavu kuna mahitaji maalum, kuna vifaa saidizi, Hapana! Tuvitoe kwa mgawanyo sahihi, kwa maana hiyo tunahitaji *data* kamili; viziwi wako wangapi? Wanapatikana mikoa mingapi? Watu wenye ulemavu tofauti tofauti wako wangapi? Hilo ni la muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri pia kufahamu namna ambavyo wanatekeleza majukumu yao katika Wizara ya Elimu, kuwafahamisha vyama vya watu wenye ulemavu ili kuweza kuwapa ushirikiano wa kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme ninashukuru sana na niwashukuru sana Wizara ya Elimu, lakini Wizara ya Elimu ya hapa Tanzania Bara na Zanzibar kuna umuhimu sana wa ku-*link* ili waweze kubadilishana uzoefu, kuona kule wanafanyaje na huku wanafanyaje kuboresha hali halisi ya elimu yetu hapa Tanzania kwa watoto wenye ulemavu kwa sababu bado tuko nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninalia sana kwa sababu huko ndiyo nyumbani na ninalia huko nyumbani kwetu Zanzibar pia hali mbaya, hali mbaya kwa watoto wenye ulemavu, Pemba kule watoto wenye ulemavu hawako kabisa mashuleni. Kwa hiyo, ninaomba sana tuweze kuungana Tanzania Bara na Zanzibar kuweza kutekeleza elimu yetu na kuifanya kuwa bora kwa watoto wetu wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja. Mungu awabariki na awasimamie kwenye utekelezaji wa majukumu yao. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Nassriya Nassir Ali. Nilimtaja Mheshimiwa Mariam Ditopile Mzuzuri; Mheshimiwa Nyamizi Simon Mhoja na Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso wajiandae.

**MHE. MARIAM D. MZUZURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa fursa hii. Kwanza nitangulie kuungana na wachangiaji wenzangu kumpongeza Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa maono yake ya kulielimisha Taifa hili tangu achukue madaraka. Tumeona namna gani ameweza kuidhinisha na kupeleka fedha za kutosha katika sekta ya elimu na sisi tunaamini kulielimisha Taifa hili ndiyo kulipa uhuru kwa nyanja zote. Kwa hiyo, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais na amejikita kuhakikisha Watanzania wanapata elimu bora na siyo bora elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendeleee pia kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuweza kutambua vipawa na talanta vya kuweza kufanya nao kazi ili kutimiza maono yake kwa Watanzania. Tumeona namna gani amekuwa anaona Wabunge bora kabisa wenye uwezo wa kufanya nao katika Baraza la Mawaziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nimpongeze sana Profesa Adolf Mkenda, kwa kweli anafanya kazi kubwa sana kwa wananchi wake wa Jimbo la Rombo na niliwahi kwenda kule kwenye moja ya matamasha aliyoandaa ya Rombo Marathon, nimhakikishie Mheshimiwa Adolf, pamoja na mageuzi anayomsaidia Mheshimiwa Rais katika sekta ya elimu, lakini wananchi wa Rombo wamenihakikishia kwamba yeye akae atulie pale mpaka atakaposema basi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakika Mheshimiwa Mkenda ana utu na utulivu, ametulia ndiyo maana unaona mikeka inapita lakini yeye ameweza kudumu kwenye Wizara hii. Kipekee nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Wanu Hafidh Ameir, kwa kweli utendaji na umakini wa Mheshimiwa Wanu umekwenda kuthibitisha kwamba Jumuiya ya Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi ama hakika ni tanuru la kuoka kiongozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wale wasiomfahamu, Mheshimiwa Wanu amepata kuwa Mwenyekiti wa UVCCM Mkoa wa Kusini Unguja na alikuwa Mjumbe wa Baraza Kuu la UVCCM Taifa. Miongoni mwa waliokuwa katika Baraza wenzake ambao wameweza kufanya vizuri na wako wanasaidia sekta mbalimbali mbalimbali katika Serikali yetu

ni Mheshimiwa Anthony Mavunde, Mheshimiwa Mtaka, Mheshimiwa Deogratius Ndejembi na akina *Comrade* Gavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hakika Mheshimiwa Wanu kwa sisi ambao tumepitia UVCCM *we are so proud of you*. Pia Mheshimiwa Wanu huyu kule Baraza la Wawakilishi ameweza kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa miaka 10 na ninakumbuka kwenye Bunge la Kumi na Moja kati ya wale wajumbe wa Baraza la Wawakilishi watano waliopigiwa kura kuja kuwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Wanu alikuwa mmojawapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haikuishia hapo, Mheshimiwa Wanu akaenda kuthubutu kugombea Ubunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Kusini Unguja kuanzia mwaka 2020 mpaka 2025, lakini kwa sasa hivi Mheshimiwa Wanu ni Mbunge wa Jimbo la Makunduchi na kwa kweli ni Mbunge ambaye ana cheti chake. Hongera sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwenye uzoefu wa uwakilishi wa wananchi, Mheshimiwa Wanu kwenye mhimili huu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kule Baraza la Wawakilishi ana miaka ya uzoefu zaidi ya 20. Ukiacha kazi za siasa ameanzisha taasisi inayoitwa Mwanamke *Initiative Foundation* ambayo kwa kifupi ni *MIF*. Taasisi hii imejikita kwenda kusaidia jamii hususani wanawake ama wasichana katika nyanja ya elimu na nimetembelea kule Jimbo la Makunduchi hakika matokeo yake ni chanya na hasa maskini wameweza kufaidika ndani ya jamii ile kupitia taasisi yake hii ya *MIF*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sifa za kipekee za kibinadamu, mwanamke huyu ni jasiri, mwanamke huyu ni msikivu, mwanamke huyu ni shupavu, ana weledi, mtaratibu, mnyenyekevu *above all* Mheshimiwa Wanu anafikika na watu wa aina na rika zote. Kwa hiyo, mimi binafsi ninaona watu wenye sifa za Mheshimiwa Wanu wanahitajika kuwa viongozi ndani ya Taifa letu na nirejee kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kumwona Wanu na kumuunganisha na Profesa Mkenda pamoja na Watendaji wakiongozwa na Mama yetu Profesa mzito kabisa, Mama Nombo ili kuweza kupeleka mbele gurudumu hili la maendeleo kwenye sekta ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nong'onong'o zipo na hazikosekani, ndiyo mambo ya siasa, mimi ninasema kimfaacho mtu chake, sasa kama mama, mtu aliyemlea hawezi kujua sifa zake na akaonyesha macheche! Eeh, tuko Wabunge hapa wengine wana biashara, mfano Mheshimiwa Shabiby, Mheshimiwa Koka, watoto wao wamewapa kurugenzi, utendaji kwenye biashara zao na wanachapa kazi. Kwa hiyo, hakika Wanu ana jambo ndani yake na hakika atafika mbali katika nyanja za siasa kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu. Kaa vizuri na Profesa Mkenda, ni mlezi na hakika basi Wizara hii itakwenda kutimiza yale yote ambayo yamewekwa kwenye Ilani, kwenye mpango wa maendeleo, lakini kikubwa kwenye maono ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile tunajadili bajeti, niipongeze sana Wizara na hapa ndiyo umakini wa Mheshimiwa Mkenda unaonekana. Wamefanya vizuri sana kwenye ukusanyaji wa maduhuli, nimesoma taarifa yao mpaka kufikia Aprili wameshakusanya zaidi ya 72, inaonesha mwanga, ikishafika mwezi Juni, basi watakuwa wamevuka zaidi ya 80%. Hongera sana kwao kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimevutiwa pia na mtiririko wa fedha hususani za miradi ya maendeleo na hasa zile fedha za ndani. Tunapoweza kutoa fedha za ndani kwenye miradi yetu ya maendeleo, hiyo ndiyo inatupa uhakika kwamba mambo yetu hayatokwama. Tumeona mpaka Aprili zimeenda zaidi ya 60% kwenye fedha zetu za ndani, lakini zile fedha za nje zaidi ya 42%. Hili inatuhakikisha kwamba Vyuo vya *VETA* vitakamilika, shule zitaongezeka na mambo mengi yatakwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatokea kule Kondoa Mjini, ninamwomba Mheshimiwa Waziri na Watendaji wote, *management* ya Wizara na Wakurugenzi wote wa taasisi ambao wanachapa kazi, Wizara nimesoma kwenye ukurasa wa 97 kipengele cha (i), wamejipanga kuwezesha ujenzi na upanuzi wa miundombinu katika shule 30 za amali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Kondoa Mjini tunashukuru tumepata Shule ya Amali pale kwenye Kata ya Kingale, walituletea shilingi 544,000,000 na kwa ufanisi mzuri wa Mkurugenzi Mtendaji, Ndugu Majaliwa, lakini kwa usimamizi wa Baraza la Madiwani ukiongozwa na Mwenyekiti wangu Mama Zainab Haroub, fedha zile zimetendewa haki, majengo yamekamilika, watoto wanasoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninaomba katika fedha zilizotengwa mwaka huu, basi watukumbuke Kondoa Mjini kwa sababu bado wanafunzi wale hawapati mafunzo kwa vitendo. Kwa hiyo, ninaomba, kwa kweli katika hili nitamsumbua sana Profesa Mkenda, ili sasa usanifu kamilifu ukaonekane kwenye ile shule ya amali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *page* ile ya 97 kipengele cha (iv) nimeona kwamba Wizara imepanga kukarabati karakana na majengo katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. Sisi kati ya halmashauri za mwanzo kabisa kupata vyuo hivi ni pale Kondoa Mjini kwenye Kata ya Serya, Mtaa wa Munguri; tunacho Chuo hiki cha Maendeleo ya Wananchi cha Munguri, hakika kinafanya vizuri na wanafunzi wanaendelea na masomo yao, lakini kimekuwa chuo kongwe. Hata hivyo tuna changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutoka mjini kuelekea kule Kata ya Serya, tunalo daraja ambalo limekatika zaidi ya miaka 15 na hii kesi anaijua Mheshimiwa Ulega; tumekwishawasiliana sana. Bila hilo daraja hiki cheti 2030 nitakipoteza. Kwa hiyo wanaweza kuona umuhimu wa kutuletea fedha ili tuweze kurekebisha majengo yale. Pia, kama tutapata tawi la pale mjini ili ikitokea changamoto za mvua nyingi, basi tuone namna gani wanafunzi wale wanaendelea kupata masomo yao bila ya kuyakatisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona ufaulu unaenda vizuri sana kwenye shule za bweni. Kwa hiyo, tunawaomba kule tulikopanga kujenga mabweni, hasa kwenye kata ambazo zipo pembezoni, ama kata ni kubwa mitaa imetawanywa kwa mbali twende tukajenge ili kunusuru pia madhara ambayo yanawafika wanafunzi, hususan wa kike. Pia kwenye shule zetu za *day* ama shule za kutwa tumeona

ufaulu wake kidogo si mzuri. Kule sisi kama wananchi tukishirikiana na baadhi ya viongozi tumekuwa tukibuni kufanya kambi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli kambi hizi zimekuwa na matokeo chanya. Kwa hiyo, muda umefika sasa, kwa sababu wamejikita katika kuhakikisha tunapata elimu bora, hebu Serikali ikae chini; na bajeti tunajua haitoshi; tuone namna gani wataunga nguvu za sisi viongozi wenzenu, kwa maana wawakilishi wa wananchi na wananchi kutuwezesha kufadhili kambi hizi ili ile azma ya watoto wetu kufaulu na elimu yetu kupanda ubora iweze kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo niendelee. Yaliyofanyika kwenye sekta ya elimu, sisi wote ni mashahidi, leo hii kwa kweli ufaulu umepanda na majengo yanapendeza. Leo ukifika kwangu kule kijijini Suruke unakuta darasa la chekechea ni sawasawa na yale ambayo tumezoea kuona huko Masaki na Msasani; sasa yamefika kule kwa wanyonge wenzangu wa Kondoa Mjini. Hizi zote ni jitihada za Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na ambaye amejikita pia kuokoa akili nzuri za watoto wa kike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono Samia *Scholarship*; kwa kweli malengo yake ni mema. Sasa hivi wamejipanga kuongeza wanafunzi wapya 1,000; basi kale kautaratibu watuwekee wazi ili na sisi; wapo Warangi wenzangu na Wakurunge wenye akili, ili nao waweze kuwa wanufaika wa Samia *Scholarship*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mariam Ditopile. Nilimtaja Mheshimiwa Nyamizi Simon Mhoja; Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso na Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete wajiandae.

**MHE. NYAMIZI S. MHOJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa ili nichangie katika Wizara hii ya Elimu. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutufikisha mahali hapa tukiwa wazima, tukiwa na afya njema mimi na Wabunge wote ambao tupo mahali hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuboresha elimu kwa watu wenye ulemavu, sambamba na wasaidizi wake, Profesa Mkenda na Mheshimiwa Wanu. Kwa kweli tunaona juhudi zao na tunaona matokeo kabisa, tunayaona kwa walimu na shule mbalimbali ambazo wanaendelea kufanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kwa moja ninaomba nijikite katika elimu jumuishi na muda ukiruhusu basi nitaenda kwenye *point* nyingine. Hapa tulipofikia ni tofauti na tulikotoka. Mfumo wa Elimu Tanzania hasa kwa watu wenye ulemavu upo tofauti tofauti. Kuna *regular schools* (shule za kawaida). Hizi shule amabazo wengi tunaona zimejengwa tangu enzi za ukoloni hadi sasa hivi zipo, ambapo pia hata watu wenye ulemavu wakuwepo, lakini haziwi rafiki kwa makundi ya watu wenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna *intellectual schools* pia. Shule hizi ni zile ambazo zinakuwa za kawaida, lakini kunakuwa na kitengo cha watu wenye ulemavu. Kwa mfano, kwa viziwi peke yao au ni wasiyoona peke yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna *special schools*. Hizi ni shule maalum ambazo zilikuwepo na bado zinaendelea. Hizi ni kwa ajili ya wale watoto ambao ndiYo wanakwenda moja kwa moja, wanahitaji shule maalum kwa ajili ya uangalizi mzuri na wa karibu ili waweze kupata elimu, zipo na zinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hivi kuna elimu jumuishi. Elimu jumuishi ipo na inaendelea kusonga mbele, tunashukuru Wizara inaendelea kuikazia kabisa hadi imeweka mwongozo au ninaweza nikasema mkakati wa elimu jumuishi, tunaishukuru sana Serikali. Kwa kupitia hivyo, ninaunga mkono hoja, hii bajeti ikiwezekana waongezewe kutokana na kuboresha elimu jumuishi. Ukiangalia *goals as Sustainable Development Goal IV*, imeeleza maana ya elimu bora; nayo imesisitiza elimu jumuishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kwenye mkataba wa kimataifa Kifungu cha 24 kimeeleza elimu bora kwa watu wenye ulemavu, lakini na elimu jumuishi. Hata kwenye Sheria ya Watu Wenye Ulemavu Na.9 ya 2010, vifungu vya 27, 28, 29 vinaeleza elimu jumuishi na yenyewe inakwenda mbali sana na kusema kwamba elimu maalum ni mpito tu kuelekea elimu jumuishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, faida yake; elimu jumuishi inapanua wigo kwa watoto wenye ulemavu kupata elimu pamoja na kupunguza unyanyapaa na ubaguzi kwa watoto hasa kwenye jamii. Kwa sababu mtoto akiwa anasoma na wenye ulemavu anamjua akiwa mdogo hata anapokua unyanyapaa utapungua katika jamii; pia watoto wenye ulemavu kujisikia wapo katika jamii kama wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie changamoto. Sasa hapa ndiyo maana ninasema ninaomba Wizara iongezewe fedha kwa ajili ya kuboresha elimu jumuishi. Maana ya elimu jumuishi ni kwamba, mtoto mwenye ulemavu yeye ndiye anayesoma katika shule za kawaida lakini zinazoboreshwa, zinawekwa jumuishi, kwa maana ya miundombinu inakuwa rafiki na mahitaji mbalimbali anayoyahitaji mtoto mwenye ulemavu, anasoma katika shule za kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto mojawapo ni kwamba, walimu waliopata elimu maalum ni wachache kulingana na idadi ya shule maalum. Vilevile miundombinu bado si rafiki kwa watoto wenye ulemavu. Kwa mfano *library* nyingi za shule; na ninaomba Mheshimiwa Waziri apange hata ziara kutembelea hizi shule jumuishi ili ajionee mwenyewe; *library* haziko rafiki, mtoto anaendaje kusoma *library* kama hawezi kufika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata *laboratory,* unakuta meza moja na nyingine mtoto ambaye anatumia *wheel chair* hawezi kupita katikati; Sasa tunamzuia asisome masomo ya sayansi; na mambo mengine mengi ambayo yanaendana na miundombinu ninaomba iboreshwe; kwa kufanya hivyo ndivyo tunaweza kuita elimu jumuishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule hizi pia zingeweza kuongezewa fedha. Kwa mfano, sasa hivi watoa ile *fee compensation*. Hizi *fee compensation* zinagawiwa sawa katika shule zote. Kwa kuwa ni shule hizi zingeongezewa hii fedha kwa sababu, kwa mfano kuna watoto ambao ni *multiple disability* kwa sababu ni jumuishi, watoto wenye ulemavu wapo pale. Kwa mfano *intellectual impairment,* huyu mtoto ana uelewa wa mbali, kumbukumbu yake ipo mbali, anahitaji mwalimu awe naye masaa 24 ili aweze kumkumbusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mzuri, hata ukiangalia Shule ya Pugu yupo mtoto kama huyo ninadhani sasa hivi atakuwa yuko *A level,* walimu wanapata shida, lakini wanajitahidi kwa kweli ninawapongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia vilevile kuna watoto wenye mgongo wazi, hawa watoto wanatakiwa wavalishwe *catheter* ya kutolea haja ndogo, pia wanavalishwa *diapers.* Hivi vyote hivi vinaingia wapi? Kwa sababu unakuta watoto kama hawa hawana uwezo, wanapata wapi? Tunajikuta sasa tunampa mzigo mkuu wa shule atafute wafadhili na kuna wakati anakosa; ilihali Wizara inaweza kuongeza bajeti katika hii elimu jumuishi, ili watoto wapate raha na kufurahia elimu. Pia watoto kama hao wanaohitaji dawa na vilevile wanahitaji mazoezi. Kwa hiyo, mambo yapo mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba elimu jumuishi kweli iwe elimu jumuishi. Tunaomba tuboreshe mambo madogo madogo kama hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, linguine ni kutokusahau maslahi ya walimu. Hawa walimu wanatakiwa walipwe *extra* ikiwezekana kwa sababu wanatambulika, mkuu wa shule anawajua, wanafanya kazi kwa sababu hakuna walezi ambao wanaweza wakafanya hii kazi. Kwa hiyo unakuta mwalimu ndiye anayemfundisha shuleni, darasani na vilevile anambadilisha, anamwogesha, wapo. Kwa hiyo, ninaomba tuzingatie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu jumuishi haiishii tu kwenye shule za msingi na sekondari. Huyu mtoto akienda chuo kule elimu jumuishi bado. Ninaomba tuzingatie kwa sababu wanafunzi wa vyuo wenye ulemavu wanapata shida, hata mimi nilipata shida kumaliza chuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuzingatia hilo ninaomba nizungumzie kuhusiana na makundi maalum *vis-a-vis* watu wenye ulemavu. Sheria zetu zote, miongozo yote imetambua watu wenye ulemavu, neno watu wenye ulemavu na siyo makundi maalum. Kwa sababu ukisema makundi maalum unajumuisha, wanawake, pia wapo kwenye makundi maalum, watoto ambao wanaishi katika mazingira magumu, siyo wenye ulemavu, wapo kwenye makundi maalum na wazee wapo kwenye makundi maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunaomba kama wataona inafaa, ushauri, watambue kabisa kwamba ni watu wenye ulemavu. Kwa sababu hatimaye nikiuliza Wizara kwamba tuje na *data* za watoto wangapi wamedahiliwa elimu jumuishi tutakosa kwa sababu ndani mle wameweka watoto wenye mahitaji maalum; sasa hapo tunapata shida kupata *data*. Ingetofautishwa watoto wenye makundi maalum wapo wengi katika mazingira yao ya kuitwa makundi maalum. Lakini watoto wenye ulemavu au watu wenye ulemavu pia wanatambulika kihivyo kwa sababu mahitaji yao yanaeleweka na inakuwa ni rahisi hata kuwahudumia vile inavyotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuendelea, ninadhani hii pia ipo kwenye TAMISEMI, kwa sababu wizara hizi lazima ziwasiliane. Kwenye TAMISEMI hiki ni kitengo jumuishi. Sasa tulikuwa tunaomba, kwa sababu umuhimu wa elimu jumuishi umeshakuwa mkubwa na imekwishakuwa ndiyo ajenda kuu ili watoto wenye ulemavu nao waweze kusoma vizuri kama nilivyoeleza faida za elimu jumuishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hiki kitengo kipewe idara kamili kwa sababu mahitaji ni mengi; iweze kufanya hata *evaluation* ya kwamba mpaka sasa tangu tulipoanza elimu jumuishi je, tumepata mafanikio mangapi, kuna shida ipi? Kwa hiyo wawezeshwe ili waweze kuboresha zaidi elimu jumuishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kusema hayo, ninaendelea kumpongeza Mheshimiwa Profesa Mkenda kwa kuendelea. Nina imani tuko na mtu sahihi pamoja na msaidizi wake, pamoja na wote ambao wanasimamia idara hii ya elimu jumuishi; kwa kweli tunaona wanajitahidi. Pia niwapongeze walimu wote wanaosaidia, wanaojihusisha na watoto wenye ulemavu, wakiwemo wanafunzi wa Pugu, wakiwemo sijui Jangwani na shule zote ambazo ni jumuishi. Kwa kweli walimu wanafanya kazi kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kusema hayo, ninaomba kuunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Nyamizi Simon Mhoja. Tunaendelea na Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso; Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete na Mheshimiwa Stella Alex Ikupa wajiandae.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa mchango katika Wizara hii ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Kwanza nianze kwa kutoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa iliyotukuka anayoendelea kuwafanyia Watanzania wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi anayoifanya historia itamkumbuka, historia itamwandika na jina lake litaandikwa kwa wino wa dhahabu. Tunamtia moyo Mheshimiwa Rais wetu, asonge mbele. Watanzania wanamwamini, Watanzania wanamhitaji na Watanzania wanamtegemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii pia kutoa pongezi kwa Waziri wetu wa Elimu pamoja na Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara hii kwa kufanya kazi na kuhakikisha kuwa maono na matarajio ya Dkt. Samia Suluhu Hassan kwenye sekta ya elimu yanafikiwa. Hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua umuhimu wa utoaji wa elimu iliyo bora katika nchi hii, ninapenda kueleza mambo machache yaliyofanywa na Dkt. Samia Suluhu Hassan katika sekta ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uongozi wake alipoingia madarakani na kwa kuwa huko nyuma kulikuwa na mahitaji makubwa ya kuboresha sera ya elimu. Nimekaa Bungeni hapa muda kidogo; tulikuwa tunasema na kuongea; na wadau wamesema kwamba sera yetu ya elimu inahitaji kufanyiwa maboresho. Alipoingia madarakani Dkt. Samia Suluhu Hassan akalibeba jambo hili kwa uzito bila kujali gharama, akahakikisha kuwa sera ya elimu inafanyiwa maboresho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maboresho haya ambayo yamefanywa au yamefanyika yamelenga kutoa elimu si tu ya taaluma bali elimu yenye ujuzi, ili kuhakikisha watoto wetu au wanafunzi wetu wanaingia kwenye soko la ajira, wanakabiliana na mabadiliko ya kiuchumi ya kisayansi, ya kiteknolojia; na kwa hakika waweze kukubalika na kuingia kwenye jamii ambayo au dunia ambayo inakimbia kwa kasi. Hii ni kazi kubwa aliyoifanya Dkt. Samia Suluhu Hassan ya maboresho ya sera yetu ya elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine lililofanywa ni maboresho ya mitaala. Huko nyuma pia kulikuwa kuna uhitaji mkubwa kutoka kwa wadau, kwamba mitaala yetu haiendani na ukuaji wa kasi ya kiteknolojia na uhitaji wa masuala yote ya kidunia kwa ujumla. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alipoingia madarakani alilibeba jambo hili na mitaala yetu leo kuanzia elimu ya msingi, elimu ya awali na sekondari imefanyiwa maboresho na inaendana na mahitaji yote ambayo dunia ya sasa. Haya yamefanywa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine, sote tu mashahidi, huko nyuma wanafunzi wa kike waliopata mimba hawakuruhusiwa kuendelea na masomo. Wanafunzi hawa walipopata mimba kutokana na sababu mbalimbali walirudi nyumbani kuendelea na ulezi, kuendelea na maisha; ndoto zao zilikatishwa, ndoto yao ya kuwa viongozi baadaye, kuwa labda wanasheria, kuwa walimu, kuwa madaktari zilififia kwa sababu walipata ujauzito na nyumbani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamii pia na wakati mwingine hata sisi wazazi tumekuwa na mitazamo mbalimbali na hisia mbalimbali, kwamba hawa watoto wakipata mimba, wakirudi shuleni hali itakuwaje? Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alipoingia madarakani kwa kutambua kwamba kila mtoto ana haki ya kupata elimu na kusiwe na kikwazo chochote, akaruhusu wanafunzi waliopata mimba kurudi shuleni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa takwimu za *BEST* yaani *(Basic Education Statistics Tanzania)* za mwaka 2020 zilionesha tuna wanafunzi takribani 4,000 wa kike walikatisha masomo kutokana na ujauzito. Sababu ambazo zilisababisha kwanza ndoa za utotoni, ubakaji, ukatili wa kingono, umaskini na wakati mwingine ukosefu wa elimu ya afya ya uzazi. Kwa takwimu hizi, kwa kweli idadi hii ni kubwa. Kwa kuwapatia elimu hawa watoto, maana yake wanaenda kutimiza ndoto zao na wanaenda kuimarika na kukabiliana na hali za kimaisha katika maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba, Sera hii iliruhusu watoto kuingia kurudi mashuleni baada ya kupata mimba, bado jamii ikawa na hofu kwamba, je, kweli watarudi? Watapokelewaje? Watatazamwa vipi? Hadi sasa tunavyoongea, takwimu zinaonyesha tuna wanafunzi takriban 10,000 wamerudi shuleni baada ya kupata ujauzito, katika mfumo ulio rasmi, ama kwenye shule ile ile, ama shule zingine walioweza kuhama na kuendelea na masomo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafsiri ni nini? Tafsiri ni kwamba Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anajali na anatamani kuona watoto wote wa Kitanzania wanapata elimu bila ubaguzi. Si tu elimu, lakini elimu iliyo bora, elimu ambayo itamwingiza kwenye soko la ajira, elimu ambayo itamwajiri ama kujiajiri katika maeneo mbalimbali baada ya kumaliza elimu yetu ya msingi, sekondari au katika vyuo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine; kwa kutambua pia suala la ujuzi ni muhimu, katika uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ujenzi wa shule za ufundi stadi maarufu *VETA* zimejengwa nchi nzima na zinaendelea kujengwa. Hii inatupa tafsiri kwamba,

Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, anaona umuhimu wa ujuzi na ndiyo maana kulikuwa kuna maboresho ya sera kwamba, si tu taaluma itamsaidia mtoto wa Kitanzania, lakini ujuzi kupitia *VETA* katika maeneo mbalimbali na huu ujenzi anaoufanya utamsaidia mtoto wa Kitanzania kuweza kujiajiri. Hii ni kazi ambayo imefanywa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua pia kuna watoto wenye vipaji na watoto hawa wanafanya vizuri katika masomo ya sayansi, teknolojia, ubunifu, uhandisi, hisabati, tiba na kadhalika Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan akaona umuhimu wa kuanzisha kitu kinachoitwa *Samia Scholarship,* ili wanafunzi hawa waliofaulu vizuri katika fani hizi adimu, fani hizi muhimu ambazo tunazihitaji, wapewe ufadhili na Serikali yake chini ya usimamizi wa Wizara husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni utaratibu mzuri, bora ambao Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameusimamia na anaendelea kuusimamia ili kupata wajuzi wengi katika nchi hii na tukitambua kwamba wanafunzi hawa wakati mwingine walikuwa wanafaulu, lakini hawana namna ya kusoma, kutokana na uwezo au kuhitajika fedha nyingi ya kwenda kupata masomo zaidi katika fani hii. Hadi sasa tuna wanufaika wengi na takwimu nilizonazo hapa tuna takriban wanafunzi 3,696 wamenufaika na utaratibu huu wa *Samia Scholarship*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, katika uongozi wa Dkt. Samia Suluhu Hassan, mikopo ya elimu ya juu imeendelea kutolewa na katika uongozi wake wameweza kutoa mikopo pia katika vyuo vya kati, ambapo huko nyuma wanafunzi ambao walikuwa wanaenda katika vyuo vya kati, walikuwa hawapati mikopo. Chini ya uongozi wake, wanafunzi hawa sasa wanapata mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si tu mikopo, jambo hili halijasemwa, lakini chini ya uongozi wake, zile pesa za wanafunzi wanazopewa maarufu *boom*, chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan fedha hizi zimeongezeka. Huko nyuma walikuwa wanapewa shilingi 8,500, lakini leo kila mwanafunzi anayenufaika na mkopo wa elimu ya juu anapata kiasi cha shilingi 10,000, ili aweze kujikimu anapokuwa katika masomo yake katika vyuo vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi yangu ni pongezi, lakini nimependa nionyeshe machache ya kipekee yaliyofanywa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika uongozi wake. Tunamtia moyo, tunamwambia Mheshimiwa Rais asonge mbele, tunamwamini, tunamtegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mapinduzi aliyoyafanya katika Sekta ya Elimu, kwa hakika kwa miaka ijayo tunakwenda kupata Taifa la watoto au Taifa ambalo jamii yake imeelimika kitaaluma na kiujuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso. Nilimtaja Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete; Mheshimiwa Stella Ikupa Alex, Mheshimiwa Yumna Mmanga Omar na Mheshimiwa Festo Richard Sanga wajiandae.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Awali ya yote ninaomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu. Baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, ninaomba nianze kwa pongezi za dhati kabisa kwa Waziri wetu wa Elimu, kwa kazi kubwa na nzuri ambayo ameifanya tangu ateuliwe na Mheshimiwa Rais wetu mpendwa, Mama Samia Suluhu Hassan, kwa kweli, Profesa amefanya kazi kubwa na nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Wabunge wenzake tunaiona, hali kadhalika na Naibu Waziri, Mheshimiwa Wanu, naye amefanya kazi nzuri ya kumsaidia Mheshimiwa Profesa, ninasema hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na pongezi hizo, kabla sijaenda kuwatambua wengine na kuwapongeza; Mheshimiwa Profesa, katika uwasilishaji wake, kwa kweli ni uwasilishaji uliokuwa wa aina yake. Ndani ya Wizara hii, amezungumza mambo mengi, amefanya mambo mengi, amegusa kila eneo, hukuacha eneo hata moja. Ndiyo maana ninasema hongera kwa kazi kubwa na nzuri

aliyoifanya. Pongezi pia, kwa Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu, watendaji wote wa Wizara, hongera sana kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi za pekee kabisa zimwendee Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa maono yake makubwa, kwa umahiri wake, kwa ushupavu wake na kwa ushujaa wake. Pamoja na changamoto nyingi, yeye kama Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ameyafanya mambo makubwa na mengi sana katika Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana Profesa Mkenda, kila atakayesimama katika Bunge hili Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, atasimama kwa kutoa pongezi juu ya kazi kubwa ambayo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kipindi chake ameweza kuifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa maono yake akitambua kwamba, hakuna kitu muhimu zaidi ya elimu, vingine vyote vinafuata baadaye. Ameweka miundombinu mizuri katika eneo letu la elimu na ndiyo pale kama Mama na ndiyo pale kama Rais Mwanamke na ndiyo pale kama shujaa, aliposimama na kusema kwamba, ninataka kujenga shule za sayansi za watoto wa kike ndani ya nchi nzima, na alifanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais akaanza na baadhi ya shule ambazo miongoni mwa shule hizo ni shule 10 ambazo alizijenga. Miongoni mwa shule 10 hizo, nitazitaja shule chache, kuna shule ya Mwanza, kuna Shule ya Samia Suluhu Hassan iko Dodoma, kuna shule iko Arusha, kuna shule iko Lindi inaitwa Lindi *Girls*, kuna shule iko Shinyanga, Dar es Salaam, halikadhalika na mkoa wa Pwani iko Kibiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule hizi ambazo amezijenga, mwaka 2025 ndipo zilifanya mtihani wake wa kwanza. Kwenye mtihani wake huo wa kwanza, nini kilichotokea katika shule hizo, ambazo takribani saba zilizofanya mtihani? Wanafunzi waliopata *division one* walikuwa 236, waliopata *division two* walikuwa 425, waliopata *division three*

walikuwa 179, waliopata *division four* walikuwa pekee yao ni 10 na *division zero* hakukuwepo na mwanafunzi hata mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni matokeo makubwa sana kwa kazi kubwa na nzuri aliyoifanya. Kama wangechaguliwa *division one* na *two* ina maana 77.79% wangeenda kwenye elimu ya juu. Kama wangechaguliwa *one, two* na *three* ina maana walifaulu kwa 98.82% na *division four* ilikuwa asilimia 0.118. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, matokeo haya ni makubwa sana na hiki tulichokuwa tunakitaka, au Mama alichokuwa anakitaka, kupata wanasayansi wengi, lakini wanasayansi hapa wa kike. Kwa nini wa kike? Akizingatia kwamba wanawake waliachwa nyuma sana na ndiyo maana akajua ukimwelimisha mwanamke, umeelimisha jamii. Hongera sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa na nzuri aliyoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo ninataka nizungumzie suala zima linalohusu KKK yaani tatu. Tunapozungumzia KKK, maana yake ni kujua Kusoma, Kuandika na Kuhesabu. Katika mazingira ya kawaida mtu anasema kujua kusoma, kuandika na kuhesabu, ni kitu muhimu sana katika ustawi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanafunzi anapoingia darasa la kwanza, ni lazima ajue kusoma na kuandika baada ya muda mfupi. Ilifikia hatua mwanafunzi anafika mpaka darasa la nne hajui kusoma, mpaka darasa la saba hajui kusoma. Wakati mwingine wanafunzi wanachaguliwa kwenda sekondari bado hapa kuna shida. Mama Samia akasema, sitaki hiyo shida, ninataka kuhakikisha wanafunzi wanajua kusoma, kuandika na kuhesabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walimu watakuwa wanajua nini msingi wa kujua kusoma, kuandika na kuhesabu. Msingi mkubwa wa kujua kusoma, kuandika na kuhesabu, ndani ya miezi mitatu mpaka sita mwanafunzi lazima awe anajua kusoma, kuandika na kuhesabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu, lazima ajue kitu kinachoitwa *alphabet*, atoke kujua *alphabet*, ajue kitu kinachoitwa silabi, atoke kujua kitu kinachoitwa silabi, ajue kitu kinachoitwa neno, akitoka kujua kitu kinachoitwa neno, ajue kusoma kwa kutumia sentensi fupi halafu kifungu cha habari kifupi na kifungu cha habari kirefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapozungumzia ajue kusoma herufi, ajue kusoma silabi, maana yake ni nini? Maana yake ni kwamba, silabi au *syllable* ina maana katika zile herufi, tuna herufi 26, ndani ya herufi 26 kuna kitu kinachoitwa, kwa Kizungu wanaita *consonant* na *vowel*. Sasa ukishakuwa na *consonant* na ukiwa na *vowel* maana yake ni kwamba, katika kuweka ile *syllable,* ni lazima uweke *consonant* ukijumlisha na *vowel*. Yaani herufi moja ukijumlisha na herufi ya pili, yaani *consonant* na *vowel* ndiyo unapata *syllable*. *Syllable;* "b" ukijumlisha na "a" unapata kitu "ba". Kwa hiyo, ukienda kwa hatua hizo, baada ya miezi mitatu au kabla ya hapo unakuwa umeshajua. Kwa hiyo, ni kitu muhimu na kitu cha msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini kifanyike? Katika hili ni lazima wanafunzi wapate walimu ambao wamesomea KKK tatu. Si kila mwalimu anajua kufundisha darasa la kwanza na darasa la pili au la tatu. Kuna taaluma maalum ambayo mwalimu anatakiwa aipate. Kwa hiyo, ninawapongeza kwa dhati na kuwashukuru, lakini pamoja na hayo wanaanzisha shule za amali na kule kwangu ipo shule ya amali; ninawashukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitaka kufanikiwa kwenye hili, ni lazima kuwe na hizo shule. Ukishakuwa na hizo shule, wanafunzi wakimaliza darasa la sita sasa hivi maana yake, wanafunzi wa darasa la sita na darasa la saba watakwenda pamoja kuanza kidato cha kwanza. Niwapongeze kwa kazi kubwa na nzuri, ambayo 2028 tutakuwa na wanafunzi takribani zaidi ya 3,000 na zaidi watakaoenda kuanza hizo shule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo kubwa na ni jambo la kihistoria, ambalo litakumbukwa katika maisha yako Mheshimiwa Profesa Mkenda na maisha ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Aendelee kuchapa kazi, tutawaunga mkono na bajeti tutaiunga mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaomba baada ya hapo iongezwe zaidi, kwa sababu mambo ni mengi, mambo makubwa, ambayo tuna dhamira ya dhati ya kuyatekeleza hayo mambo yaliyopo mbele yetu, ukizingatia vipaumbele vile vitano vilivyowekwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja na ninawatakia kila la kheri. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Stella Ikupa Alex; Mheshimiwa Yumna Mmanga Omar, Mheshimiwa Festo Richard Sanga na Mheshimiwa Kijakazi Yunus Mohamed wajiandae.

Mheshimiwa Yumna. Hapana, Mheshimiwa Stella.

Waheshimiwa Wabunge, muwe mnasajili *(log in)* mapema na kujiandaa, kabla ya kuitwa.

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa fursa ya kuchangia, muda huu. Awali ya yote nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa upendeleo wa uhai na uzima, kwangu binafsi, lakini kwa kila mmoja aliyepo mahali hapa, pia kwa viongozi wetu wakuu: Mheshimiwa Rais, Makamu wa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitumie fursa hii kumshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa mageuzi makubwa aliyoyafanya kwenye sekta ya elimu. Tukisema mageuzi makubwa ni makubwa kweli kweli. Tukianzia kwenye eneo la mitaala, mitaala ambayo inalenga kumfanya kijana wa Kitanzania, anapomaliza shule kwenye awamu yoyote, aweze kufanya chochote na si kukaa tu. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kama Watanzania tunamshukuru sana na tunampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kumshukuru Mheshimiwa Rais, kwa mambo makubwa ambayo ameendelea kuyafanya katika sekta hii ya elimu ikiwemo, *home schooling* kwa watu wenye ulemavu, pia, ongezeko la shule na ongezeko la shule za amali. Kwa kweli, Mheshimiwa Rais mambo ambayo amefanya ni makubwa sana. Kwa sisi watu wenye ulemavu, vifaa vya kujifunzia na kufundishia ameendelea kuhakikisha kwamba vinapatikana. Ongezeko pia la walimu wa elimu maalum, ameendelea kuhakikisha kwamba wanaongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii pia kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya ya kumsaidia Mheshimiwa Rais wetu kutimiza maono yake katika sekta hii ya elimu. Mawaziri hawa ni wasikivu, wana upendo, wanyenyekevu na wanafikika. Hongera sana kwa Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapoendelea kuchangia, ninaomba ninukuu Isaya 62:6(b) inasema kwamba: "Ninyi wenye kumkumbusha Bwana msiwe na kimya." Haya ambayo ninaenda kuyazungumza hapa leo si mageni, ni mambo ambayo nimeendelea kuishauri Serikali. Hivyo, kwa kuwa hata maandishi Matakatifu yanashauri kwenye kukumbusha, ama yanaelekeleza kwenye kukumbusha, basi leo nitaendelea kuikumbusha Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Elimu, Utamaduni na Michezo, imeongelea suala la upungufu wa bajeti ya mafunzo ya walimu ambao wako kazini. Katika eneo hili, Kamati imeshauri kwamba Serikali iendelee kutenga fedha kwa ajili ya mafunzo hayo. Ninaunga mkono 100% pendekezo la Kamati, kwa sababu katika walimu hawa wako walimu wa elimu maalum ambao wanakuwa wanakosa mafunzo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kwa jinsi ambavyo nimeiangalia nimeona kwamba hii ni *short term plan*, ninaona niendelee kupendekeza *long term plan*. Katika eneo hili nimekuwa nikishauri kwamba Serikali ione haja ya walimu wote kusoma elimu maalum, kwa nini? Kwa sababu kila mwalimu atakapokuwa

amesoma elimu maalum tutaondoa hii *gap* ya walimu ambayo ipo lakini pia tutamfanya mtu mwenye ulemavu asome kwenye mazingira yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuna shule jumuishi, kuna shule maalum, lakini shule hizi changamoto ni moja kwamba unakuta mtoto anakaa mbali na mahali ilipo shule jumuishi au mtoto anakaa mbali na mahali ilipo shule maalum na uwezo wa wazazi wa kumchukua kila siku kumpeleka kwenye hizi shule unakuwa haupo. Hivyo, kama walimu watapatikana wa kutosha na kila mwalimu atakuwa na uelewa ama atakuwa na *skills* za kumfundisha mtoto mwenye ulemavu, ina maana kila mtoto mwenye ulemavu atasoma kwenye mazingira yake. Kwa hiyo, niombe Serikali ione ama iweke mazingira ya kila mwalimu kujifunza elimu maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, ninaomba niendelee kushauri kwenye eneo la wasaidizi. Nimewahi kuuliza swali hapa Bungeni na ni baada ya kuona tukio moja ambalo mzazi alihamia shuleni kwenda kumsaidia mtoto wake, mwenye ulemavu. Kuna hizi *homeschooling* Serikali imefanya kazi kubwa sana, lakini kutokana na upungufu wa walimu ni ngumu watoto wote wenye ulemavu uliozidi watapata walimu wa kuwafuata majumbani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna ulemavu ambao mfano kama ulemavu wangu ni mambo machache tu ambayo yanahitajika katika usaidizi. Sasa katika hizi shule za bweni ambazo zina watoto wenye ulemavu kama watapatikana wasaidizi hata kama ni wasaidizi wawili wa kuwasaidia hawa watoto wanapokuwa shuleni mfano, ninaweza kufua, lakini siwezi kunyanyuka kwenda kuanika, siwezi kwenda kuanua, siwezi kwenda kuchukua chakula, kazi kama hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Serikali ikiajiri wasaidizi kama hawa itasaidia sana watoto wenye ulemavu kufurahia mazingira wanapokuwa shuleni ama wanapokuwa *boarding*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo pia ninaomba niendelee kuikumbusha Serikali yangu na kuiomba kwa habari ya mikopo ya elimu ya juu kwa watu wenye ulemavu. Nimekuwa nikishauri na kuomba kwamba watu wenye ulemavu ambao wanafika hatua ya elimu ya juu ama vyuo vya kati huwa wanakuwa ni wachache siyo wengi sana na nimekuwa nikiiomba Serikali kwamba mikopo hii itolewe kama ruzuku isiwe mikopo. Yaani kwa watu wenye ulemavu iwe ni ruzuku, kwa nini? Ni kutokana na hali ya maisha yetu. Maisha ya mtu mwenye ulemavu ni gharama kubwa sana, kila aina ya ulemavu ina gharama zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu mwenye ulemavu wa viungo unapoajiriwa huwezi kufika kazini kwenda kugombea madaladala, utahitaji ukodi bajaji, ni mshahara huo huo ambao pia unakatwa kwenye bodi ya mikopo. Kwa hiyo hoja yangu iko hapo, lakini kuna ulemavu wa macho wasioona atahitaji kuwa na mtu wa kuongozana naye. Kuna kiziwi atahitaji kuwa na mkalimani na vitu kama hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana Serikali iendelee kuliangalia hili na kuona ni jinsi gani basi mikopo hii kwa sisi watu wenye ulemavu itolewe kama ruzuku na isiwe mikopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo nimekuwa pia nikiishauri na kuiomba Serikali na hata wakati ule wa mabadiliko ya mitaala niliweza kupendekeza kwamba lugha ya alama iingie kwenye mitaala, ifundishwe kama somo ili tutengeneze kizazi cha Watanzania ambao tutaweza kuwasiliana na wenzetu viziwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ilivyo sasa hivi kutegemea wakalimani, si kweli kwamba kiziwi ataenda sokoni atakutana na mkalimani. Si kweli kwamba kiziwi ataenda kwenye daladala atakutana na mkalimani, ataenda kituo cha polisi atakutana na mkalimani, lakini tutakapotengeneza mtaala ama tutakapoandaa kizazi kijacho ambacho kila Mtanzania atajua lugha ya alama, ina maana itakuwa ni rahisi kuwasiliana na kiziwi popote ulipo; atakuja saluni utawasiliana naye, atakuja kwenye kituo cha polisi utawasiliana naye hospitali na maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niendelee kuiomba na kuishauri Serikali siku za usoni ione ni jinsi gani basi kila Mtanzania ama tunatengeneza kizazi ambacho kinaweza kuwasiliana na wenzetu viziwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna kitengo cha elimu maalum maoni; hata wakati ule nilishauri kwamba ianzishwe bodi au mamlaka ya elimu jumuishi. Hii itasaidia sana na ni kutokana na ukubwa wa jinsi ambavyo hii elimu imekuwa sasa hivi. Kwa kuwa kitengo kinakuwa hakifanyi kazi vizuri, lakini tukipata bodi au mamlaka ambayo itakuwa inasimamia hili eneo itakuwa ni kitu kizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niipongeze Serikali kwa kuona umuhimu wa teknolojia ya akili unde na kuchukua hatua ya kwenda kuwafundisha vijana wetu kwa mujibu wa hotuba, vijana 50.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kushauri kwamba, vijana hawa wanapokwenda huko na kurudi wawe na kitu cha kufanya kwa sababu vitu ambavyo wanakwenda kufundishwa huko ni vitu *sensitive*. Sasa kama atakwenda huko atarudi mtaani akaanza kukaa tu na kuzagaa bila shaka tunakwenda kutengeneza kitu cha hatari sana kwenye jamii yetu. Kwa hiyo, Serikali ione ni kwa jinsi gani ambavyo vijana hawa wakienda basi wanakuwa wameandaliwa mazingira ya kutumia kile ambacho wamekipata huko kwa manufaa mazima ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya machache, ninaomba niunge mkono hoja na ninaomba kuwasilisha. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Stella Ikupa ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge kabla hatujaendelea na michango ya Wabunge wengine tuna wageni ambao wapo muda huu katika Bunge letu.

Ninaomba tuwatambue kwenye Jukwaa la Mheshimiwa Spika, wapo wageni wa Mheshimiwa Profesa Adolf Faustine Mkenda, Waziri wetu wa Elimu, Sayansi na Teknolojia ambaye ni Mheshimiwa Dogo Iddi Mabrouk, Makamu Mwenyekiti Jumuiya ya Wazazi wa CCM Taifa. Karibu sana. *(Makofi)*

Yupo ndugu Khadija Shabani Kangero, Mjumbe wa Kamati ya Siasa kutoka Rombo. Karibu sana. *(Makofi)*

Wageni wengine ni wanafunzi kutoka Chuo cha Ufundi Stadi *VETA*. Karibuni sana wanafunzi wetu kutoka *VETA*. *(Makofi)*

Wapo wadau wa elimu *Faith Based Organization* kutoka Dar es Salaam na Taasisi ya *Organization for Community Development* kutoka Dar es Salaam. *(Makofi)*

Ndugu na jamaa zake kutoka Jijini Dar es Salaam. Ninaona hawajaingia bado.

Wageni wanne wa Mheshimiwa Amour Seif Abdalla, wafanyabiashara kutoka Zanzibar. Karibuni. *(Makofi)*

Wageni watano wa Mheshimiwa Hamisi Shabani Taletale, walezi wa *Day Care Center* kutoka Jijini Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Yohana Stephen Msita, wapiga kura wake kutoka Mkoani Singida. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni ambao wametembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, wanachama 36 kutoka Chama cha Wakutubi Tanzania. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wanafunzi 112 na Wakufunzi saba wa Shule ya Sekondari Lukundo kutoka Jijini Dodoma. Karibuni sana wanafunzi wetu. Karibuni sana wageni wetu wote katika Bunge letu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Mheshimiwa Yumna Mmanga Omar, Mheshimiwa Festo Richard Sanga na Mheshimiwa Kijakazi Yunus Mohamed ajiandae.

**MHE. YUMNA MMANGA OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema ya uhai na uzima, lakini pia kwa kutupatia Rais Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote tunatambua jitihada zake uongozi wake ulio thabiti na maono yake ya kuyaletea maendeleo Taifa hili. Nitakuwa sijautendea haki huu muda ikiwa nitaacha kuwapongeza Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda sambamba na Naibu Waziri Mheshimiwa Wanu Hafidh Ameir, pamoja na uongozi mzima wa Wizara ya Elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli watu hawa wamekuwa wakizitendea haki nafasi zao. Nami kama Mjumbe wa Kamati nimepata fursa ya kutembelea miradi mbalimbali na nimejionea ni kwa kiasi gani wanatekeleza elimu jumuishi. Lakini tu nitoe msisitizo kwamba jambo hili liendelee kwamba miundombinu hii ya elimu iwe *inclusive from design and not from by correction*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoandaa miundombinu jumuishi kuanzia hatua za awali za mchoro tunahakikisha kwamba hata baadaye tunaepuka gharama za ziada. Lakini pia majengo haya hayamnufaishi mwanafunzi tu hata wafanyakazi wa pale. Tuna wanawake wanafanya kazi wanaweza wakapata ujauzito; tuna watu wafanyakazi wanaweza wakapata changamoto za maradhi. Tunapoweka miundombinu rafiki ya ku-*access* jengo zima tunahakikisha kwamba Taifa hili halimwachi mtu yeyote nyuma katika kuleta maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye mchango wangu kwanza kabisa ningependa kuishauri Serikali kwamba itekeleze suala zima la *assessment early childhood assessment* ili kuweza kubaini changamoto za watoto wenye ulemavu katika ngazi ya awali. Sote

tunatambua kwamba tutakapomtambua mtoto mapema ni rahisi kumwekea mazingira rafiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafiti mbalimbali *UNESCO* na *UNICEF* za mwaka 2024 hadi 2026 zinathibitisha kwamba mtoto ambaye anatambuliwa mapema ni rahisi kumwekea mazingira rafiki na anastawi zaidi kielimu. Kuna watoto ambao tunawaona ni watoro, tunawaona ni wazembe, tunawaona kwamba hawataki kusoma lakini pengine wame-*delay speech*, pengine wana *autism* pengine lakini tumeshindwa kuwatambua. Kwa hiyo, ni ombi langu kwa Serikali kwenda kutekeleza miradi hii ya kuwatambua watoto mapema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishauri Serikali vilevile kwenye suala zima la *inclusive educational data*. Wenzangu wamegusia kidogo nami niongeze msisitizo kwamba tunahitaji takwimu za watoto wenye ulemavu, siyo takwimu tu ambazo zitaonyesha *enrollment* mwaka huu tumedahili wanafunzi wangapi, lakini takwimu hizi zitatusaidia kujua ni aina gani ya watoto wenye ulemavu? Wako wapi? Tupeleke vifaa gani visaidizi? Tunapoandaa bajeti hatuandai bajeti kwa ujumla, lakini tunaandaa bajeti *specific* kwa kujua wapi kunahitajika nini kwa kiwango gani na huu ndiyo uwekezaji wa elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua kwamba elimu ni ufunguo wa maisha, lakini ndiyo chachu ya maendeleo. Tunapowekeza kwenye watoto wenye ulemavu tunahakikisha kwamba ile *human investment* hatuitupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mtoto aliyepata elimu ni fursa na kila mtoto ambaye tumemwacha nyuma ni fursa tuliyoitupa. Kila mwanafunzi ana sababu yake ya kuwepo hapa duniani. Ana talanta zake, ana vipaji vyake na ana uwezo mkubwa wa kuchangia maendeleo ya Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi ni wito wangu ni maombi yangu kwa Serikali kuona ni namna gani wanaanzisha takwimu hizi zitatusaidia kwa kiasi kikubwa sana kuhakikisha kwamba hii bajeti siyo

tu jumla jumla, lakini inakwenda kugusa kwa uhalisia, kuangalia ni aina gani ya *disability* ni wapi wanapatikana na ni kwa kiasi gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nigusie pia suala la walimu. Wenzangu wametangulia, lakini nami nitaweka msisitizo. Ninatambua ni kwa kiasi gani wameongeza jitihada kuhakikisha kwamba walimu wa elimu maalum wanaongezeka. Hata hivyo, kuna haja ya kuongeza jitihada kwamba hapo tulipo tuzidi zaidi na zaidi kwa sababu mahitaji yake ni makubwa, lakini pia ni katika kuweka mazingira rafiki kwa watoto hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *disability* ni *diverse* na ni *broad*. Siyo jambo ambalo mtu anasomeshwa kwa *topic* moja darasani akaweza aka-*accommodate* wanafunzi. Tuna ulazima wa kuhakikisha kwamba somo hili wanafundishwa walimu wote tena siyo tu *topic* moja, lakini iwe kozi kabisa hata kama ni kozi atai-*carry* kwa *semester* zote kwa sababu ya ukubwa wake na mapana yake na kuhakikisha kwamba kila mwanafunzi anaweza kupata mwalimu atakayemsaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami niungane na mwenzangu kwa kuunga mkono hoja hii na kuomba kwamba bajeti ikiwezekana iongezwe kwa sababu mahitaji ya watu wenye ulemavu si gharama bali ni fursa ya kuleta maendeleo kwa watu wenye ulemavu na Taifa hili. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yumna Mmanga Omar Ahsante sana. Mheshimiwa Festo Richard Sanga, atafuata Mheshimiwa Kijakazi Yunus Mohamed na Mheshimiwa Amina Mussa Mkumba ajiandae.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza nipende kumpongeza Mheshimiwa Waziri Profesa Mkenda kwa kazi kubwa ambayo anaifanya, ameituliza Wizara, Wizara imetulia. Tunaona matokeo, tunaona mambo yanaenda hakuna heka heka. Hongera sana Mheshimiwa Waziri na hii ni *tendency* yake hata alivyokuwa Katibu

Mkuu na hata sehemu zote alizopita amekuwa akifanya vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze pia Mheshimiwa Wanu Hafidh kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya, tumeona wakizunguka. Hata hivyo, nichukue nafasi hii pia kuwapongeza watendaji wenzake ambao wanafanya nao kazi. Ukiangalia Katibu Mkuu wa Baraza la Mitihani anafanya kazi nzuri sana, lakini pia watu wa *TEA* tumeona na wamefika hadi Makete. Dkt. Kishepa kama sikosei Mkurugenzi Mtendaji wa *TEA* amefika hadi Makete kwa ajili ya kazi, tunawapongeza kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niseme bajeti yetu ni bajeti nzuri tuna trilioni 2.39 na katika trilioni 2.39 unazungumza trilioni 1.69 zinaenda kwenye maendeleo. Huo ni utofauti mkubwa sana katika Wizara nyingi ambazo tumepita. Hongera sana kwa Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, fedha ni ndogo sana ambayo inatoka kwa washirika wa nje. Unazungumza 359,000,000,000. Ni fedha ndogo ambayo na sisi kwetu inatuonyesha kwamba tunajikwamua kwamba tunakwenda kukua. Ni hili kubwa kwetu kwa sababu ukiangalia Wizara zingine fedha za washirika hazijaja, kwa hiyo na sisi tumetenga fedha ndogo ili tusiwategemee zaidi. Tafsiri yake ni kwamba tuna malengo makubwa kwa ajili ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii pia kuipongeza Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Watanzania ni lazima wafahamu kuna mambo ambayo kama nchi tumeyapitia, katika ukuaji wa elimu yetu unazungumzia nchi ambayo mwaka 1995 ilikuwa na shule za msingi 335 tu, lakini unazungumza leo shule za msingi ziko 18,158. Tafsiri yake kuna kazi kubwa ambayo Serikali ya Chama Cha Mapinduzi imefanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unazungumzia nchi ambayo mwaka 1995 wakati sera ya elimu inaanzishwa kulikuwepo na shule za sekondari 482, lakini nazungumza leo mwaka 2026 chini ya Serikali ya Chama Cha Mapinduzi tumejenga shule 5,092. Ni mapinduzi

makubwa sana ambayo kama nchi tumeyafanya na tuna kila sababu vijana ambao wanatusikiliza wajue nchi kuna sehemu imetoka na kuna sehemu inakwenda na ni jambo la kujivunia katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unazungumza nchi ambayo tulikuwa na walimu chini ya 10,000 mwaka 1995. Leo tunazungumza walimu 274,441 ambao wako kwenye ajira na wanaitumikia nchi yetu, kutoka walimu chini ya 10,000 mwaka 1995. Tafsiri yake ni kwamba nchi yetu imeenda mbali na imesogea mbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unazungumzia nchi ambayo mwaka 1995 tulikuwa na vyuo vikuu vitatu, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, *Open* mnakumbuka? Sasa hivi tunazungumzia zaidi ya vyuo vikuu 50 na kitu ambavyo vimejengwa katika nchi yetu na Serikali inaendelea kujenga kwenye mikoa mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni mapinduzi ya elimu ambayo vijana wa nchi lazima wafahamu kwamba Taifa letu limesogea, Taifa letu limesonga. Pale wanapojenga hoja kwenye vijiwe wanavyokaa wajue kwamba nchi yetu kuna hatua kubwa sana imepigwa na imepigwa chini ya Serikali ya Chama Cha Mapinduzi. Kwa hiyo, tuna haki ya kuendelea kuaminiwa, tuna haki ya kuendelea kuiamini Serikali na hiki ndiyo chama ambacho kinaweza kufanya mambo makubwa na yenye mabadiliko kwenye Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unazungumzia nchi ambayo ilikuwa na *VETA* moja tu ambayo ilijengwa ya kwanza ndani ya Wilaya ya Makete. Ndiyo ilikuwa *VETA* yetu ya kwanza, lakini saa hizi tunazungumzia nchi ambayo inaenda kujenga *VETA* wilaya zote katika nchi yetu. Hili ni jambo kubwa sana ambalo tumelifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amefanya pia mabadiliko kwenye mambo ya *scholarship*, mitaala ya elimu wamefanya *revolution* kubwa sana kwenye eneo hili wana kila sababu kuipongeza Serikali yetu kwa kazi kubwa ambayo wameifanya, lakini zaidi kashfa za kuvuja kwa mitihani kumekwisha kabisa. Hili ni jambo kubwa na ni jambo ambalo linaonyesha u-*serious*

na ndiyo maana nimempongeza pia Katibu Mkuu wa Baraza la Mitihani kwamba tumeona uvujaji wa mitihani haupo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niko hapa kuonyesha kwamba lazima tujue nchi ilikotoka, ilipo na inapokwenda kwamba kuna vitu ambavyo tumevifanya katika nchi yetu. Kwa hiyo mtu akikaa sehemu akasema Serikali ya Chama Cha Mapinduzi haijafanya kitu? Tuna takwimu za kumkataa na tunamshinda. Watu wanasema kama hujafanya utafiti usijenge hoja, jenga hoja kama umefanya utafiti. Basi mtu yeyote anayepingana na takwimu hizi na yeye alete takwimu zake ambazo zinaonyesha Serikali yetu haijafanya kitu, tunaamini CCM imefanya kazi kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo machache ya kushauri; jambo la kwanza, ninalotaka kukushauri Mheshimiwa Waziri ni kwenye kuimarisha nchi katika mambo ya utafiti. Ninajua Mheshimiwa Waziri kwenye ripoti yake amezungumza wanakwenda kufanya miradi ya utafiti 1,390.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yoyote duniani inawekeza katika utafiti, katika moja kati ya nchi za Afrika, Afrika Kusini ndiyo inayoongoza kwenye kuwekeza kwenye utafiti. Haya maandiko mbalimbali ambayo wasomi wetu wanaandika wanayawekeza kwenye utafiti Mheshimiwa Waziri ni vema tukayatumia katika kujibu hoja za matatizo mbalimbali kuliko wakiyaandika na kwenda kuyaweka kwenye ofisi itakuwa haileti tija. Kwa hiyo, ninatamani kwamba tafiti mbalimbali ziendelee kufanyiwa kazi ili maeneo mbalimbali yaendelee kuibua na fursa kwa ajili ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ambalo nataka kumshauri Mheshimiwa Waziri, tuna hawa vijana ambao wako kwenye vyuo wanasoma wana changamoto za maeneo ya *field* au *internship*. Hili jambo limekuwa na changamoto kubwa, vijana wengi wanavyopita kipindi cha kwenda kufanya *field* mwaka wa kwanza au wa pili au wa tatu wamekuwa wakipata changamoto kwenda kuandika barua maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri Wizara kuna nyakati fulani ilizungumzwa Serikalini kwamba wanataka taasisi za Serikali zihusianishwe moja kwa moja na hivi vyuo ili mtu akitaka kwenda *field* basi aende akafanye *field* kwenye maeneo ya taasisi za Serikali lakini pia kwenye miradi ya Serikali kwa sababu kuna watu wanasomea *engineering,* lakini anahangaika eneo la kufanya *field.* Kwa hiyo, ninatamani tuwarahisishie wanafunzi wetu wa vyuo vikuu vile vya kati na vile vya juu kuhakikisha kwamba wanapata maeneo ya *field* kiurahisi ili wasisumbuke na iweze kutusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapompeleka kwenye ofisi za umma tafsiri yake ni kwamba unamwandaa kwamba baadaye aje kuwa mtumishi bora na mtu ambaye anazingatia maadili. Kwa hiyo, ninatamani sana hili Wizara waliangalie pamoja na Wizara ambazo ni mtambuka kama Wizara ya Utumishi waweze kushirikiana kwenye kuhakikisha kwamba vijana hawa wasiteseke maeneo ya kufanya f*ield,* basi vyuo na ofisi za Serikali, miradi ya Serikali na taasisi za Serikali ziweze kuwachukua ili waweze kufanya *field* kirahisi na baadaye kuendelea kufanya shughuli zao za kimasomo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo Mheshimiwa Waziri, Watanzania huko nje ukizungumza kuhusu elimu wanajua ni Wizara ya elimu. Suala la TAMISEMI huwa hawalifikirii sana, wanaiwaza ya Wizara ya elimu. Sasa ninatamani kujua kwamba Mheshimiwa Waziri kama nchi tumesambaza umeme sana tumewafikia watu wengi sana kwenye umeme, tumefikia karibu shule nyingi sana, uhitaji wa *computer labs*, uhitaji wa *photocopy* mashine, uhitaji wa vitu ambavyo vina *ICT facilities* ni mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninamwomba Mheshimiwa Waziri ili walimu wakuu wetu wasipate shida ya kuhangaika kutafuta *facility* za kusaidia aidha kuzalisha mitihani na kufanya kupakua vitabu na maeneo mengine, basi Wizara yako ifanye sensa ya kujua ni shule ngapi zina uhitaji ili washirikiane na TAMISEMI kuhakikisha watu wanaweza kupata hizo *facility* ili iweze kuwasaidia Mheshimiwa Waziri. Hilo ni eneo ambalo ninatamani kukushauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine Mheshimiwa Waziri ni kwenye eneo la Bodi ya Mikopo. Mheshimiwa Waziri ninajua wameongeza idadi ya watu kwenye Bodi ya Mikopo kwa sababu Mwaka wa Fedha 2025/2026, wanafunzi waliokuwa wananufaika na mikopo walikuwa ni 252,773 na Mwaka wa Fedha 2026/2027, wameongezeka 292,981. Ni kweli idadi hii ya wanafunzi imeongezeka, lakini takwimu ya wanafunzi wa vyuo vikuu inazungumza tuna wanafunzi 252,000 walioko kwenye vyuo vikuu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafsiri yake kuna nusu ya wanafunzi hawanufaiki na Bodi ya Mikopo. Kwa hiyo, tunahitaji kutafuta Mfuko wa Elimu ile hoja ambayo Wabunge wengi wameizungumza nami ninachagiza tutafute Mfuko wa Elimu ambao tutautungia sheria, tunaufanyia *ringfencing* ili fedha hizo ziweze kusaidia watoto wengi zaidi wa Kitanzania kupata mikopo. Tofauti na hapo Mheshimiwa Waziri tutakuwa na idadi kubwa pia ya vijana ambao wako mitaani wana hamu ya kusoma, lakini wamekosa mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa jinsi ambavyo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anafanya kazi vizuri, basi tuwekeze nguvu hapa kwenye kuhakikisha kwamba tunapata fedha za kuwasaidia wanafunzi wenzetu. Mimi ni mnufaika mojawapo wa mkopo nilivyokuwa ninasoma Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaamini kabisa kuna wanafunzi wengine au kuna watoto wengine watu maskini wako nyuma yetu ambao wanatamani kupata fursa hii, lakini uchache wa fedha unawafanya wakose. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri awekeze hapa ili tuendelee kuwaokoa vijana hao. Kwa sababu ndiyo *Gen Z* wenyewe tunaowazungumzia, wana hamu ya kwenda kusoma, lakini sasa wanakosa mikopo. Kwa hiyo, tuliangalie hilo jambo kwa ukaribu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu nyingine ambayo Mheshimiwa Waziri siku zote anaifahamu, nilichangia siku zile tunawashukuru kwa kujenga vyuo. Tumejenga vyuo maeneo mengi ya nchi yetu, hadi Njombe tumepata chuo kikuu lakini Mheshimiwa Waziri atakumbuka nilijenga hoja siku moja hapa kwamba ukienda

Taifa la China wamejenga *specialization* ya vyuo kwamba ukienda eneo fulani vinapatikana vyuo vya vinahusisha labda sekta cha kilimo tu, ukienda eneo fulani vinahusika na eneo fulani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatamani sana msingi huu uendelee kwamba ukija Njombe basi ujue ni chuo ambacho kinajikita kwenye mazao ya misitu na mazao ambayo yanatokana na *let's say* maparachichi na mambo mengine kuliko tukafanya mchanganyiko kwenye vyuo vikuu kwamba. Kwa mfano, unakuta Mwalimu Nyerere alianzisha Sokoine kwa ajili ya kilimo lakini leo ukienda Sokoine wanatoa utalii, wanatoa *education*, wanatoa vitu tofauti tofauti. Hivi vitu kama nchi tunataka kuijenga, ni kweli ulinijibu siku ile kwamba *its universal* kwa sababu *university is Universal,* akaniambia kwamba vyote vinaweza vikaingia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatamani tuwe na *model* yetu kama nchi kwamba chuo fulani kina-*deal* na jambo fulani, *MUHAS* ana-*deal* na afya, basi tukija Sokoine ana-*deal* na kilimo tukienda kwenye Chuo cha Mzumbe tujue wana-*deal* na kuandaa watu kuwa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, huo ndiyo ushauri wangu. Ninaona muda umenikimbia, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Festo Sanga. Nilimtaja Mheshimiwa Kijakazi Yunus Mohamed; Mheshimiwa Amina Mussa Mkumba na Mheshimiwa Regina Henry Mikenze, wajiandae.

**MHE. KIJAKAZI Y. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Bajeti ya Wizara hii muhimu sana kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema ambaye amenipa kibali leo hii kuweza kusimama hapa ili niweze kuchangia Bajeti ya Wizara hii ya Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa dhamira yake ya dhati ambayo tunaiona. Tunaona kabisa kwamba amedhamiria kuinua ama kuboresha sekta ya elimu hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikisema hivyo ninamaanisha mengi ambayo tumeyaona na mengi yamesemwa hapa, lakini niseme, kwa mfano, amejenga miundombinu ya elimu nchi nzima. Hali hii inasababisha wale wanafunzi ambao wametoka kwenye mazingira duni, ambao nyumbani pako vibaya, lakini kutokana na mazingira mazuri ya shuleni inamlazimu au anavutiwa kwenda shuleni kutokana na mazingira mazuri ya shule. Kwa hiyo, tumpongeze na tumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kitu hiki kikubwa ambacho anakifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumpongeze pia Mheshimiwa Rais moja kati ya jambo kubwa ambalo amelifanya ambalo limeonesha kwamba kweli yeye ni mama na ana uchungu na watoto wake, ni kitendo cha kuruhusu wanafunzi ambao wamepata ujauzito wakiwa shuleni, kurejea shuleni. Tumeona wapo wanafunzi ambao wamerejea katika vyuo vya ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii wanafunzi wale hususan waliotoka kwenye maisha duni anapokwenda kupata mafunzo kwenye shule za ufundi maana yake ni kwamba, akitoka pale ataweza kwenda kujiajiri na kukomboa familia yake. Kwa hiyo, hiki ni kitu kikubwa sana tunampongeza Mheshimiwa Rais na tunaiona dhamira yake ya dhati ya kuhakikisha kila mtoto wa Kitanzania anapata elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii pia kumpongeza sana Waziri kaka yangu Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda. Jamani Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote ni mashuhuda. Tunaona tangu Mheshimiwa Mkenda amechukua nafasi hii tunaiona dhamira yake ya dhati ya ya kumsaidia Mheshimiwa Rais kuyabeba maono yake na kuyatekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona mageuzi makubwa ambayo yanafanyika katika sekta ya elimu. Tumpe maua yake na tumpongeze na tunakushukuru sana Profesa kwa kuonesha kwamba wewe kweli ni msaidizi wa Mheshimiwa Rais. Dada yangu Mheshimiwa Wanu anafanya kazi kubwa, kazi nzuri na ameanza vizuri sana. Nimtie moyo kwamba anaweza, anamsaidia vizuri Profesa Adolf Mkenda. Aendelee kukaza buti safari hii ndiyo kwanza imeanza. Sina dhamira ya kueleza *CV* yako Mheshimiwa Mariam hapa ameeleza ila nitumie nafasi hii kumpongeza sana. *(Makofi)*

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Kuna taarifa

**TAARIFA**

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Wakati dada yangu anaendelea kumeza mate hapa ninataka nimwongezee taarifa tu anaposema anawashukuru viongozi wa Wizara ya Elimu kwa dhamira yao njema ya kusaidia watoto maskini katika nchi hii. Hivi juzi kulikuwa na jambo ambalo limesambaa karibu nchi nzima ya mtoto ambaye amemaliza *form six* na kupata *division one* lakini akawa anaokota makopo Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampa taarifa msemaji kwamba Mheshimiwa Waziri alimpigia simu *live* kwenye vyombo vya habari ameongea naye na yule kijana amepokelewa na *University of Dar es Salaam* anaendelea kusaidiwa. Kwa hiyo, huu ni uthibitisho wa dhamira njema aliyokuwa nayo Profesa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Unaipokea hiyo taarifa Mheshimiwa Kijakazi.

**MHE. KIJAKAZI Y. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa mikono miwili na unyenyekevu, ninaipokea taarifa hii na niliifuatilia taarifa ile na ni mmoja kati ya watu ambao nilizungumza na Mheshimiwa Profesa Mkenda na kumpongeza sana kwa jambo lile ambalo alililifanya. Kwa hiyo, ninaipokea na ninaendelea kupongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii inafanya mambo mengi sana, mimi ni shuhuda kwa sababu ni Mjumbe wa Kamati. Nimetembelea miradi kadhaa kwa mfano tumekwenda Tanga. Tanga pale kimejengwa chuo ambacho kipo katika eneo la msitu. Hii ni kuonesha kwamba Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan hachagui wala habagui, popote walipo Watanzania anapeleka huduma ambayo eneo hilo inastahili kufika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekwenda, tumeona kazi ambayo inafanyika, lakini haya yote ambayo yanafanyika kabla sijasonga mbele nikipongeze sana Kitengo cha Habari, wanahabari wenzangu wa Wizara hii Kitengo ambacho kinaongozwa na dada yangu Sylvia. Wanafanya kazi kubwa sana, mengi tunayafahamu kupitia vyombo vya Habari, lakini nani ambaye anapanga mikakati hii kuhakikisha vyombo vya habari vinatoa taarifa hii ni Kitengo cha Mawasiliano au Kitengo cha Habari cha Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwapongeze wanafanya kazi nzuri ila niwaombe wakaze buti waongeze kutoa taarifa ili Watanzania wajue kwamba Rais wetu anafanya kazi gani, lakini Serikali yetu inafanya nini katika kuboresha maisha ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana au niipongeze Serikali kwa kutuletea chuo kikuu pale Lindi Kampasi ya Ngongo na Ruangwa. Kampasi hii ambayo itakwenda kugharimu takriban shilingi 13,000,000,000 za Kitanzania. Ujenzi umeanza, na unaendelea vizuri. Kukamilika kwa ujenzi ule ambao tulitarajia ukamilike mwaka huu na kuweza kuanza kudahili, chuo kile kitachukua wanafunzi takribani 18,000. Wanafunzi 18,000 huu ni uchumi katika Mkoa wa Lindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini ninasema uchumi? Wote tunafahamu wanafunzi wale watakapokuja katika Mkoa wa Lindi kwa sababu hatutarajii kupata wanafunzi kutoka Mkoa wa Lindi peke yake. Wanafunzi kutoka mikoa mbalimbali watakuja kusoma katika chuo kile. Kwa hiyo, watakapokuja watatuletea uchumi kwa sababu wataishi kwenye nyumba zetu, watapanga. Watakula chakula

ambacho mamalishe wetu wanapika. Watafanya biashara kwenye maduka jirani na chuo kile au maeneo wanayoishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, uchumi wa Lindi ambao mpaka sasa ni ukweli usiopingika bado uko chini utaendelea kukua. Kwa hiyo, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa jitihada hii ambayo ameifanya. Niombe kwa Mheshimiwa Profesa Mkenda chuo kile mpaka sasa kiko takriban 70% na kitu na Mheshimiwa Waziri Mkuu tulikuwa naye Lindi alikuja kuweka jiwe la msingi pale mapema mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Waziri chuo kile kikamilike, kwa sababu kama tuko *almost 70%* tunaanza kupoteza matumaini kwamba je, kweli chuo kitakamilika? Kweli udahili utafanyika? Kwa hiyo, niombe na ninawaamini sana Watendaji wa Wizara hii, ninaomba twende tukakamilishe chuo kile ili Wanalindi tuweze kunufaika na chuo kile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie mpango wa Serikali wa kujenga Vyuo vya *VETA* katika Wilaya 64. Tumetembelea baadhi ya vyuo ikiwemo chuo kimoja kilichopo Mkoa wa Morogoro. Tunaona kwamba kazi hii bado inasuasua. Dhamira ya Serikali tunajua ni njema kabisa, lakini nimesimama hapa kuomba tuongeze *speed* ya ujenzi wa vyuo hivi. Ukiangalia changamoto kubwa ambazo zinachelewesha ujenzi wa vyuo hivi vya *VETA* ni pesa. Kule kwetu Lindi tunacho Chuo cha Kilwa, Wilaya ya Kilwa ujenzi unaendelea uko takriban 69%. Tunacho Chuo cha Liwale tunacho chuo Nachingwea, hivi vyote bado hali ipo chini sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunategemea sana vyuo hivi kwa sababu kama nilivyosema uchumi wetu upo chini. Tunategemea kwamba vijana wetu watakapokwenda kusoma kwenye vyuo hivi wakipata ujuzi, basi wataweza kujiajiri, watajikomboa wao na familia zao na Mkoa wetu wa Lindi na Taifa kwa ujumla. Kwa hiyo, niiombe sana Serikali twende tukajitahidi kutafuta pesa tupeleke kwenye vyuo hivi vianze kufanya kazi, vijana wetu tuwakomboe na ajira waweze kupata kipato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Chuo cha Ruangwa kwa miaka miwili mfululizo vijana wetu walikuwa wanapata *scholarship* inayotokana na Ofisi ya Waziri Mkuu. Ile *program* ni *program* ya uanagenzi. Sasa kwa mwaka huu hatujapata na kwa kweli programu ile ilikuwa inanufaisha vijana kutoka Wilaya ya Liwale, Wilaya ya Ruangwa yenyewe na Wilaya ya Nachingwea, lakini mwaka huu kwa kukosa *scholarship* ile kuna vijana wengi ambao wameshindwa kupata elimu hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakuwa shuhuda hapa kusema kwamba programu hii miaka miwili iliyopita wapo vijana ambao walinufaika. Juzi hapa nilikuwa Ruangwa nilifuatwa na baadhi ya vijana walikuwa watatu ambao walikuwa wanatoa ushuhuda kwamba programu ile iliwapa ambayo imewapatia ajira mpaka sasa. Wanaendelea na shughuli zao, wanaongeza kipato kwenye familia yao na wanasaidia familia zao. Kwa hiyo, nimetoa huu ushuhuda kutaka kuonesha tu ni kwa namna gani kwamba programu hii ni muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Waziri mwaka ujao waturejeshee hii *program*. Kama nilivyosema na nitarudia tena kwamba sisi Mkoa wa Lindi bado tuko nyuma sana kiuchumi. Familia zetu bado ni duni. Uwezo wa kulipa hata kile kidogo tu kinawashinda. Kwa hiyo, tunaomba watutazame kwa jicho la huruma na jicho la umuhimu waweze kuturudishia ile *program*.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. KIJAKAZI Y. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ahsante sana, ninaunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kijakazi. Tunaendelea na Mheshimiwa Amina Musa Mkumba, Mheshimiwa Regina Henry Mikenze na Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi wajiandae.

**MHE. AMINA M. MKUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Awali ya yote nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa kuweza kuchangia hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nianze kwa kumpongeza sana Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa mapinduzi makubwa ambayo ameyafanya katika sekta ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto za mifumo ya elimu nchini zimekuwa ni *discussion* ya muda mrefu. Hoja kubwa imekuwa ni *gap* kubwa kati ya kile kinachofundishwa darasani na soko la ajira. Hata hivyo, tunamshukuru Mheshimiwa Rais ameweza kufanikisha kwamba sasa elimu iendane na soko la ajira, lakini elimu iendane na maendeleo ya sayansi na teknolojia. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaipongeza sana pia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Mheshimiwa Waziri kasi yake tunaiona wewe ni *man of action,* hongera sana. Pia, tunampongeza sana Mheshimiwa Wanu Hafidh Ameir. Juhudi zake tunaziona tunamwona akikimbia kimbia huku na kule kuhakikisha kwamba elimu yetu inakuwa ni elimu yenye tija. Hongera sana kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashukuru sana vile vile kwa kuweza kutekeleza maoni ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, Toleo la 2013. Kupunguza muda wa elimu ya lazima ya miaka 10 katika elimu ya msingi kutoka miaka saba kwenda miaka sita, hili ni jambo la msingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitaalam tunaambiwa kwamba mtoto anajifunza kwa haraka sana akiwa na umri mdogo, lakini pia akimaliza elimu yake akiwa na umri mdogo anakuwa na muda wa ziada wa kuweza kufanya mambo mengine, lakini pia atakuwa na muda mrefu katika kulitumikia Taifa lake. Kwa hiyo, niwapongeze sana hili ni jambo la msingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nimpongeze sana katika kutumia Lugha ya Kiswahili katika kufundishia masomo ya amali. Hiki ni kitu cha msingi sana. Watanzania wengi tunatumia Kiswahili, Watanzania wengi tunaelewa Kiswahili. Kwa hiyo, hii itamwezesha mwanafunzi kuweza kuelewa kile kitu ambacho anafundishwa, ataweza kuhoji, ataweza kujadili na ataweza kuwasiliana na wenzake. Kwa hiyo, hii itakuwa ni elimu yenye tija kwa sababu mwanafunzi anaielewa. Lengo la masomo haya ya amali ni kuweza kutatua jamii inayomzunguka. Kwa hiyo, Lugha ya Kiswahili ninaamini itafanikisha elimu hii. Kwa hiyo, nipongeze sana suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni kuwa na mikondo miwili. Mkondo wa kawaida wa nadharia ambao tumezoea, lakini mkondo wa amali, hapa mtoto anaenda kusomea ujuzi. Hii itasaidia sana kuhakikisha kwamba mtoto anapomaliza elimu yake anaenda kupata ajira, atakuwa na sifa za kujiajiri au kuajirika. Kwa hiyo, hili ni jambo la msingi sana, ninaomba niwapongeze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni matumizi ya teknolojia akili mnemba na hizi *artificial intelligence*. Hizi ni muhimu sana. Haiwezi kuchukua nafasi ya mwalimu, lakini inakuwa ni *personal assistant* inamsaidia mwanafunzi pale ambapo atakuwa mbali na mwalimu na pia inamsaidia mtoto. Watoto wametofautiana, kuna watoto ambao ni *quick learner* na kuna watoto ambao ni *slow learner. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii *artificial intelligence* itamsaidia yule mtoto ambaye ni *slow learner* kuweza kujifunza kadri ya uwezo wake na yule *quick learner* pia, itamsaidia kwa hiyo, hiki ni kitu kizuri sana, ninakipongeza. Kingine ambacho ninakipongeza sana ni shule za wasichana za sayansi za mikoa. Lengo la Mheshimiwa Rais hapa ni kuwa na watoto wa kike wengi madaktari, wahandisi na wanasayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapongeza sana hapa na niseme kwa niaba ya wanawake, wanawake wengi sana wanatamani Ma-*Gynecologists* wote wangekuwa ni wanawake. Tunakutana na mazingira magumu sana, unaenda hospitali unakutana na daktari mwanaume, kuna yale maswali yake ya kidaktari anakuuliza, halafu

baadaye anakwambia toa nguo panda kitandani. Kwa kweli, huwa ni kitu kigumu sana. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongezae sana Mheshimiwa Dkt. Samia. Ninaomba sana Wizara ihakikishe kwamba, inawawekea miundombinu watoto hawa, madaktari hawa ili waweze kufikia ndoto zao na ndoto ya Mheshimiwa Rais ya kuwa na madaktari wengi wanawake iweze kutimia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwenye suala la *Samia Scholarship,* hili ni jambo zuri sana na la huruma kwa watoto wa kike. Aliwahi kusema Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba, akasema, "*Sasa mtoto wa maskini anao uwezo wa kuwa daktari, anao uwezo wa kuwa mhandisi*" kwa hiyo, ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa jambo hili la *Samia Scholarship.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni mpango wa kutoa mkopo kwa wanafunzi 292,981 hii ni hatua kubwa katika elimu yetu ya juu. Hapa labda nitoe ushauri kwa Wizara, tumekuwa na changamoto kubwa sana katika mikopo. Ninaomba Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wasimamie, wahakikishe kwamba, hii mikopo inatolewa kwa haki na uwazi. Lengo ni kuwasaidia watoto ambao wana hali ya chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na changamoto za hapa na pale wanapata na wengine wanakuwa hawapati. Mtoto anatoka huko anajua nikifika kule nitapata mkopo. Kwa hiyo, ninawaomba wahakikishe kwamba, mikopo hii inapatikana kwa watoto ambao wamekusudiwa. Pia, hata ile *amount* ambayo inatolewa ikidhi basi, kwa sababu, watoto wa maskini wengi hawana msaada wa ziada zaidi ya hii mikopo. Kwa hiyo, iwe ni mikopo yenye tija, ambayo itam-*support* mtoto moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapongeza sana Mpango wa *VETA* katika wilaya zote na ninashukuru Kibiti tunayo *VETA,* lakini na yenyewe bado inasuasua. *VETA* hii ni muhimu sana katika Wilaya yetu ya Kibiti, ndicho kivuko cha vijana, tuna vijana wengi ambao ni wasomi hawana kazi wako pale kwa hiyo, ninaiomba Wizara wahakikishe kwamba, *VETA* ya Wilaya ya Kibiti inakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kozi zitakazotolewa katika *VETA* ya Wilaya ya Kibiti ziendane na *resources* ambazo tukonazo pale Kibiti. Sisi tuna misitu, tuna mazao ya kilimo na mazao ya Bahari kwa hiyo, katika kozi watakazotoa wahakikishe kwamba, tunapata kozi ambazo zinaendana na *resources* ambazo tuko nazo pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapongeza sana katika suala la tathmini na mitihani. Hii itawapa sana watoto moyo wa kusoma kwamba, sasa hivi mtoto atapimwa ujuzi, anajua nini, tofauti na mwanzo watoto walikuwa wanakariri nadharia pekee. Hii inafanya udumavu, lakini sasa hivi mtoto anajua kwamba, nitapimwa kwa kile ninachokijua kwa hiyo, hili ni jambo zuri sana, ninaomba nishukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nishauri katika utekelezaji wa mtaala mpya, *Skills Based Education;* ili mtaala huu ufanikiwe hasa katika amali ni lazima tuwe na karakana za kutosha na vifaa vya kisasa. Ninaweza kushauri tuwe na vituo vya umahiri, *Center of Excellence,* katika mikoa, ambapo hizi zitakuwa ziko *full equipped;* kwamba kila kitu kiko pale kwa hiyo, sehemu nyingine wanaweza kuwa wanajifunza pale. Kila mkoa uwe na shule yake ambayo iko na *facilities* zote na inatoa kozi nyingi. Wilaya nyingine zitakuja kujifunza pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni uhaba wa walimu na wafanyakazi. Sisi Kibiti tuna uhaba sana wa walimu na hii ni kutokana na jiografia yetu kule kwa sababu, mwalimu anapangwa kule, anaenda, ili aondoke kwa hiyo, mimi ninaomba kuwe na mfumo wa kuboresha usambazaji wa walimu, *Teacher Deployment Strategy*. Maeneo haya ya pembezoni sana na vijijini kuwe na motisha, motisha ya *hard to reach allowance,* ili kuweza kuwavutia walimu waweze kukaa maeneo haya hata kama yana mazingira magumu. Lengo ni kuweka uwiano kati ya wanafunzi na walimu, ili kuweza kuboresha elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni kuwekeza zaidi kwenye elimu ya msingi, kama msingi wa elimu yote. Hii ni changamoto kubwa sana, hasa katika maeneo ya vijijini. Kule vijijini, sisi kwetu mtoto anafika

darasa la tatu hajui kusoma wala hajui kuandika. Kwa hiyo, ninaomba Wizara ihakikishe kwamba, shule za msingi zinakuwa na madarasa ya awali na pia, kunakuwa kuna walimu wabobezi. Tujitahidi kuweka picha za kadi na vitabu vya hadithi, lakini pia, watoto wasome kwa njia za kucheza, *learning through play*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kusema hayo ninaomba nirudie tena kuwashukuru sana Wizara. Ninawapongeza sana, ninawatia nguvu na ninaunga hoja mkono kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mussa Mkumba. Nilimwita Mheshimiwa Regina Henry Mikenze na Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi, ajiandae.

**MHE. REGINA H. MIKENZE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi, ili niweze kuchangia katika Wizara muhimu kabisa ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Ninakushukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kazi kubwa ambayo anaifanya katika nchi yetu ya Tanzania na hususani katika suala zima la elimu. Tunamshukuru na tunampongeza sana kwa kazi kubwa ambayo anaifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitaja mambo machache ambayo Rais wetu ameyafanya katika utawala wake, tunamshukuru kwa kuendelea kutoa elimu bila ada. Suala hili ni muhimu sana, tunaweza tukalichukua kawaida, lakini ni suala ambalo limesaidia sana watoto wa Kitanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiwa wa kweli kipindi cha nyuma watoto wengi walishindwa kuendelea na masomo kwa sababu ya kukosa ada, lakini Mama yetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ameendelea kupambana kutafuta fedha, ili watoto wote wa Kitanzania wasome bila bughudha yoyote ya ada. Kwa hiyo, tunamshukuru na tunampongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Mheshimiwa Rais Samia kwa kuboresha mtaala na kuruhusu watoto wa Kitanzania wasome tangu shule ya awali mpaka kidato cha nne bila kikwazo chochote. Watoto wengi, tukiwa wa kweli, waliishia darasa la saba na wazazi waliokuwa na uwezo ndiyo waliwaendeleza watoto wao kuendelea na kidato cha kwanza mpaka cha nne kwa shule za *Private,* lakini kwa sasa kwa hili ambalo Rais amelimaliza katika mtaala huu ulioboreshwa ni suala la kusifiwa na la kupongezwa. Tunampongeza sana na kwa niaba ya wazazi wote wa Kitanzania, ninatumia nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Rais Samia, anafanya kazi njema sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza pia, katika suala zima la kuboresha mtaala. Suala hili siyo rahisi, limehitaji fedha nyingi sana, ujasiri na kujitolea. Kama ambavyo tunatambua unapobadilisha mtaala utabadilisha vitabu kwa hiyo, vitabu vya kufundishia vimebadilishwa kuanzia shule ya awali mpaka kidato cha sita. Tunampongeza sana Mheshimiwa Rais Samia kwa ujasiri, uthubutu na kwa kutokuogopa gharama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna msemo mmoja unasema, kama elimu ni gharama basi jaribu ujinga. Mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ametazama akagundua kwamba, kuongoza Taifa ambalo halina elimu bora ni gharama kubwa kuliko kugharamia leo elimu kwa gharama kubwa, ili upate elimu bora, wananchi walio bora na uongozi wako uwe rahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, katika hili Mama anawekeza hela nyingi sana, anatafuta hela nyingi kwa jasho, ili Tanzania ya kesho iwe njema. Tunaamini kwa kufanya hivi ndipo ile dhima yake ya kuwaachia tabasamu Watanzania itakwenda kutimia. Tunampongeza sana Mama yetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa kuendelea ninapenda kuchangia mambo machache katika kuishauri Wizara yetu hii ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Ninapenda kushauri jambo moja la kwanza kwamba, katika elimu ya vyuo na vyuo vikuu, ninaomba katika kila kozi, somo la biashara liwe la lazima. Kwa nini ninasema hivyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona wanafunzi wengi wanamaliza chuo kikuu na hawawezi kuanzisha biashara yoyote. Ninasema nikiwa na mfano thabiti kabisa, nimeona kule kwangu. Mimi nimefuatwa na mtoto anaomba nimtafutie kazi, amemaliza chuo ana miaka mitano yuko nyumbani, lakini kuna mikopo inatolewa, mikopo ya halmashauri, kijana huyu anasema yeye hayuko tayari kufanya biashara kwa sababu, hakujiandaa *psychologically.* Tangu akiwa darasa la kwanza ameandaliwa kuajiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninashauri suala hili la kuanzisha elimu ya biashara katika kila kozi litasaidia wanafunzi kuweza kuwa na mtazamo chanya kuhusiana na suala zima la biashara. Pia, ninaomba kuishauri Serikali kuhusiana na suala zima la *Startup;* katika hili pia, ninampongeza Mheshimiwa Rais na yeye ameanzisha *Samia Startup Fund*. Hii ni kuwasaidia vijana waweze kupata mikopo waweze kuanzisha biashara ndogondogo na kubwakubwa, lakini pia, ku-*support* teknolojia na maono mbalimbali ya vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninashauri suala hili la *startups* pia, lianziashwe katika vyuo vikuu. Tusisubiri waliomaliza tu ndiyo waanzishe, wapewe pesa, kwa ajili ya ku-*support* maono na *idea* mbalimbali walizonazo. Kwa hiyo, ninaomba sana. Tushirikishe pia, sekta binafsi iweze kusaidia katika ku-*support* maono mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiona wafanyabiashara wakubwa wapo ambao wamefanikiwa katika biashara, nao waweze kupelekwa katika shule, yaandaliwe makongamano waweze kuongea na wanafunzi, kuwa-*motivate*. ili waweze kupata morali kubwa ya kuanzisha biashara. Kwa kufanya hivyo tutasaidia kupata wanafunzi ambao watamaliza vyuo, lakini tayari wana maono ya biashara au tayari wakiwa wameweza kuanzisha biashara zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na ninakushukuru sana kwa kunipatia nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Regina Henry Mikenze.

Nilimtaja Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi. Mheshimiwa Profesa Pius Zebhe Yanda na Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, wajiandae.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi, ili niweze kuchangia hoja ya bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Kwa namna ya pekee ninawapongeza watendaji wa Wizara hii, akiwemo Mheshimiwa Profesa Mkenda na Naibu wake Mheshimiwa Wanu, kazi yao inaonekana. Wameitendea haki Wizara hii kwa kujua kwamba, kweli elimu ni ufunguo wa maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee ninampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Katika kipindi hiki kuna maboresho mengi sana yamefanyika katika Wizara hii, kuanzia kujenga shule shikizi, shule za msingi, sekondari na hata vyuo vikuu kila sehemu, ameweka alama kubwa sana. Tunamshukuru na tunampongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo ni mengi, dakika ulizonipa hazitatosha nikianza kusema katika miaka minne, ambayo Dkt. Samia Suluhu Hassan ameyafanya. Ameongeza shule za msingi kutoka 16,656 Mwaka wa 2020 hadi 19,783, sekondari kutoka 5,000 mwaka 2020 hadi 5,926 mwaka wa 2024 na ongezeko la vyumba vya madarasa, kwa ajili ya walimu na mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu leo ni kuhusu elimu ya lazima. Ninaipongeza Serikali kwa jambo hili, kutekeleza hii Sera ya Mwaka 2014, Toleo la 2023, kufanya elimu ya lazima kwa wanafunzi kuwa miaka 10, waanze shule miaka sita hadi kumaliza shule ya lazima miaka 16 mpaka 17.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema hivyo kwa sababu, kwa kweli, tumewatendea haki watoto wa Tanzania ambao wengi walikuwa wanapoteza kesho yao. Kabla elimu hii haijafikisha miaka hiyo, wakati elimu ya lazima ilipokuwa ni miaka saba, wanafunzi walikuwa

wanamaliza elimu ya lazima wakiwa na miaka 13 na 14. Kwa wale ambao wamechaguliwa kuendelea na sekondari ilikuwa ni ahueni. Kwa wazazi ambao hawakuweza kuendeleza watoto, aidha kwenye shule za ufundi au kuwapeleka *private,* hawa watoto wamekuwa na kesho mbaya kwelikweli na siyo kosa lao, hatukuwatendea haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wengi wamechukuliwa kama wasaidizi wa nyumbani, walioitwa *house girls* na *house boys*. Wamepelekwa mijini, wamenyanyaswa, hawakutendewa haki na hawajawahi kuwa na kesho bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wako wengi wamechukuliwa kama wafanyabiashara, wamebebeshwa masinia ya ndizi, vitumbua na vinginevyo na hawajawahi kuwa na kesho bora. Tena hawa wanaposhindwa, wamefukuzwa bila kurejeshwa kule walikotolewa. Wamekuwa wazururaji mjini, wamezalishwa, tumewaharibu watoto wa Tanzania, ambapo siyo kosa lao. Wengine wameenda kwenye ndoa za utotoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo limekuwa mwarobaini wa kuwasaidia watoto wa Tanzania, watoto wa maskini, watoto wa wakulima kwamba, sasa walelewe, wakuzwe kimwili, angalau wamalize elimu ya msingi wakiwa na miaka 16 – 17. Alelewe kitaaluma na kiroho, ili anavyotoka huko hata akichagua kwenda kuwa msaidizi wa shughuli za ndani, basi aende akiwa na akili zake timamu na kwamba, anaweza kuwa na maamuzi inapotokea changamoto yoyote kwa hiyo, ninaipongeza sana Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema kwamba, kwa kipindi hiki tunajua Januari 2028 kuna wanafunzi zaidi ya milioni tatu 21,177 wanatakiwa kuingia *form one*. Hili linaendana na mabadiliko ya mitaala na kama linaendana na mabadiliko ya mitaala maandalizi ya Serikali yakoje? Isije ikawa tunapitisha tu, maadamu wamemaliza elimu ya lazima na wakawa baadaye hawana msaada?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, kuna umuhimu wa kuwa na vitabu, mwenzangu amesema. *Ratio* ya vitabu inatakiwa kila mwanafunzi awe na kitabu chake. Serikali ijipange ipeleke fedha, ili

hawa watoto sasa wanapofundishwa watoke hapo na elimu bora. Hii mitaala, mwalimu ndiye mpishi mkuu jikoni, kama hatujampika vizuri mwalimu tusitegemee kuwa na wanafunzi bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walimu wenyewe wanasema mitaala ni migumu kwa sababu ya ku-*condense* elimu ya miaka saba katika miaka sita. Ukikutana na mwalimu yeyote, hata ukifuatilia habari za watoto, utaona kwamba, watoto sasa hivi wanafundishwa mambo magumu kwa hiyo, kuna maandalizi makubwa sana yanatakiwa katika kubadilisha huu mtaala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni maandalizi ya vyumba vya madarasa. Wewe unaona kabisa wenzetu wa shule za *private* wanakaa si zaidi ya wanafunzi 40 kwenye darasa moja. Sisi darasa linakuwa na wanafunzi mpaka 100, hebu ona huo ushindani. Ndiyo maana zamani tukishindanishwa shule za *private* na shule za Serikali utaona kwamba, shule za *private* siku zote zilikuwa zinaongoza namba moja mpaka tano, mpaka kumi zilikuwa shule za *private* na *seminary* kwa sababu, mwalimu anaweza ku-*manage* wanafunzi 30 na kitu mpaka 40 kwa hiyo, tuji-*tune*. Kama tunataka kuwapa elimu bora, vyumba vya madarasa vitoke tena kwa *ratio* ya darasa moja linapaswa kuwa na wanafunzi wangapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni la walimu. Iko shule Mwalimu wa *Physics,* Mwalimu wa *Chemistry* na Hesabu ni mmoja, anafundisha *form one* mpaka *form four.* Kwa kweli, tujipange, tuombe Serikali iajiri walimu wa sayansi, ili hawa wanafunzi tunaokwenda kuwapika wakitoka hapo, basi wawe majasiri, waweze kujiajiri waweze kupambana na maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu mwingine ni kuhusu mabweni shuleni, ninaipongeza sana Serikali. Serikali ilipoleta mfumo wa kuwa kila kata iwe na sekondari ilifanya kitu kizuri sana, vinginevyo watoto wa Tanzania wengi wasingesoma. Ninaipongeza na ndiyo maana zaidi ya 90% au 99% ya kata zote sasa hivi zina sekondari za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba tuhame. Kuliko kuendelea kujenga, kuna kata zina sekondari mbili hadi tatu. Sasa hivi tuhamie kwenye kwenda kujenga mabweni katika hizi Shule za Serikali. Ninasema hivyo kwa sababu, maeneo kama ya kwangu Manyara, ukienda Kiteto, ukienda Simanjiro, hata Hanang, bado kuna wanafunzi wanatembea kilomita kumi asubuhi kwenda shule na kilomita zaidi ya kumi kurudi nyumbani. Wanaamka usiku, ukiamka saa kumi, saa kumi na moja, unakutana na wanafunzi na kuna wanyama wakali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine inakuwa adha kwa wazazi kuwasindikiza kwenda shule hiyo asubuhi; wamenyeshewa, wamefanywa nini! Hawa watoto wana utulivu wa kusoma saa ngapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakitoka shule wanakutana na changamoto kibao njiani, wakifika nyumbani hakuna utulivu. Wazazi wengine ni walevi, wakikuta wazazi wanaogombana, wanafunzi hawawezi kuwa na utulivu wa kusoma kwa hiyo, inaathiri sana taaluma ya wanafunzi. Mabweni ni kitu muhimu sana, tujielekeze kwenye kujenga mabweni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wako wazazi wanafunzi wakifika *form four* wanatakiwa wasome mpaka saa nne ile *prep* na wazazi wako pale wanawasubiri, kwa hiyo, inakuwa adha kwa wazazi kuwasubiri wanafunzi, wamalize *prep*, wawachukue wale wanafunzi waende nao. Ninaiomba sana Serikali tukiwahamasisha wazazi vizuri na halmashauri kwa sababu shule ni mali ya jamii, shule ni mali yetu wenyewe. Wazazi wako tayari tuwaongoze tuanze kujenga mabweni kwa kila hosteli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaendana na kitu kinaitwa *exposure*, *exposure* ni uelewa wa wanafunzi. Ninatamani wanafunzi wa Tanzania wapate *exposure,* watoke nje ya kata. Wako wanafunzi wanaanza kusoma shule shikizi kwenye kata hiyo, shule ya msingi kwenye kata hiyo, sekondari kwenye kata hiyo, hawa watoto wanapata *exposure* lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, zamani watoto walikuwa wakizaliwa tulikuwa tunaandaa kama *manpower*, unajua mtoto akikua ni wa kuchunga ng'ombe na kwenda kulima, siyo dunia ya leo! Dunia ya leo inahitaji mapambano kweli kweli. Watoto wetu lazima tuwape *exposure* na ni elimu muhimu kuliko elimu ya kukaa darasani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana watoto wana simulizi mbaya toka zamani kwamba ukienda sehemu fulani makabila yana tabia hiyo, wanakula hivyo, bwana mtoto akimaliza chuo hata akipata *posting* kwa mfano, mtoto wa Arusha au Manyara ukampeleka Sumbawanga, Katavi kule, huwa ni msiba mwingine kwake, siyo kwake tu hata kwa mzazi, analia kwa sababu hataki kwenda kule mbali, hajawahi kusikia, hajawahi kuona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu sasa hivi sasa tujielekeze kwa sababu shule zote zitakuwa za bweni, watoto wa mkoa mwingine waende kwenye mkoa mwingine wakajifunze utamaduni wapate *exposure* ili siku moja nje ya maeneo wanayotoka wapambane na maisha, wapambane na ajira, wapambane na kazi ndani ya Tanzania, nje ya Tanzania, nje ya Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu liingine ni kuhusu chakula shuleni. Chakula shuleni wenzangu wameongea sana, chakula ni jambo muhimu sana, hili linawezekana tukiwa na utaratibu mzuri na wazazi. Ninashauri kipindi hiki tunapoenda kwenye mavuno, kama mwanafunzi mmoja anatakiwa kuwa na debe nne za mahindi, debe moja ya maharage, ndiyo kipindi cha kukusanya mazao haya yapelekwe shuleni, lakini utunzaji kule shuleni ni changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatamani Wizara ya Afya sasa itupe kama ni *design* wanavyojenga shule, ina jengo la utawala, ina bweni, ina maabara, ina nini. Sasa hivi iwe sehemu ya kuwa na stoo ya kuhifadhi vyakula vya wanafunzi vikae mwaka mzima ili wazazi wasisumbuliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukimwambia mzazi Januari apeleke debe nne za mahindi, apeleke na maharage, amebakiza maharage ya mbegu tu, hana pale nyumbani, ni kilimo…*(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Tunaendelea na Mheshimiwa Profesa Pius Zebhe Yanda, Mheshimiwa Subiri Mwaifunga ajiandae.

**MHE. PIUS Z. YANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia majadiliano yanayoendelea sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote ninaomba kuanza kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda na Mheshimiwa Wanu kwa kazi kubwa ambayo wamefanya. Hakika wamefanya mageuzi makubwa sana kwenye sekta hii, hiyo yaani iko wazi kabisa. Mfano mzuri tu ambao ningependa kuutoa ni kwamba, kwa upande wa watafiti vyuo vikuu na vyuo vingine ambavyo vinafanya utafiti, ameweza kuanzisha tuzo ya wale watafiti ambao ni bora kabisa na kwa kutumia vigezo vya kimataifa na hasa wale ambao wanakuwa wamewasilisha au wame-*publish* maandiko yao kwenye makala za kimataifa za hali ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale wanapewa tuzo na hiyo imekuwa ni motisha kubwa sana katika upande wa vyuo vikuu. Jambo moja tu ambalo ningeweza kuomba ni kwamba, sasa kuna haja basi Wizara ifikirie kuweka pesa za kutosha kwa ajili ya utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka mingi iliyopita tumekuwa tunapata *support* ya Serikali kwenye vyuo vyetu kuwezesha utafiti na hilo zoezi linaendelea na miaka ya hivi karibuni kulikuwa na *location* zaidi, lakini sasa wakati ule tulikuwa pia tunapata *support* kutoka kwa wenzetu *development partners*, ninafikiri sote tunajua kwamba mambo yanazidi kubadilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ili tuendelee kuwa kwenye *pace* kama vyuo vikuu kama vyuo vikuu vingine, inabidi tuwe na mkakati wa ziada wa kuhakikisha kwamba tunapata fedha za kutosha ili vyuo vyetu viweze kuendelea kufanya utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo moja ambalo linaweza pia lika-*compromise* hizi juhudi za utafiti, ni *teaching workload*. Ukweli ni kwamba Wahadhiri wana kazi kubwa ya kufundisha na inaweza pia ikaathiri kupata muda wa kuweza kufanya utafiti, sababu kubwa ni kwamba *of course* muda unavyozidi kwenda Wahadhiri wana-*retire* hasa *Professors*, lakini sasa pamoja na hivyo, tumeona na tunamshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amekuwa anawekeza hela za kutosha kwa ajili ya kuajiri walimu wapya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tujue kwamba hawa inabidi wakue kwenye *process* ili waweze kufika kwenye kada za kuweza hata kufundisha au kusimamia wanafunzi wa *Masters and PhD*. Sasa kulingana na vigezo na miongozo ya *TCU*, kwa vyovyote vile lazima kuwe na mchanganyiko kati ya *juniors* na *seniors*. Sasa inapofika mahali ambapo *seniors* wanapungua kwa sababu ya ku-*retire*, hiyo inaleta changamoto sana kwenye vyuo vingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda hadi muda tumeona pia udahili umekuwa ni mkubwa kwenye ngazi ya *degree* ya kwanza, ya pili, ya tatu. Kwa hiyo Walimu au *Professors* wanabeba mzigo mkubwa wa *supervision,* lakini pia na kufundisha darasani. Sasa hiyo inaweza ika-*compromise research* kwa sababu tunahitaji pia tuendelee kuchangia kwenye mambo ya utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukumbuke pia kwamba sisi vyuo vyetu vina wajibu wa kufanya utafiti, kufundisha lakini pia tunaita kuchangia katika maendeleo ya jamii. Maendeleo ya jamii ni kwamba pamoja na kwamba tunafanya tafiti, tunahitaji zile tafiti ziwezi kuchangia katika michakato ya maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niwape mfano mzuri ambao kwa kweli ninasema ni *best practice* na ninaomba ku-*declare interest* kwanza kwamba mimi nimeshiriki katika kuandaa Dira ya 2050. Mheshimiwa Profesa Mkumbo alichokifanya ninafikiri ni mfano wa kuigwa, aliteua wataalamu *on merit* katika makundi matatu, kundi moja likuwa ni kundi la wataalam ambao wanafanya *synthesis* ya zile tafiti zote ambazo zimefanyika iwe zimefanywa na Watanzania au nje ya Tanzania, lakini kulikuwa na kundi la uandishi, kulikuwa na kundi

lingine la wale ambao watakuja ku-*review* lile andiko, kwa hiyo, sasa wale walikuwa wanafanya *synthesis* walikuwa wanaangalia *on thematic based*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ni mambo ya afya, kunakuwa na wataalam kwenye masuala ya afya, mazingira na hivyo hivyo. Wanachambua, wanachakata zile taarifa, zikiiva vizuri ndiyo wanawapatia waandishi. Sasa pendekezo langu ninalotoa ni hivi, kwamba hatuwezi kuwa tunafanya hivyo kulingana na mahitaji ya wakati. Tungeweza kuchukua *model* ambayo nchi nyingine zinatumia kwa mfano, nchi za Ulaya, Marekani na kwingine hata Afrika. Kwa mfano, *South Africa*, *Egypt* na Ethiopia, Kenya na Rwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wao wanafanya kitu wanaita *synthesis report*. Wanateua wataalam, wanachakata zile taarifa na pendekezo langu kwa upande wa Tanzania, tungeweza tukafanya kila baada ya miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni nini? Ni kwamba tunapofikia sasa tunaingia kwenye awamu ya miaka mingine mitano, tunajua kwamba ndani ya hii miaka minne kuna *generation* ya *information*. Sasa wataalam wakae chini waweze ku-*update* zile *report then* tutakuwa na taarifa ambazo zitaweza ku-*inform* mchakato wa kuandaa miaka mingine mitano ya maendeleo ijayo kwa sababu kutakuwa na *new knowledge* ambazo zinakuwa zimekuwa *generated*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiwa hivyo maana yake sasa zile *documents* zinakuwa ni *reference documents* kwa kila sekta kulingana na mahitaji, badala ya kila wakati tunahitaji kutengeneza sera, tuna-*commission* watu wanafanya *synthesis,* lakini tutakuwa na *consolidated documents* ambazo zinaweza zikasaidia kwenye ku-*inform policy, actions* na *practice*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningeomba kulizungumzia pia ni suala la *VETA*. Ninakumbuka Waheshimiwa wengi wamezungumzia kuhusu *VETA*, nami ninaomba kusisitiza pia kwamba pamoja na kwamba wanaweza wakawa na mitaala ambayo ni

*standardized*, lakini pia tufikirie ni jinsi gani wanaweza wakaweza kuhitaji au ku-*solve* au kuweza kusaidia jamii husika kulingana na mazingira husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kama ni maeneo ambayo kuna wakulima wanalima mazao ya matunda na kila kitu, vijana wafundishwe jinsi ya kuchakata yale matunda kwa kutumia *technology* ambayo tayari tunayo. Sasa hiyo itaweza kusaidia jamii inayozunguka ile *VETA* kwa urahisi zaidi na kwa *arrangement* ya namna hiyo, inaweza ikafanywa kwa kushirikiana na kwa mfano na *SIDO*, taasisi kama hizo na wananchi wataweza kuweza ku-*appreciate* kwa ule mchango ambao *VETA* inachangia.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa, muda wako umemalizika. Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza kabisa ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya na uzima, nimesimama hapa kuchangia hoja hii ya Bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Ninapenda kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa ambayo anaifanya katika sekta hii ya elimu. Mimi binafsi nimekuwa kipindi cha tatu sasa kwenye Bunge hili, nimekuwa shahidi wa ambayo yamefanyika katika Sekta hii ya Elimu nchini kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Waziri, Kaka yangu Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda kwa kazi kubwa ambayo anaifanya, sina mashaka naye. Amekuwa Katibu Mkuu Wizara ya Viwanda na Biashara, tumefanya pamoja, niliona jinsi alivyokuwa anafanya. Pia amekuwa Katibu Mkuu Wizara ya Maliasili na Utalii amefanya vizuri zaidi, leo amekuwa Waziri wa Elimu kwa kweli anafanya vizuri kwelikweli. Ninampongeza kwa dhati ya moyo wangu kwa sababu ninajua ambacho anakifanya kiko kinatoka moyoni mwako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana pia Mheshimiwa Naibu Waziri ndugu yangu, pacha wangu Wanu kwa kazi kubwa ambayo aafanya. Nimekuwa nikimwona na nikimfuatilia mara kwa mara kwenye maeneo mbalimbali amekuwa akitembelea kuangalia sekta ya elimu na changamoto zake. Kwa kweli amekuwa akitoa majibu ya yale ambayo yamekuwa yakitukabili. Ninaomba kuwakaribisha sana kwenye Jimbo langu la Tabora, zipo changamoto, lakini wafahamu Tabora ni kitovu cha elimu katika nchi yetu, wanafahamu hata Baba wa Taifa amesoma Tabora, viongozi wengi mbalimbali katika nchi hii wamesoma Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo zipo changamoto ambazo zinatukabili ninaomba waje wazione lakini tusaidiane kuzitatua ili kuhakikisha Tabora inaendelea kuwa kitovu cha elimu kama ilivyokuwa huko miaka ya nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizi ninasema tu kwanza Jimbo la Tabora Mjini pamoja na kwamba zamani ndiyo ilikuwa inasikika sana kwa kutoa elimu bora na elimu nzuri kwenye shule zake mbalimbali, lakini pia tunavyo vyuo mbalimbali katika Mkoa wetu wa Tabora na hususan viko pale kwenye Jimbo letu la Tabora Mjini. Ninaomba kumwambia Mheshimiwa Waziri kwamba sisi pale tuna Chuo cha Ualimu Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Walimu wengi walioko humu ndani wamepita kwenye Chuo kile cha *TTC* Tabora, chuo hiki kilikuwa kinatoa elimu maalum. Sasa ninamwambia Mheshimiwa Waziri kwamba, elimu hii maalum waliiondoa, tafadhali sana wajaribu kuangalia uwezekano wa kuweza kurudisha elimu maalum katika Chuo cha Ualimu kilichopo Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu baada ya kuondoa elimu hii maalum, wakaacha pale majengo yako yenyewe, wale walimu waliokuwa wanafundisha kutoa hiyo elimu maalum wakawapeleka maeneo mengine. Chuo kimeendelea kuwa *dormant* kwa sababu kinategemea Walimu watakaoletwa kuja kuwa Walimu wa baadaye, matokeo yake walipozuia mwaka mmoja pale chuoni kwamba watu wasipelekwe tena kusomea ualimu, chuo kile kikawa hakuna

chochote ambacho kinaendelea, hivyo kupelekea sasa chuo kuwa na majengo na madarasa ambayo ni chakavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana kwa Serikali yangu hii ya Awamu ya Sita, Serikali sikivu, sasa tuelekeze nguvu kubwa kwenye vyuo hivi na hususan vyuo hivi vya zamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Elimu cha Ualimu Tabora kwa kweli majengo yake yamechakaa, lakini ni majengo mazuri ya muda mrefu ila yamefika mahali Mheshimiwa Waziri yanavuja hata kwenye madarasa ambayo wanafunzi wanapata elimu. Ukiangalia hata mabwalo hayana ile hadhi ya Chuo cha Ualimu cha *TTC* yaliyokuwepo zamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba sana Mheshimiwa Profesa Mkenda, ninajua yeye pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri wake lakini na Katibu Mkuu wako vizuri na wamekuwa wasikivu, waiangalie Tabora kwenye *angle* hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilizungumza hapa kuhusiana na zile shule za zamani *Tabora Boys, Tabora Girls*, Mirambo, wamekwenda kuzifanyia ukarabati leo ukifika *Tabora Boys* unasema kweli hii shule Mwalimu Nyerere alisoma kwa sababu majengo yamekarabatiwa, na yanakwenda vizuri na sasa hivi ukifika pale geti kubwa ukiingia unaona kabisa kwamba hii ndiyo *Tabora Boys*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba sana, wafanye hivyo pia kwenye hiki Chuo cha Ualimu sababu ni chuo cha muda mrefu, kimesomesha watu wengi lakini pia kina maeneo makubwa sana. Kama wanataka kuweka elimu ama masomo mengine yoyote tafadhalini, kwa sababu pale kuna maeneo mpaka wanaingia wale Nguchiro wanaingia yaani kwa sababu ni maeneo ambayo hayana kazi. Hebu waende pale wakaweke majengo angalau wawe na chuo kingine ndani ya Chuo cha Ualimu kwa sababu ninaamini kabisa watu wanahitaji elimu na watafika kusoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza na kuishukuru Serikali kwa ujenzi wa Chuo Kikuu pale Tabora maeneo ya Manoleo iko Tabora Mjini. Kwa kweli ujenzi unaenda kwa kasi na ninaendelea kuipongeza Serikali yangu kwa kusikia kilio cha watu wa Tabora, kwamba tulikuwa tunahitaji Chuo Kikuu cha Serikali. Leo ninavyozungumza, chuo kile kinajengwa kwa kasi ya hali ya juu. Ni imani yangu Waziri atasema jambo atakapokuja kuhitimisha hapa kuhusiana na chuo hicho, lini kitakuwa tayari na lini watoto wataanza kusoma pale ili Mkoa wetu na Jimbo letu la Tabora kwa ujumla liweze kupata uchangamfu wa watoto watakaokuwepo pale wanakuja kusoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunacho Chuo cha Utumishi wa Umma pale Tabora, chuo cha Uhazili. Masekretari wengi waliopita pale wanakifahamu chuo hiki, wakati ninakua chuo hiki kipo. Pale kwenye kile chuo kuna majengo mengi, lakini majengo mengi unakuta ni *white elephant* kwa sababu si watoto wengi sasa hivi wanakwenda kusoma *secretarial*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wizara iangalie, ninajua Waziri ana wataalam wengi na una vichwa vizuri sana. Waangalie waone namna gani ambavyo wanaweza kuleta kozi nyingine mbalimbali kwenye kwenye chuo kile na isiwe ni *secretarial* pamoja na mambo ya *Records* pekee yake, kuwe na mambo mengine ambayo yanaweza yakafundishwa pale na kile chuo kikawa na tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wao pia wana changamoto zao ikiwepo uchakavu wa hosteli, majengo yao yana hali mbaya, lakini wamekuwa na upungufu pia kwenye masuala ya kompyuta wanazotumia zaidi kwa ajili ya kufundishia, lakini pia madarasa yanatakiwa yafanyiwe ukarabati na hususan kuwawekea viti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanatamani kuona wanawekewa viti vile vya kuunganisha vya kung'ang'ania hapohapo, kwa sababu hivi viti vya kutoa na kurudisha imekuwa ni changamoto kwao kiasi kwamba wanaweza wakaleta kesho wakakuta kiti hakipo, lakini vikiwepo viti vya hapohapo itasaidia vile viti kuwepo kwa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafahamu Mheshimiwa Rais amefanya kazi kubwa sana kuhusiana na suala zima la Vyuo vya *VETA,* mimi hapa ninatoka Tabora Mjini. Katika Tabora Mjini, binafsi tunacho Chuo cha *VETA* cha Mkoa, lakini kinatumika zaidi na wanafunzi wanaotoka pale kwenye Jimbo la Tabora Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutuletea walimu kutoka Indonesia kwa ajili ya kufundisha wanafunzi pale, utengenezaji wa vikoi bora ambavyo vinaleta ushindani kwenye soko la ndani pamoja na soko la nje. Kikubwa ninachowaomba, tusaidieni pale kwenye Chuo cha *VETA* tunahitaji magari ya kufundishia wanafunzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanakodisha magari kwa ajili ya kufundishia wanafunzi, mengine nimeleta kwa maandishi ninaomba watusaidie walau wapate gari moja ama mawili ili wanafunzi wanaojiandikisha kwenye suala la udereva wawe na magari badala ya kusubiri kukodisha, hii ni kadhia kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho lakini siyo kwa umuhimu, pale Tabora tunayo Shule ya Sekondari ya Kazima. Hii shule ya Sekondari ya kazima ina wanafunzi mchanganyiko wakiwepo wanafunzi wenye mahitaji maalum. Ninaomba sana Mheshimiwa Waziri, atakapokuja Tabora afike pale ajionee hali halisi. Pale wanafunzi wenye mahitaji maalum wana changamoto kwa sababu bajeti inayopelekwa pale ni ile ile ambayo imekuwa ikitolewa hata kwenye shule nyingine zenye wanafunzi wa kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefika pale na nimeshuhudia, nimekuta wanafunzi wenye mahitaji maalum. Wapo wanafunzi hawawezi kuamka asubuhi kwenda darasani mpaka wapate kitu cha moto tumboni, lakini ukiangalia bajeti haimtoshelezi kuweza kumfanyia yule ili aweze kwenda darasani. Inawalazimu walimu wachukue hatua za ziada ili waweze kuwasaidia wanafunzi hao waweze kuingia madarasani. Kwa kweli, jambo hili ni gumu, jambo hili ni zito, tunawapa wakati mgumu sana walimu wetu kufanya mambo ambayo kidogo yanakuwa magumu kwenye maisha yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninaiomba sana Serikali iangalie hii Shule ya Kazima iongeze bajeti kwa ajili ya wanafunzi hawa wenye mahitaji maalum ili wanafunzi hawa na wao waweze kupata elimu kama ambavyo wanafunzi wa kawaida wanapatiwa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona umeshawasha kisemeo, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi, lakini kwa sababu ya muda mengine nimeyaandika na nitawapatia Wizara waweze kuyafanyia kazi. Ninakushukuru sana. *(makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga mchangiaji wetu wa mwisho mchana huu.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nitawataja wachangiaji ambao wataanza siku ya leo jioni. Tutaanza na Mheshimiwa Mohammed Musa Utaly, Mheshimiwa Boniface Mwita Getere, Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako na Mheshimiwa Juma Abdallah Juma. Hao ndiyo wachangiaji wataanza jioni ya leo

Waheshimiwa Wabunge, tuna matangazo kidogo. Kwanza Waheshimiwa Wabunge, ninaomba tukumbushane kuhusiana na suala la mavazi Kanuni ya 173(1) inamtaka Mheshimiwa Mbunge aje na mavazi au avae mavazi nadhifu yenye kuhifadhi heshima yake, hadhi ya Bunge na utamaduni wa nchi. Kwa hiyo, ili tuweze kwenda vizuri, turudi kwenye Kanuni ya 173(4)(a) kwa wanawake na Kanuni ya 173(4)(b) kwa wanaume. Hii itatusaidia kuepusha kuzuiliwa kuingia katika Vikao vya Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, vikao vya Bunge siyo humu ndani tu, lakini popote pale kwenye Kamati na hata sehemu nyingine yoyote ambayo shughuli ya Bunge inafanyika. Kwa hiyo, tunaomba sana tuzingatie kanuni tuvae mavazi ya heshima ili tulinde heshima yetu sisi wenyewe. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maelezo hayo, tuna tangazo la wageni ambao wapo muda huu.

Wageni 56 wa Mheshimiwa Muhsin Haji Ussi ambao hao wanatoka Taasisi ya *Empowerment Bridge Initiative* kutoka jijini Dodoma. Karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Wageni wengine ni wageni 13 wa Mheshimiwa Ussi, wanafunzi kutoka *Hope for Students Tanzania*, karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Wageni wengine ambao wametembelea kwa ajili ya mafunzo. Kuna wanafunzi 90 na wakufunzi watano wa Chuo cha *Tabora Polytechnic* kutoka Mkoani Tabora, karibuni sana wanafunzi wetu kutoka huko Tabora.

Tunao pia vijana 50 wanaosoma Sayansi ya Siasa na Utawala wa Umma kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma *(UDOM)*. Karibuni sana wanafunzi wetu. Karibuni sana wageni wetu wote katika Bunge letu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, ninawatakia kila la kheri na tutakutana Saa 11.00 jioni kwa ajili ya kurudia Bunge.

*(Saa 7.02 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

*Mwenyekiti (Mhe. Deodatus P. Mwanyika) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea na majadiliano; kwa hiyo niwaite sasa; Mheshimiwa Mohamed Mussa Utaly atafuatiwa na Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere na Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako ajiandae.

**MHE. MOHAMED M. UTALY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nishukuru kwa nafasi hii ya kuchangia katika bajeti hii ya Wizara ya Elimu. Niungane na wenzangu kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa fursa hii adhimu na afya njema inayotuwezesha kukaa katika Bunge hili na kuweza kuchangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumpongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna anavyoweza kuinua suala la elimu katika nchi yetu. Waheshimiwa Wabunge wote waliopita kuzungumza hapa, wamezungumza na kuonyesha ni namna gani miundombinu imejengwa kila mahali. Hili ni jambo ambalo ni maono ya Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nitoe pongezi za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Profesa Adolf Mkenda. Pongezi zingine ni kwa Mheshimiwa Wanu Ameir kwa namna ambavyo wanafanya kazi nzuri katika Wizara hii. Ninapenda pia nimpongeze Katibu Mkuu wa Wizara, Profesa Carolyne Nombo, ambaye ni Mtendaji mzuri sana na ni mtu ambaye anashirikisha watu wake katika utendaji kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa nilete shukrani za dhati kutoka kwa wananchi wa Jimbo la Lindi Mjini kwa kitendo cha

Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuwajengea Chuo Kikuu cha Dar es Salaam Kampasi ya Ngongo. Chuo kikuu hiki ndicho chuo kikuu cha kwanza katika Jimbo la Lindi; na kwetu chuo hiki ni kuongeza fursa ya Elimu ya Juu katika Jimbo letu. Pia kwetu sisi chuo hiki ni kichocheo muhimu sana cha uchumi wa Mji wa Lindi. Vilevile, chuo hiki tunakitazama kama njia ya kuongeza ajira rasmi na ajira zisizokuwa rasmi kwa wananchi wa Lindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kujenga chuo hiki mwanzoni sisi Lindi tulitoa ekari 100 kwa ajili ya ujenzi wa chuo hiki, lakini baadaye tukaombwa kuongeza eneo kwa ajili ya chuo hiki; tukaongeza ekari 332 na kufanya jumla ya eneo ambalo litajengwa chuo hiki kuwa ekari 432. Katika kuongeza chuo hiki tulilazimika kuchukua eneo ambalo imejengwa Shule ya Sekondari ya Ngongo. Kwa hiyo shule hii inatakiwa iondoke katika eneo la chuo kikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, alipokuja Mheshimiwa Waziri Mkuu Lindi ili kuweka jiwe la msingi la chuo hiki tulimwba Wizara iweze kuijenga shule hii ya sekondari. Kwa sababu tunayo maagizo kwamba inapofika mwezi Septemba shule hii inatakiwa iwe imeondoka; sasa hapa tunalo jambo mbuzi wa Bwana Kheri amekula shamba la Bwana Kheri. Bado shule hii inahusiana na Wizara ya Elimu, na chuo hiki kinahusiana na Wizara ya Elimu. Kwa hiyo tunamwomba Mheshimiwa Waziri, kwa kuzingatia agizo lile alilolitoa Mheshimiwa Waziri Mkuu tupatiwe fedha ili majengo ya Shule hii ya Sekondari ya Ngongo yaweze kujengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba pia nizungumzie kuhusiana na suala la ujenzi wa chuo kitakachotoa elimu ya ufundi wa gesi na mafuta Lindi. Kwa kuwa sasa hivi tuko katika maandalizi, baada ya majadiliano maana yake tutasainia na mkataba juu ya *LNG*. Tuliahidiwa kwamba Arusha *Technical* itajengwa pale Lindi. Chuo hiki kusudio lake ni kuwawezesha vijana wetu kupata mafunzo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kwa upande wetu kama Halmashauri tumetekeleza majukumu yetu tumetoa eneo la takribani hekta 236,000 tangu mwaka 2004, lakini tunachokiona sasa hivi katika eneo lile ni bango tu limeandikwa Arusha *coming soon*. Sasa sijui

kama toka 2004 mpaka leo bango hili lina uhalali wa kusema Arusha *technical coming soon*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliambiwa kwamba zipo fedha ambazo zitapatikana kama *CSR* kutoka katika Mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere na kwetu tuliambiwa kwamba zitapatikana shilingi 67,000,000,000. Ningeomba kama fedha hizo zimepatikana au kama hazijapatikana basi juhudi ifanyike ili chuo hiki kiweze kujengwa ili vijana waweze kupata mafunzo tuweze kuwa na watu ambao watashiriki katika *LNG* wakiwa na taaluma inayohusiana na masuala ya gesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa sasa nizungumzie suala la ikama ya walimu. Ninajua kwamba baadhi ya mambo hapa yatahusiana na TAMISEMI, lakini Mheshimiwa Waziri wa Elimu ndiye Mnyamwezi ambaye tunaye hapa sasa hivi; kwa hiyo sisi tutambebesha tu mzigo kwa sababu suala lenyewe linalozungumzwa ni suala la elimu na yeye ndiye baba wa elimu katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika siku zake 100 miongoni mwa walimu walioajiriwa na sisi Lindi tumepata Walimu 75 wa Sayansi. Hata hivyo, ule mpango wa kuwabadilisha walimu wa *diploma* kutoka kufundisha sekondari na kwenda kufundisha shule ya msingi imetuletea pengo kubwa la walimu wa *arts,* walimu wa masomo ya sanaa. Sasa hivi Lindi tuna uhaba wa walimu 100 wa sanaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningemwomba Mheshimiwa Waziri kwa namna yoyote ilivyokuwepo, yeye ni Profesa na mwenzake ni Profesa. Maprofesa wao wanavyokaa lugha zao wanaelewana; wazungumze, watupatie walimu hawa 100 ili tuweze kufanikisha suala la utoaji wa elimu katika Jimbo la Lindi Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo madai ya walimu wetu, madai ya likizo, madai ya uhamisho, fedha za kujikimu za ajira mpya 2024/2025 na fedha za kujikimu za ajira mpya 2025/2026. Hili jambo la walimu wapya kuletwa mahali halafu wakawa hawana fedha za kujikimu ni jambo ambalo linawachanganya sana walimu wetu.

Kwanza anakuja katika mazingira mapya tofauti na mazingira aliyoyazoea. Anakuja pale hana uwezo wowote hana mjomba wala shangazi, anachotegemea ni ajira yake na pesa ya kwanza ambayo angepewa ingemsaidia ni fedha ya kujikimu. Ninaomba walimu hawa wapewe fedha hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kunakuwa na tatizo katika miji yetu walimu wakifika wakiona hali ni ngumu na fedha za kujikimu hawajapewa wanaondoka; jambo ambalo sisi tusingependa tukose walimu kwa sababu sisi Lindi tumejipanga katika jambo la kuhakikisha kwamba vijana wetu wanapata elimu inayotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haya machache, ninaunga mkono hoja. Ahsanteni sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako. Nilimwita Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere na Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili nichangie Wizara ya Elimu. Kwanza ninawapongeza viongozi wote wa Wizara, tukianza na Waziri Profesa Mkenda, anajulikana kwamba ni mtendaji kazi na mzalendo, Mtanzania mzalendo. Naibu wake anafanya kazi vizuri mimi nimekuwa naye vipindi vitatu sasa. Sifa yake kubwa ni kwamba ni mwepesi wa kufikika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kumwona Wanu wala huwazi kwamba unamwona mtoto labda wa mkubwa au wa mfalme, yeye anafikika mapema sana na hana tatizo. Waziri wake pia hana tatizo. Profesa Carolyne ni mtendaji kazi mkuu; Katibu wao ni mzuri sana kwenye kazi za utendaji, anafanya kazi vizuri, na watendaji wote wa Wizara tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Mheshimiwa Rais. Mimi kitu pekee ambacho ninataka kumwambia Mheshimiwa Rais ni kwamba tumwombee aendelee na msimamo wake wa kulilinda Taifa letu. Taifa lolote duniani linatakiwa kulindwa. Elimu tunayoipata isiwe

elimu ya kubomoa dunia. Kwa hiyo tunamwomba, Rais ni *system,* aendelee na *system* yake ya kulilinda Taifa letu, tuendelee kupata elimu kwa utulivu tulinde amani yetu. Ninamshukuru Rais kwa sababu pia ametuletea Chuo Kikuu cha Butiama na ametupa fedha nyingi ya kujenga shule za amali, ikiwe Shuye ya Amali ya Manchimweru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina la kusema juu ya Mheshimiwa Profesa. Wananchi wa Jimbo la Bunda walivyolia sana juu ya *VETA* akawapa Shule ya Amali ya Manchimweru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu kubwa hapa ni kwamba ile shule imejengwa na imejengwa imekamilika, lakini baada ya awamu ya pili, awamu ya tatu haina majengo ya karakana na wala haina vifaa vya ufundi. Ni juu ya Profesa kwenda kumalizia ile shule ambayo kila mara nimekwenda ofisini kwake kuona namna ya kunisaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona pia kwenye Ibara ya 56 kwenye Hotuba yake, anasema uwezeshaji wa shule za msingi na sekondari. Ninaomba sana; Shule ya Msingi ya Mariwanda, Shule ya Msingi ya Manchimweru A, Shule ya Msingi ya Mikomariro A na B, Shule ya Msingi ya Rakana na Shule ya Msingi ya Mihingo zina hali mbaya sana, majengo ni chakavu. Ninaomba katika ule uwezeshaji wake wa Ibara ya 56 anisaidie kupata kurekebisha hizo shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna uwezeshaji vilevile wa shule za sekondari; nina shule mbili mbovu mbovu mbovu kupita kiasi; Shule ya Sekondari ya Sanzate na Shule ya Sekondari ya Tingirima. Ninaomba tafadhali sana anisaidie kwenye hizo shule ili tuweze kufikia malengo ya kupata wanafunzi bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 76 amezungumzia kuhusu ubora wa elimu. Hapa niongee na hapa niwe mkweli. Hivi kweli kwa hali tuliyonayo nikilinganisha na hii ambayo imesema *Samia Scholarship;* na *Samia Scholarship* nimeiona mara mbili, ipo ya wanafunzi 1,051 na kuna Samia *Scholarship Extended* ambayo ina wanafunzi 50. Nilikuwa ninatazama, hivi ni kweli hao wote

wanaofadhiliwa hawa na Samia *Scholarship* ya 1,050 ni *Extended* wote ni Wanafunzi wa Tanzania; wote ni wa Tanzania; lakini, kama hatuna mfumo mwingine wa kawaida tutampataje mwanafunzi anayetoka Shule ya Nyamang'uta kwenye Jimbo langu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nenda angalia, shule bora 20 za Tanzania utakuta Kemebos, huku kwetu kubwa utakuta Tabora *Boys,* utakuja Ilboru; lakini shule nyingine zote ni Mariwanda na shule zote za *private*. Wanafunzi wenye *GPA* kubwa wote wanatoka kwenye za *private;* na shule ambazo zinasoma kwenye viwango vikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano *Kemebos*, wanafunzi wanamaliza *form six* ni 30 tu na wote wana A, wana *GPA* kubwa. Je, kama hii Samia *Scholarship* hatuwezi kufanya upendeleo wa kwenda kupata watu kwenye kanda, hata kama ana *GPA* kubwa hailingani tutampataje mwanafunzi wa Nyamang'uta? Nimwombe Profesa tutafute namna. *GPA* ni *GPA* tu, lakini mtu anaweza kuipata kwa mazingira yapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tuone ni namna gani ya kuwasaidia wanafunzi ambao wana jitihada. Tutenge, kama wako 1,050 chukua watu hata 100 tuseme hapa tutawatoa kwenye mikoa mbalimbali kutokana na *GPA* waliyokaribia, hata wale wanaokwenda nje wale tuangalie ni wapi ambao wamekaribia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu vinginevyo na kama tunavyojua, kwamba hizo shule kubwa zinazolipa fedha nyingi zinakwenda kwenye watu wenye uwezo. Kwa hiyo tukiwapa tena kwenda nje tunapeleka palepale. Itakuwa sawasawa na kusema kwamba maji yanayoenda ziwani. Kwa hiyo nimwombe Profesa kwenye hili jambo alizingatie vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili wao wanatoa sera, wanatoa na mitaala. Tushirikiane na TAMISEMI tuangale hali zetu za shule. Hivi kweli twende huko ndani tukute shule moja haina dawati na shule moja haina viti vya kukalia. Watanzania ni wale wale wa kwetu, ni wale wale; sisi tujitahidi tuone. Huwa ninanaangalia kwenye tozo za

barabara kuna fedha imetengwa, kwenye umeme kuna fedha inatozwa; kwa nini sasa tusitafute namna ya yoyote ya kupata chanzo chochote cha shuleni ambacho tutatoza kwa ajili ya kufanya vitu vidogo vidogo hivi, uchimbaji wa choo lakini pia kwenye madawati na nini tusiwepo ili watoto wetu wasome kwa namna ambayo tunaweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kipimo cha ubora wa shule kinategemea watakaposhughulikia. Wakati fulani huwa ninajiuliza sana; Serikali inatumia nguvu sana kuifanya siku ya mitihani iwe siku maalum. Magari makubwa, ulinzi, polisi nini, wanaenda kupima mtihani ule ufanyike, lakini, ni nguvu gani imetumika sasa kuweka uwiano wa mafundisho kwenye maeneo hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninafikiri kwamba tusipoji-*attack* sisi wote tunabadilika, Mwalimu alisema tusiahirishe. Niseme tu ukweli, haitokei na haitatokea, kwamba amekuja Rais mwingine, sijui atakuwa bora, atamaliza kila kitu. Maendeleo ni kila siku yapo, kila Rais akija atakutana na matatizo yaleyale yatakuwepo. Leo Marekani, tunazunguza Marekani lakini hali ni hivyo hivyo. Kwa hiyo nimwombe sana Mheshimiwa Profesa; Shule ya Amali ya Manchimweru anisaidie na hizo shule ambazo nimetaja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru sana watendaji wote wa Wizara, wanafanya kazi vizuri sana. Ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwita Boniphace Getere. Nilimwita Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako na Mheshimiwa Juma Abdalla Juma ajiandae.

**MHE. PROF. JOYCE L. NDALICHAKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Ninaomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema. Kipekee niwashukuru sana wananchi wa Kasulu Mjini kwa imani yao kubwa kwangu na kwa ushirikiano ambao wanaendelea kunipatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukrani hizo ninaomba nitoe pongezi za dhati kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uongozi wake mahiri uliotukuka, lakini kubwa zaidi kwa muktadha wa hoja iliyoko mbele yetu kwa uthubutu wake wa kuweza kufanya mageuzi makubwa katika sekta ya elimu. Ninampongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia nimpongeze kaka yangu, Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda kwa kazi kubwa ambaye kwa kweli amebeba maono ya Mheshimiwa Rais na kuyasimamia, kuyatafsiri, kuweza kufanya maboresho ya sera ya elimu pamoja na mitaala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana dada yangu Wanu Ameir Hafidh kwa kumsaidia Mheshimiwa Waziri, Profesa Mkenda katika kusimamia Sekta ya Elimu bila kusahau watendaji wakiongozwa na Katibu Mkuu, bingwa kabisa mahiri dada yangu Carolyne Nombo. Hakika wanafanya kazi vizuri, watendaji wote wa Wizara na taasisi zake, ninawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini kwamba wanatembea na ile kauli kwamba, elimu ndiyo msingi wa maendeleo ya Taifa letu. Bila kuwa na elimu imara Taifa letu haliwezi kusonga mbele. Kwa hiyo waendelee kuchapa kazi, waendelee kutekeleza na kusimamia maono ya Mheshimiwa Rais na maboresho yaliyofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nifikishe salamu za wananchi wa Kasulu kutokana na kazi kubwa iliyofanywa na Serikali ya kujenga Chuo cha Ualimu cha Kabanga. Kwa hakika chuo kile kimejengwa kwa viwango vikubwa, kinapendeza; ni fahari ya Kasulu tunaipongeza sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, Chuo hiki ni miongoni mwa Vyuo vichache ambavyo vilipata bahati; jiwe la msingi limewekwa na Makamu wa Rais na uzinduzi wa chuo ukafanywa na Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Waziri atambue itifaki hiyo, akiangalie hicho chuo kama mboni ya jicho lako.

Tunashukuru kwamba kwa sasa Serikali inatuletea wanafunzi wa elimu maalum na Serikali inawafadhili kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wananchi wa Kasulu wamenituma nifikishe shukrani hizo, lakini wameniomba nifikishe pia salamu zao kwa Mheshimiwa Waziri pale. Tuna uhaba wa walimu wa sayansi pamoja na walimu wa elimu maalum. Tunaamini kwamba Serikali imefanya kazi kubwa na itaweza kutatua tatizo hilo ndani ya muda mfupi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kusahau, (maana wanasema "Usiache Mbachao kwa sala Upitao") Chuo cha Ualimu Kasulu ambacho ni chuo kongwe zaidi na chenyewe kina changamoto za miundombinu. Kwa sasa hivi hakina ukumbi wa mikutano. Kwa hiyo, bwalo la wanafunzi la kulia chakula ndiyo linatumika kama mikutano. Kwa hiyo, kunapokuwa na mikutano wanafunzi wanapata adha ya kulia chini ya miti. Kwa hiyo, Serikali hii imefanya mambo makubwa, ninaomba kwamba Chuo cha Ualimu Kasulu kiangaliwe kiweze kupata ukumbi wa mikutano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niendelee na mchango wangu kwa kuzungumzia mabadiliko, mageuzi makubwa katika Sekta ya Elimu ambayo yamefanyika. Tumeona kwamba katika mageuzi hayo kwanza muda wa wanafunzi kukaa katika elimu ya msingi umebadilika kutoka miaka saba mpaka miaka sita, lakini sasa elimu ya lazima imekuwa ni miaka 10. Vilevile, Serikali imeanzisha Mkondo wa Elimu ya Amali. Hii elimu ya amali; (hata Roma haikujengwa siku moja), tunaenda awamu kwa awamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa mujibu wa hotuba ya Waziri, kwa kuanzia wameanza na shule 201. Ninadhani iko katika ukurasa wa 51. Sasa katika Mkoa wetu wa Kigoma tunazo shule za amali tatu. Moja iko kwa dada yangu Mheshimiwa Florence Kibondo kule Kisogwe, nyingine iko Kishaga kule Buhigwe na shule ya tatu iko Kana kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma. Kwa hiyo, halmashauri nyingine ikiwepo Halmashauri ya Mji wa Kasulu bado hazijaingia katika huu mpango na tunaamini katika awamu nyingine watatukumbuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu, kwamba hizi shule za elimu ya amali zilizoko katika Mkoa wa Kigoma ni Shule ya Kisogwe peke yake ambayo ni ya bweni, hizi nyingine mbili ni shule za kutwa. Kwa hiyo, sasa tunaomba nazo zikiwa za bweni zitawezesha wanafunzi kutoka wilaya ambazo hazijawa na shule za amali kuweza kupeleka wanafunzi wakati Serikali inaendelea na utaratibu wa kuhakikisha kwamba wilaya zote nchini zinakuwa na shule hizo za amali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiwa bado katika eneo la amali, kwa sababu tunazungumzia shule za sekondari, lakini pia ninashukuru kwamba kule Kasulu Mjini tuna vyuo; Chuo cha Maendeleo ya Wananchi pamoja na Chuo cha Ufundi Stadi. Lakini kwa mapenzi makubwa ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na kwa kuona umuhimu wa kuhakikisha kwamba hakuna Mtanzania ambaye anaachwa katika kupata elimu na ujuzi, alianzisha ujenzi wa vyuo vitatu vya watu wenye ulemavu katika nchi yetu; ambavyo moja kimejengwa Kigoma, kingine kimejengwa Songwe na kingine kimejengwa Mkoa wa Ravuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ombi langu Mheshimiwa Waziri, ninatambua kwamba chuo hicho sasa kimehamishiwa rasmi kwenye Wizara yako. Juzi nilikuwa ninamsikia Naibu Waziri anajibu maswali kwamba, vyuo vyote vya *VETA* vitakamilika ifikapo Septemba. Ninaomba na hicho chuo cha watu wenye ulemavu Kasulu, chuo cha ufundi stadi ambacho kinajengwa kwenye Kata ya Nyumbigwa, kiwe katika mipango yenu na kiwe miongoni mwa vyuo ambavyo mnasema vyote vya ufundi stadi vitakamilika mwezi Septemba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sasa nijielekeze mchango wangu katika udhibiti ubora wa shule. Tunafahamu kwamba udhibiti ubora wa shule ndiyo jicho letu katika Sekta ya Elimu, kama ambavyo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali alivyo jicho letu kwenye masuala ya kifedha. Ninashukuru sana Serikali imeendelea kufanyia kazi ofisi za uthibiti ubora kuhakikisha kwamba zinaendelea kufanyiwa maboresho ya vifaa, lakini pia kuhakikisha kwamba wathibiti ubora wanafanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, kutokana na mageuzi makubwa ya kihistoria ambayo tumeyafanya katika Sekta yetu ya Elimu, ni muhimu zaidi kuhakikisha kwamba Idara hii ya tdhibiti ubora wa Shule inawezeshwa kikamilifu ili iweze kusimamia na kufuatilia kujiridhisha kama mitaala ambayo imeboreshwa, taratibu za elimu na masuala yote ambayo yanaambatana na mageuzi ambayo yamefanyika yanazingatiwa ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni muhimu sana Mheshimiwa Waziri kuhakikisha kwamba udhibiti ubora wanapata vitendea kazi, lakini pia wanawezeshwa kwenda kukagua shule. Nimefurahi kuona kwamba kwenye ripoti yako unaonyesha wameshaanza kufuatilia hizi elimu za amali. Elimu ya Amali ni muhimu sana katika kumkomboa kijana wa Kitanzania, kwa sababu itampa nyenzo za kuweza kujiajiri au kuajiriwa. Katika hii Mheshimiwa Waziri, tunapofuatilia udhibiti ubora tusisahau kuendelea kutoa mafunzo kazini kwa walimu, kwa sababu walimu ndiyo wanaotekeleza hii mitaala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaweza ukamfundisha mwanafuzi hata akiwa chini ya mti, lakini kama hakuna mwalimu huwezi kufanya kitu. Katika hilo ninaipongeza Serikali, imezingatia sana suala la miundombinu, kama ambavyo nimeeleza, shule zinaendelea kujengwa, shule za msingi, shule za sekondari na ni shule za kisasa, yaani zinapendeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule kwetu Kasulu kuna tope, wakati mwingine mwanafunzi anaogopa hata kukanyaga zile *tiles* maana yake zinakuwa zinang'aa. Kwa hiyo, tunapongeza sana kazi kubwa ambayo imefanyika, lakini tusisahau, msingi mkubwa wa mafanikio katika mitaala ni weledi wa walimu na Serikali imeonyesha utayari wa kuhakikisha kwamba inaimarisha walimu katika kutekeleza mitaala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo Mheshimiwa Waziri ametoa taarifa yake kwenye hotuba yake, mwezi uliopita walimu 150 wa Elimu ya Amali walienda India kwa ajili ya kupatiwa mafunzo. Kwa kweli hiyo ni hatua muhimu na inaonyesha utayari na dhamira ya

dhati ya Serikali ya kuhakikisha mabadiliko yaliyofanywa katika Sekta ya Elimu yanafikiwa kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali, walimu hao 150 ni chachu kwa walimu wengine. Tuendelee kuwa na mipango thabiti ya kutoa mafunzo kazini kwa walimu wetu, walimu wa mafunzo ya amali na masomo mengine ili kuendelea kutoa elimu iliyo bora kwa watoto wa Kitanzania. Kwa hiyo, tuwapeleke nje ya nchi kama ambavyo mmefanya kwa hawa walimu 150. Tuendelee kufanya hivyo, India pamoja na nchi nyingine ambazo zimejikita zaidi katika kutoa elimu ambayo ni ya mafunzo ya ufundi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niongelee kuhusu elimu maalum. Nchi yetu inatekeleza elimu jumuishi kuhakikisha kwamba hakuna mtoto wa Kitanzania ambaye anaachwa kwenye elimu. Watoto wote wa Kitanzania wapate elimu iliyo bora katika mazingira yaliyo bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza sana Wizara, wameonyesha vitu ambavyo wamepeleka, wamenunua vifaa mbalimbali kwa ajili ya kuboresha elimu maalum. Ninaomba sana waendelee kuangalia shule ambazo siyo shule za elimu maalum, lakini zinachukua wanafunzi wenye ulemavu kwa sababu nchi yetu inatekeleza elimu jumuishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake mara nyingi vifaa vinakuwa ...

**MWENYEKITI:** Profesa muda wako umekwisha, ninaomba uhitimishe.

**MHE. PROF. JOYCE L. NDALICHAKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ooh! Ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako. Ninamwita sasa Mheshimiwa Zuberi Yahya Mfaume, atafuatiwa na Mheshimiwa Alan Thomas Mvano, Mheshimiwa Kija Limbu Ntemi ajiandae.

**MHE. ZUBERI Y. MFAUME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa ili nichangie katika wasilisho hili la bajeti ya Wizara ya Elimu. Kwanza kabisa ninapenda nitoe pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Rais kwa namna anavyoongeza pesa katika Wizara ya Elimu. Maana yake nini? Maana yake anataka kufuta ujinga katika Taifa letu. Ahsante sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda pia nimpongeze kaka yangu na *school mate* wangu Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda kwa kazi nzuri anayoifanya katika Wizara yake, pamoja na dada yangu Mheshimiwa Wanu ambaye pia tunatoka Umoja kule Morogoro Kusini. Hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoa pongezi za dhati kwa sababu moja ya ajenda iliyonileta Bungeni ni elimu katika Jimbo la Morogoro Kusini. Tuna changamoto kubwa sana ya elimu na mwanzo mpya kwetu ni kwa Mheshimiwa Rais kutujengea Sekondari ya Sayansi ya Wasichana ya Kimkakati. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba sasa Mheshimiwa Waziri, sekondari ile ina ubadhirifu. Pesa iliyotumika katika ujenzi imekwenda nyingi kulingana na kile ambacho mpaka sasa kimefikiwa. Ninamwomba Waziri aunde tume maalum kwenda kuichunguza Shule ya Sekondari ya Morogoro. Pia, ninamwomba Mheshimiwa Profesa, shule hii pia inakosa walimu wa kusaidia ndugu zetu wenye ulemavu. Shule ile pia ina wenzetu wasiosikia, wenzetu wasioona na wale *slow learners*, lakini hakuna walimu wa kuwasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu kubwa 70% ya majengo katika shule yetu katika jimbo letu ni chakavu na hayatoshi kusema yanaweza kutoa elimu bora. Mengi hayafiki vyumba saba, ni vyumba vitatu mpaka vinne ambavyo ndivyo kuna darasa la kwanza mpaka la saba. Unaweza ukafikiria ni elimu ya namna gani inatoka hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haitoshi, jiografia ya jimbo letu ni ya milima, mito na makorongo kwa kweli. Kwa hiyo, walimu wanaofanya kazi katika mazingira yale ni sehemu ya walimu miongoni mwa watumishi katika Idara ya Elimu wanaofanya kazi katika

mazingira magumu sana. Kwa namna ya kipekee ninaiomba Wizara ya Elimu kutengeneza posho maalum ya mazingira magumu ya kazi. Huko ni kugumu na ninapenda pia niwaalike siku moja tukatembelee Jimbo la Morogoro Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia niiombe sasa Wizara ya Elimu ikapitie pia utaratibu ambao unamwondoa mtoto wa Kitanzania aliyefaulu lakini ametokea *private school* kukosa mkopo kutoka Bodi ya Mikopo. Utaratibu huu unawabagua watoto wetu ambao wote wanakuja kulitumikia Taifa hili kwa pamoja. Kwa hiyo, ninapenda utaratibu huu uangaliwe upya ili uweze kutoa nafuu kwa watoto wa Kitanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, sikuwa na mengi sana ya kuchangia zaidi ya kusema ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Zuberi Yahya Mfaume. Nilimwita Mheshimiwa Alan Thomas Mvano, atafuatiwa na Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela.

**MHE. ALAN T. MVANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ili niweze kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia; Wizara ambayo ni muhimu sana katika Taifa letu; Wizara ambayo inaandaa kizazi na Wizara ambayo ndiyo inayotengeneza maarifa na ustawi wa jamii yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipatia nafasi hii, lakini vilevile ninampongeza pia Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo anaendelea kuifanya katika Taifa letu. Sisi wote tunaona mageuzi yanayoendelea kufanyika katika Wizara hii ya Elimu. Kwa kweli lazima tumpongeze kwa sababu tunaona kazi anayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia katika hotuba iliyowasilishwa hapa, ufaulu umekuwa ukiongezeka, na kwa mwaka uliopita darasa la nne wamefaulu 88.91%. Ukiangalia darasa la saba wamefaulu kwa 81.8%. Ukiangalia kidato cha pili 91.13% na kidato cha nne 94.15%.

Hata katika Wilaya ya Kakonko mimi binafsi nimeshuhudia namna ambavyo Mheshimiwa Rais amewekeza katika elimu, kwa sababu Shule ya Sekondari ya Amani *(Amani Girls Secondary School)* imekuwa ya kwanza katika Mkoa wa Kigoma kutokea katika Wilaya ya Kakonko. Kwa hiyo, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais. Tunaipongeza sana kazi kubwa inayofanywa na Wizara yetu hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia yapo mambo mengi ambayo yameendelea kufanyika. Vyuo vya *VETA* vinaendelea kujengwa na sisi katika Wilaya ya Kakonko tunaendelea kushukuru kwa sababu Chuo cha *VETA,* ujenzi wake umefikia 77%. Tunaamini kwamba muda siyo mrefu chuo hicho kitakamilika na kitatoa huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mambo hayo, Wilaya ya Kakonko imepokea watumishi walimu wapya takribani 60 ndani ya muda mchache uliopita. Kwa hiyo, tunashukuru sana na tunaamini hili linakwenda kufanya mageuzi katika eneo hili la elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mambo hayo na pongezi hizo, yapo mambo machache ambayo katika Wilaya ya Kakonko tungependa kuona pia yanafanyika ili tuweze kuendeleza ufaulu wa watoto wetu na kuifanya elimu iweze kupaa zaidi. Kwanza kabisa kama nilivyosema awali, tunaomba chuo hiki cha *VETA* kiweze kukamilika ili hawa wanafunzi wanaomaliza shule za sekondari, basi waweze kupata sehemu ya kwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, tumekuwa tukishuhudia uhaba wa mabweni na mojawapo kati ya shule ambayo ni muhimu sana imekuwa ikihudumia watoto wenye mahitaji maalum; Shule ya Msingi Itumbiko. Shule hii tunaomba sana sana Wizara hii ya Elimu itusaidie kwa kushirikiana na TAMISEMI ili tuweze kuongeza mabweni, watoto wetu wenye mahitaji maalum tuweze kuwachukua na kuwaweka pale ili waweze kupata ujuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo, zipo shule za sekondari mbili; Shule ya Sekondari ya Gwanumpu na Shule ya Sekondari ya Muhange. Shule hizi tulipenda ziwe shule ambazo zitakuwa na kidato cha tano na cha sita, lakini tumeshindwa kuendelea mbele kwa sababu ya uhaba wa mabweni. Tunashukuru Serikali kwamba tarehe 13 ya mwezi Aprili, mwezi uliopita, tumeweza kupata usajili wa shule tatu za kidato cha tano na sita. Hii inakwenda kuongeza shule hizo kufikia idadi ya shule tano, wakati awali tulikuwa na shule mbili peke yake. Kwa hiyo, tunaomba Wizara hii ya Elimu ituangalie na tuweze kupata ongezeko katika eneo hilo la mabweni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo, ili tuweze kutengeneza ufaulu mkubwa kwa watoto wetu tunahitaji kuwa na mazingira mazuri ya watumishi wetu. Zipo shule ambazo zimekaa katika maeneo ambayo upatikanaji wa nyumba za kupanga ni changamoto na nyumba za walimu ni sawa na hakuna, ni chache kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitataja mfano wa shule tatu. Shule moja inaitwa Shule ya Msingi Nyamwilonge. Pale walimu wa kike na walimu wa kiume wanaishi kwenye nyumba moja tu iliyoko pale ya Serikali. Kwa hiyo, tunaomba sana Serikali itusaidie ili tuweze kupata ongezeko la nyumba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shule ya Msingi ya Kavungwe na Shule ya Msingi Nanyakaviru zote zimekuwa zina changamoto kubwa ya uhaba wa nyumba za watumishi. Kwa hiyo, tunaomba sana Serikali ituangalie ili walimu wetu hawa waweze kufanya kazi katika mazingira mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho katika maeneno ambayo tungependa kuona yanafanyika katika Wilaya ya Kakonko, tunaomba pia na sisi katika mpango unaokuja basi tuweze kupata shule ya amali ili tuweze kupata vijana wengi ambao watanufaika na kuongeza ufaulu wao na ujuzi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mambo hayo yote, yapo mambo kadhaa ambayo yanaligusa Taifa katika ujumla wake. Jambo la kwanza ninapenda kushauri, kwa sababu ili tuweze kujenga

mabweni, ili tuweze kujenga madarasa, tuweze kuwa na madawati, tunahitaji fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, ninapendekeza kwamba, Wizara iangalie ikiwezekana kuanzisha Mfuko Maalum wa Maendeleo ya Miundombinu ya Elimu katika Taifa letu, ili Mfuko huu uhusishe wadau mbalimbali, wafanyabiashara, watu wote wenye mapenzi mema basi waweze kuchangia ili mwisho wa siku tuweze kutumia Mfuko huu kwa ajili ya kujenga miundombinu hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ninaendelea kuweka msisitizo kwenye jambo ambalo tayari limekwishasemwa kwamba wapo vijana wengi ambao wamesoma wametoka vyuoni wako mtaani. Vilevile, tunaendelea kuona uhaba wa walimu katika shule zetu. Kwa hiyo, ninaendelea kupendekeza kwamba Wizara ione sababu ya kuanzisha ajira za mikataba kwa walimu wetu ili kuongeza idadi ya walimu katika shule zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukubaliane kabisa kwamba, Wizara itusaidie kigezo cha kujitolea katika shule zetu; walimu wanaojitolea katika shule zetu, walimu ambao watatumika kwa kupitia hii mikataba mifupi ya ajira, basi inapotokea ajira zimetangazwa wapewe kipaumbele, yaani hili liwekwe kabisa kama jambo muhimu ili tuwatie moyo vijana wetu na tuweze kuongeza *speed* ya walimu wetu katika kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu na la mwisho ambalo ninapenda kupendekeza kwenye eneo hili la elimu ni kwamba ili tuweze kuibua na kuendeleza vipaji na kwa kuwa ukiangalia jukumu la Wizara ya Elimu, jukumu namba sita ni kuendeleza vipaji na jukumu namba tisa ni kubaini na kuendeleza ujuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapendekeza kwa Wizara kwamba, kila sekondari sasa ianzishwe klabu za ubunifu *(innovation clubs)* ili watoto wetu waweze kuibua vipaji vyao, wapate nafasi ya kuonesha uwezo wao na mwisho wa siku kama tunavyoona mpango mzuri wa kutoa motisha kutoka Serikalini basi watoto wetu hawa waweze

kupata moyo, wajengwe vizuri na mwisho wa siku waje wawe na mchango mkubwa katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie tena kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Profesa Mkenda, lakini Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Wanu, vilevile Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa na dhamira njema ambayo tunaiona, sisi kazi yetu ni moja ni kuwatia moyo na kuwapatia ushirikiano kuhakikisha kazi waliyoifanya inaendelea kuleta matunda katika jamii yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, ninaunga mkono hoja.  Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako. Nimwite sasa Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela, atafuatiwa na Mheshimiwa Arif Suleiman Premji, Mheshimiwa Wanu Hafidh Ameir ajiandae.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa nafasi, nitaanza kujadili au kuchangia hotuba hii aliyoitoa Mheshimiwa Waziri, kwa aya moja ya *Quran,* lakini aya moja pia ya Biblia. Lengo ni kujaribu kukumbusha umuhimu wa elimu, kwenye *Quran* kuna sura maarufu kabisa sura ile inayozungumzia masuala ya elimu *(Iqra)*, *Iqra bismi Rabbika Iladhi khalaq*, kuanzia aya ya kwanza na mpaka *akhirihi*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Hosea kwenye Biblia, Hosea 4:6, inasema kwamba "Watu wangu wanaangamizwa kwa kukosa maarifa." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nimezungumzia hizi sura mbili za dini katika suala la elimu, imesisitiza sana sana umuhimu wa elimu kwa sababu kwenye *Quran* kama ilivyozungumza ni cha msingi kabisa kwamba hakuna kitu cha msingi muhimu duniani zaidi ya elimu na ndiyo sura ya kwanza kabisa imezingatiwa kupewa Nabii Muhammad *(S.A.W)* kwa ajili hiyo, kwamba achukue mazingatio hayo, lakini pia kwenye Biblia kama tulivyoona imeonesha kwamba mtu yule ambaye

hana elimu anafananishwa na mtu aliyeangamia au anatafsiriwa kwamba ni mtu aliyeangamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ni silaha muhimu sana ya mapambano ya maendeleo kama mtu yoyote yule anahitaji kuendelea basi kitu cha msingi kabisa lazima awe amepata elimu ya kutosha kabisa itakayomwezesha yeye kujihami na mazingira yanayomkabili, lakini elimu ndiyo inayotofautisha jamii yoyote iliyostaarabika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tofauti yetu sisi na watu wale walioendelea hakuna kitu kingine chochote; siyo mali, vyanzo vya mali wala nini isipokuwa ni elimu tu, kwa sababu tumeona nchi nyingi duniani ambazo hazina mali kwa maana ya maliasili lakini zimefika kuwa na maendeleo makubwa sana, lakini sisi ambao tayari tunazo maliasili za kutosha bado tukiendelea kuhangaika na kuumia na umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa kukosa elimu ndiyo tumeendelea kuwa na maisha duni na kuendelea kuumia na maradhi hali ya kuwa tumezungukwa au tumezingirwa kama nilivyosema pale mwanzo na maliasili lukuki kabisa. Katika kukosa elimu kumetupeleka sehemu ambapo sasa hivi tunajiuliza tukijifananisha na nchi ambazo tulikuwa nazo katika mustakabali uliokuwa sawa kabisa wa kiuchumi. Kwa mfano *per capital income* mwaka 1960 kwa Tanzania ilikuwa ni takribani Dola za Marekani 112, hali ya kuwa nchi kama China ilikuwa na *per capital income* ndogo kabisa ya dola 90, kwamba sisi tulikuwa na *per capital income* kubwa kuliko hata China mwaka 1960.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini kimeendelea *so far*, mpaka sasa hivi Tanzania *per capital income* ni dola 1.4 hali ya kuwa wale wenzetu wa China sasa hivi *per capital income* imepanda kutoka zile dola 90 na kufika dola 14,800. Hii yote ni kwa sababu ya sisi kukosa maarifa au kukosa elimu tukashindwa ku-*sustain* kuwa katika hali ambayo ya maendeleo, lakini tukashuka, yaani badala ya kuendelea tumerudi chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili siyo rahisi kulizungumza tu hivi kama huna uelewa. Tunalizungumzia hili jambo ni kwa sababu gani, sisi tunahitaji maendeleo, lakini ni gumu. Ugumu wake unakuja vipi? Kuwekeza katika elimu ni suala gumu sana, hususani sisi wanasiasa kwa sababu tunatamani sana kuona uwekezaji ukitokea katika eneo ambalo lina matokeo. Matokeo yanayoonekana hapo kwa hapo: mimi Mbunge halikadhalika Diwani na wanasiasa wengine wangetamani sana kuona uwekezaji umefanyika katika sehemu ambapo utaleta *interest* yako kuonekana kwa wazi, kwa maana gani? Kwamba kunatokea kusudi baadaye uweze kunufaika kisiasa hapo baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya hali hiyo ya elimu lakini imekuwa ni kitu muhimu sana ambayo kwa namna moja au nyingine tunatakiwa sote kwa pamoja tupambane au tuungane mkono kwa dhati kabisa tuhakikishe kwamba tunawekeza elimu kwenye elimu kwa kiwango kikubwa kabisa. Kwa mfano, hali ya sasa ilivyo, kumekuwa na ongezeko la wanafunzi ambao watakuja kujiunga katika shule za sekondari wanafunzi takribani 1,600,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanafunzi hao mahitaji yao kwa pamoja yatahitaji takribani isiyopungua shilingi trilioni 2.4 mpaka tano hivi, kwa nini? Kutakuwa kunahitajika majengo ya maabara yasiyopungua takribani 9,300, lakini majengo ya shule yatahitajika takribani 35,000, halikadhalika kutahitajika pia ajira za walimu wapya takribani 35,000, halikadhalika kutahitajika mashimo ya choo takribani 72,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla wake mahitaji yake yatakuwa siyo pungufu ya shilingi trilioni 2.4. Hapo panahitaji nguvu kubwa sana katika kuhakikisha jambo hili linafanikiwa na ndipo pale niliposema kwamba, ni vigumu sana au jambo hili la uwekezaji ni ngumu kwa hiyo, linahitaji mkanda kwetu sisi sote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwamini sana sana Mheshimiwa Waziri, kwa *transformation*. Alishafanya *transformation* kwenye kilimo, hakuna mtu asiyefahamu kwamba matokeo ya kilimo ambayo mpaka sasa hivi tumekuwa tukiyaimba kwa kipindi kifupi japo

hayakwenda vizuri sana yalianzia kwake na hata hili la elimu pia tumeona pale alipoanzia na huku anapoelekea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hakika ninataka nimpe moyo, lakini nimpe moyo Mheshimiwa Rais kwa kazi hii ngumu ambayo tunatakiwa kwa pamoja tuanze kuhangaika kuisukuma kwa sababu hatuna njia wala hatuna jinsi ya kukwepa. Elimu ni sehemu muhimu ambayo itaweza kututoa, vijana wanasema hatuwezi kutoka bila elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijaribu kuzungumza kuhusiana na hali halisi iliyopo kwa mfano katika jimbo langu, maana yake ningeomba nisilisahau pia. Ninashukuru sana kwa jitihada za Mheshimiwa Rais, tumepata sekondari katika kata zote 18, sasa hivi kuna shule za sekondari katika kata zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na shukrani hizo bado kumekuwa na changamoto moja ndogo ambayo ningeomba rasmi kabisa kwa Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Waziri ambaye ni pacha wake katika Wizara ya TAMISEMI, kunisaidia kuhakikisha kwamba tunapata mabweni kwa sababu gani? Kwa sababu shule hizi zipo mbali kutoka vijijini kuelekea pale shule zilipokuwa zimejengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejaribu kuuliza mara kwa mara jambo hili hapa ndani nimepata majibu ya kuambiwa kwamba kuna mpango wa kupeleka shule maeneo jirani. Mpango huu unaweza kufanikiwa katika miji peke yake, sababu kubwa ni nini? sababu mjini kuna usafiri, kuna mabasi ambayo yanaweza kusafirisha wanafunzi wakaenda katika eneo la shule, yaani kwa maana ya *public transport*...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mchungahela, muda wako umekwisha, ninaomba uhitimishe.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nimwite sasa Mheshimiwa Arif Premji, atafuatiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri.

**MHE. ARIF S. PREMJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwanza nichukue fursa hii kukushukuru kwa kuwa nimepata nafasi ya kuchangia kwenye Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Awali ya yote, niwapongeze sana Waziri wetu na Naibu Waziri wetu na Mheshimiwa Rais wetu kwa ujumla. Sababu zipo za kimsingi kabisa, moja ya sababu ukiangalia kwenye bajeti ya *execution report* ya 2024/2025, Wizara hii imefanya kazi yake kwa 90% ukiangalia kwenye wasilisho lao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine Mwaka wa Fedha 2024/2025 wameajiri walimu takribani 4,016 kwa mwaka uliopita, lakini hawa walikuwa wa *primary* lakini pia wameajiri kwenye upande wa sekondari 8,660. Lingine ndani ya siku 100 Mheshimiwa Rais akatoa ajira ya walimu 7000, hiyo ni dhahiri kabisa bila hiyana inabidi tuwapongeze sana kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 610 *AD (Anno Domini)* ni Kilatini hicho maana yake *in the year of the Lord*. Nje ya Makka kwenye Pango la Hiraa ndiyo Mtume wetu alipelekewa ujumbe wa kwanza na Malaika Jibril ndiyo likaja lile neno "*Iqra*", maana yake "Soma", mwanadamu soma na huo ndiyo msingi wetu wa maisha na ndiyo Taifa ambalo inabidi tuwekeze sana kwenye elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niendelee kwa kuchangia, tunapochukua watoto wetu na kuwapeleka shule lazima tunakuwa na dhamira, je, dhamira yetu ni kuwachukua watoto wetu kuwapeleka shule na wakishahitimu watoke na *CV* zao kwenda kwenye taasisi au makampuni kuomba ajira? Au tunataka kuwapeleka shule wapate ujuzi, wapate elimu warudi kwenye jamii waangalie changamoto iliyopo ndani ya jamii watatue kwa kuona kama ni fursa na kuwasaidia kuwapatia ajira watu wengine, inabidi tujitafakari hapo, lazima tujue dhamira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ninataka niainishe kitu kimoja; tuna changamoto, mfano wa uhalisia kabisa; kompyuta ya kwanza

kutengenezwa ilikuwa mwaka 1945/1946 ndiyo kompyuta ya kwanza ilitengenezwa *electronic computer*. Mwaka 1951 ikatengenezwa kompyuta ya kibiashara *(universal automatic computer)* na mwaka 1971 ndiyo ikatengenezwa *personal computer (PC)* ya kibinafsi ambayo ilikuwa inaitwa *Kenbak-1*. Sasa tujiulize swali moja, mwaka 1971 mwaka huu ni 2026 ni miaka mingapi iliyopita? Ni miaka 55.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tujiulize kwenye shule zetu za msingi, za sekondari kuna kompyuta ngapi? Ukiangalia takwimu kwenye vijiji, ninaongelea vijijini maana yake mimi ninatokea vijijini huko *fourteen points, one percent something like that*. Kwa hiyo, bado tunauhitaji mkubwa, bado Wizara hii inahitaji fedha kubwa kuwekeza kwenye elimu kwa ajili ya Taifa letu na hiyo itasababisha tuweze kufikia kwenye lengo la dira ya 2050. Bado tupo *behind 55 years*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ni changamoto ya muda, tumeachwa na muda, kwa hiyo, ni lazima *we should pick up ourself increase the pace* tuweze kufika huko. Jambo lingine tuje; hatuna utaratibu wa ku-*acknowledge* vitu ambavyo tunavyo na hii nitaongea kwa *fact* pia, kuna wanasayansi wetu ambao walienda *glass globe* 2025, ninadhani ni wanasayansi watano walitoka *Ifakara University* na wakatengeneza *system* ambayo wanaweza wakajua malaria kwa kutumia *artificial intelligence*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa cha kustaajabu utakuta *university* nyingine ambazo zipo nje ya nchi wanapewa tuzo, lakini sisi humu ndani kwenye *acknowledge* hatuwa-*acknowledge*. Lazima tuwape *morale*, tuwape motisha ili ku-*encourage* kuwekeza zaidi na zaidi kwenye *science* yetu, kwa kuwa wao ni wanasayansi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nije; uwekezaji kwenye teknolojia bado tupo nyuma na hiyo ninataka niongee kwa *fact* pia. Ulimwengu wa sasa hivi unahitaji *EV batteries*, sisi Mwenyezi Mungu ametujaalia *Graphite*, *Nickel*, *Lithium* vyote vipo nchini kwetu, lakini teknolojia ya kuibadilisha iweze kutengenezwa kuwa *battery* hatuna. Ni jukumu la Wizara hii kuwafunda watoto, kuwatengeneza vijana wetu waweze kutumia rasilimali hizo na kuzigeuza ili ziwe fursa kwa wananchi wetu, ndiyo kinachotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe sana, bajeti hiyo ni ndogo mno kwa wakati ambao tunakwenda, tupo kwenye *digital era*. Tunatambua, Serikali yetu inafanya jitihada kubwa sana katika kuwekeza kwenye elimu, sayansi na teknolojia, *they are doing they are best,* lakini kwa *error* ambayo iliyoko waongeze kasi, muda unatuacha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niende kwenye Jimbo langu la Mtwara Vijijini. Tumepokea shule ya amali, ninashukuru sana lakini tuna uhitaji wa bweni pale. Mheshimiwa Profesa, Waziri wetu bweni pale litaleta mantiki maana yake katika kata 21 shule iliyopo ni moja tu hiyo hiyo. Kwa hiyo tukuombe hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala lingine kwenye Ilani yetu ya Chama Cha Mapinduzi ya 2025-2030, Mkoa wa Mtwara imeainishwa kwamba kuna chuo kikuu cha Serikali. Ninaomba waliangalie na hilo pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia niwaombee sana kila la heri Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri, tena nilikuwa ninapita pita nikawa ninaangalia maana ya neno Adolf, ukienda Ujerumani kule wanasema maana yake ni *noble warrior* na ukienda China maana ya neno Wanu ni *elegant* na *graceful*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa faida ya muda, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Premji kwa mchango wako. Ninamwita sasa Naibu Waziri, Mheshimiwa Wanu Hafidh Ameir.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii na kabla ya yote niseme ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya, uzima na uhai kwa kukutana leo hii hapa kujadili bajeti hii ya mwaka wa fedha 2026/2027 ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ninaomba nichukue fursa hii kumshukuru Rais Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri na kubwa ambayo ameifanya katika sekta hii ya elimu ambayo kila mmoja wetu aliyesimama hapa kuchangia bajeti hii amezungumzia mazuri ambayo yamefanywa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nichukue fursa hii nimpongeze msaidizi wake, Mheshimiwa Dkt. Emmanuel Nchimbi kwa kazi kubwa anayoifanya ya kumsaidia Mheshimiwa Rais. Pia, nichukue fursa hii kumpongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba kwa kazi nzuri sana anayoifanya ya kumsaidia Mheshimiwa Rais. Hivi tunavyozungumza Mheshimiwa Waziri Mkuu yupo Gairo akizungumza na wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshiriki pia ziara zake nyingi sana, tukifika kule huwa kuna deski la kero. Tukiingia pale tunakuta lundo la kero, lakini hadi tunaondoka pale kero zile anakuwa ameshazishughulikia. Kama ni kiatu basi Mheshimiwa Waziri Mkuu ameleta pea mpya. Kama ni kufananisha, basi tumsubiri atakayefuata yeye ili tuone kama kimemtosha au kinampwaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama wengine wote walivyosismama hapa, nichukue pia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuniteua kuwa msaidizi wa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia. Ninaamini haya si matakwa yake yeye ila ni matakwa ya Mwenyezi Mungu na wala siyo matakwa ya kwangu mimi ila ni matakwa ya Mwenyezi Mungu. Kwa ku-*cement* hilo ninaomba ninukuu kutoka katika vitabu vitakatifu. Kwanza nianze na *Quran, surat Al Imran* aya ya 25; "Ewe mola aliyeumiliki ufalme wote humpa ufalme amtakaye na humwondolea ufalme amtakaye na kumtukuza amtakaye na kumdhalilisha amtakaye. Heri imo mwa mikononi mwako bila shaka wewe ni mwenye uwezo juu ya kila jambo." Mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia ninukuu kutoka maandiko matakatifu ambayo pia yanasema: "Anayemteua yeye

hakuna wa kumpinga." Nikishukuru Chama changu Cha Mapinduzi kwa kunipa ridhaa ya kuwawakilisha wananchi wa Jimbo la Makunduchi. Hata hivyo, kama ilivyoelezwa kwamba sikuanzia hapo, niliingia katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nikiwakilisha Baraza la Wawakilishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliingia awamu ya pili kwa kuwawakilisha wanawake wa Mkoa wa Kusini Unguja na sasa hivi nipo hapa kuwawakilisha wananchi wa Jimbo la Makunduchi. Kabla ya hapo nilishawahi ku-*serve* Baraza la Wawakilishi kupitia vijana, lakini pia kupitia wanawake wa Mkoa wa Kusini Unguja, ninawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kuwashukuru Wananchi wa Jimbo la Makunduchi kwa kunipa ridhaa ya kuwawakilisha katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na niwaahidi kwamba nitawatumikia kwa moyo wangu wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nichukue fursa hii kumshukuru Waziri wangu, *the man himself,* Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda kwa kunipokea kwa mikono miwili kuwa msaidizi wake, lakini pia malezi yake, maelekezo yake, ushauri wake na maono yake ndiyo yamenifikisha hapa leo. Amekuwa *boss* mwema na ninamshukuru kwa kazi kubwa anayoifanya ya kutafsiri maono ya Mheshimiwa Rais kuyaleta katika vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii pia kumshukuru Katibu Mkuu Mama shupavu kabisa na hodari; na *management* yake kwa ushirikiano wao wanaonionesha tangu nimeingia Wizara ya Elimu *day one* nimepokelewa kwa furaha na ile furaha ipo hadi leo. Pia, ushirikiano wao wanaonipa ndiyo leo umetufikisha hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii imechangiwa na jumla ya wachangiaji 45 na wachangiaji sita wamechangia kwa maandishi. Nichukue fursa hii kuwapongeza sana Waheshimiwa Wabunge kwa moyo wangu wa dhati kabisa kwa michango yao, maono yao, mapendekezo yao waliyoyatoa kwa Wizara yetu juu ya mustakabali mzima wa elimu yetu kwa watoto wetu wa Kitanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaambie kwamba yale yote ambayo wameyawasilisha kwetu tumeyapokea na tunaahidi kwenda kuyafanyia kazi kama vile ambavyo tumekuwa tukipokea maoni ya Kamati kwa niaba yenu na tumeyafanyia kazi kama Kamati ilivyoeleza hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wangu akija atatoa ufafanuzi wa hoja nyingi ambazo zimetolewa hapa, lakini nitagusia maeneo mawili matatu ambayo kwa sasa hivi nitaanza na *hot topic* kwenye Bunge hili ambayo ni vyuo vya *VETA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkutano huu, kikao hiki cha Bunge nina maswali ambayo yameelekezwa kwenye Wizara yetu maswali 27; maswali 17 yote yanahusiana na *VETA* na maswali 10 yanahusiana na mambo mengine. Kwa hiyo, tutaona ni jinsi gani ambavyo *VETA* imekuwa muhimu kwa wananchi wetu kwenye majimbo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono mapendekezo yote ambayo Waheshimiwa Wabunge wametoa kuhusiana na *VETA* na ninaomba nipitie hoja zao na kujibu hoja zao kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kutoa fedha kwa ajili ya vyuo hivi na kama nilivyokuwa nikijibu katika maswali yangu hapa ya msingi kwamba Serikali ilianza kutoa fedha, lakini pia inaendelea kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa vyuo hivi pia kwa ajili ya kumalizia ujenzi wa awamu ya kwanza ambayo Waheshimiwa Wabunge wengi imekuwa ndiyo *concern* yao katika Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya shilingi bilioni 106 zimetolewa kwa mwaka wa fedha 2022/2023 hadi 2025/2026. Kati ya fedha hizo, shilingi 21,000,000,000 tayari zimetolewa ikiwa ni bakaa ambayo imebaki kwa ajili ya kumalizia ujenzi wa awamu ya kwanza. Tayari fedha zimepatikana na kwa mantiki hiyo ule usemi wangu ulikuwa unasema kwamba tukutane Septemba, Waheshimiwa Wabunge tukutane Septemba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa vyuo hivi vimefikia 68% ya utekelezaji wake aidha, kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Serikali

imetenga shilingi 120,000,0000,000 kupitia Fungu 21 Hazina zitakazowezesha kuendelea na ujenzi wa *VETA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ninavyosema kila siku ujenzi wa awamu ya kwanza unatarajiwa kukamilika mwezi Septemba, 2026. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wasiwe na wasiwasi na nichukue fursa hii niwaombe na niwape habari njema kwamba tayari fedha tumepokea. Tukimaliza kupitisha bajeti hii fedha zile zitaenda kugawanywa kwa zile wilaya ambazo zinaendelea na ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii pia niwaombe Waheshimiwa Wabunge, wameona ni jinsi gani wamepata shida kuomba fedha za vyuo hivi vya *VETA*. Niwaombe sana waende kusimamia fedha hizi ili tuhakikishe kwamba ujenzi wa vyuo hivi unakamilika kwa awamu ya kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja vile vile kuhusu ajira za walimu wa *VETA*. Kwa mwaka huu wa fedha, Serikali imetoa kibali cha kuajiri walimu 760 ambao pia tunakwenda kuwagawanya katika vyuo hivi ili wanafunzi wetu ama vijana wetu waendelee kupata elimu ya ufundi na stadi za kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja ya ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika vyuo vya *VETA*. Kupitia Mradi wa *Education and Skills for Productive Youth,* Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 150.33 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia. Vyuo 80 vinatoa mafunzo kwa hivi sasa na vyuo 65 vinavyoendelea kujengwa vitanufaika; na tunaamini baada ya Septemba, 2026 vyuo hivi vitakuwa vimekamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikifanya haya yote ili kuhakikisha kwamba tunaendana na mabadiliko ya teknolojia na mahitaji ya ujuzi kulingana na soko la ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumzia *VETA,* ninaomba sasa nizungumzie hoja ya kuimarisha Mafunzo ya Walimu Kazini (MEWAKA). Kwa lengo la kuimarisha mafunzo endelevu Serikali katika mwaka wa fedha 2026/2027 imetenga takribani jumla ya shilingi

bilioni 44.7 kwa ajili ya kuendelea kutoa mafunzo kazini kwa walimu. Kati ya walimu 1,489 wa elimu maalum walipatiwa mafunzo. Aidha, Serikali imegharamia mafunzo ya walimu wa amali 150 ambao wamepewa mafunzo Nchini India na juzi tulikuwa nao hapa wamesharudi wamejifunza na wanakwenda kusambaza ujuzi huu katika shule zetu za amali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, walimu 25 wa ufundi stadi *VETA* wamegharamiwa mafunzo ambayo yanatolewa Nchini Finland. Kwa hiyo, haya yote yamekuwa yakifanyika na tunaamini yanaenda kuleta mabadiliko chanya katika vyuo vyetu vya *VETA* na katika shule zetu za amali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge *almost* wengi walizungumzia kuhusu hoja kuhusu elimu jumuishi na katika hili Waheshimiwa Wabunge wanaowakilisha watu wenye mahitaji maalum wote walichangia katika eneo hili. Nichukue fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wale kwa kutekeleza kazi nzuri ambayo wenzao wenye mahitaji maalum wamewatuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kujenga miundombinu rafiki na utoaji wa vifaa visaidizi vya kujifunzia, kuimarisha mafunzo kwa walimu wa elimu maalum na kuanzisha na kuimarisha madarasa jumuishi. Niwaambie kwamba yale yote ambayo wameyapendekeza, tunaenda kuyafanyia kazi na tunaenda kuhakikisha hakuna mtoto ambaye anaachwa nyuma katika elimu ya Mtanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja ilikuja kuhusu ushirikiano wa vyuo na viwanda. Tarehe 9 Februari, 2026 tulizindua mkakati wa kuimarisha ushirikiano kati ya vyuo na viwanda kwa lengo la kuhakikisha kuwa wahitimu wa vyuo wanapata ujuzi unaokidhi mahitaji ya soko la ajira. Hadi sasa *VETA* imeingia makubaliano ya ushirikiano takribani 87 na viwanda mbalimbali kwa lengo la kuimarisha mafunzo ya ufundi stadi na kuwajengea vijana ujuzi unaoendana na mahitaji ya soko la ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makubaliano haya hayakusainiwa tu yakabaki kwenye karatasi makubaliano haya yameanza kufanya kazi. Nichukue fursa hii kipekee kumpongeza mmiliki wa *Emirates Aluminium Profile* kwa kukubali kusaini ushirikiano baina yao na *VETA* kwa ajili ya kuchukua wanafunzi na kwenda kujifunza katika viwanda vyake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mmiliki huyu anafanya kazi nzuri, nilikwenda pale kumtembelea na nilikuta zaidi ya mafundi 700 wako pale. Kilichonifurahisha zaidi mbali na kuwafundisha ujuzi lakini pia anawajenga kizalendo. Kwa hiyo, makubaliano yale hayakubaki kwenye karatasi tayari yameanza kufanya kazi na tayari tumeanza kuona matokeo chanya ya mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mengi na makubwa yamefanyika katika sekta ya elimu. Nilipokuwa nikisikiliza wachangiaji walivyokuwa wanachangia bajeti ya maji, wengi wao walitumia msemo wa 'mnyonge mnyongeni, haki yake mpeni.' Sasa mimi ninataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge kwamba pamoja na kwamba Mheshimiwa Dkt. Samia ni mnyonge, tusimnyonge na haki yake tumpe. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa malizia.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na ninawaomba Waheshimiwa Wabunge waipitishe bajeti hii ili tukatekeleze yale mazuri ambayo tumeyapanga kwa mwaka huu wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Naibu Waziri Mheshimiwa Wanu Hafidh Ameir. Ninamwita sasa Mtoa hoja aweze kuhitimisha hoja yake, Mheshimiwa Profesa Adolf Faustine Mkenda, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa fursa hii ya kuja kuhitimisha hoja yetu ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muhtasari Naibu Waziri ameelezea waliochangia, walioandika na hatua ambazo tutazichukua ikiwa ni kuhakikisha kwamba, hakuna maoni yaliyotolewa hapa, ambayo tutayachukulia kwa wepesi. Tutajitahidi kweli kuyafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba nianze, kwanza kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote humu ndani kwa michango yao mizuri sana, michango ya kututia moyo na vilevile wametupa mzigo mkubwa. Tuna dhamana kubwa sana ya kuhakikisha kwamba, tunarudisha imani waliyoonesha kwetu na kuhakikisha tunatekeleza yale ambayo tumeahidi kwenye bajeti hii kwa ukamilifu na ni ahadi yetu kwenu nyote Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatumia fursa hii kushukuru viongozi wetu; wewe Mwenyekiti wetu wa Bunge na Wenyeviti wote, Naibu Spika na wote chini ya uongozi wa Mheshimiwa Spika kwa kutuongoza vizuri katika shughuli hizi. Shukrani za pekee tunazipeleka vilevile kwa Mwenyekiti wa Kamati yetu, Mheshimiwa Husna Sekiboko, Makamu wake Mheshimiwa Magembe na Wajumbe wote wa Kamati ya Elimu, Utamaduni na Michezo kwa kweli, kwa kutusimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wametusimamia kwa umakini sana, wametoa ushauri sana, wametufuatilia sana, wametuweka wakati mwingine saa nyingi sana, kwa ajili ya kujieleza, lakini vilevile wamejaribu kutuonesha njia. Tumepokea ushauri wao, hapa tulipo kwa kweli, kama kuna mazuri ni yetu pamoja, mabaya ni ya kwetu sisi wenyewe kwa hiyo, tunaishukuru sana Kamati yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niwashukuru viongozi wenzangu katika Wizara; Mheshimiwa Wanu Hafidh Ameir, yeye ameanza siasa mimi bado ninapiga chaki. Alikuwa Mwenyekiti wa *UVCCM* Mwaka 2008, mimi wakati huo ninapiga chaki darasani kwa

hiyo, kwa kweli, nimemkuta kwenye siasa, amenikuta kwenye Wizara, tunafanya kazi vizuri, ninashukuru sana kwa ushirikiano wake. Siyo maneno mengi, lakini sisi Wizarani tunajua vitendo vyake na vingine tunaviona anavyofanya sasa hivi, hasa kujenga ushirikiano kati ya vyuo na waajiri na moja hili amelizungumza hapa, ninamshukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Katibu Mkuu wetu, Profesa Nombo, pamoja na Manaibu Katibu Wakuu kwa kazi kubwa na nzuri, ambayo wanaifanya kutusaidia mimi na Mheshimiwa Wanu katika kazi zetu. Ninawashukuru Wakurugenzi, Kamishna wa Elimu, Wakuu wa Taasisi na wenzetu wote ambao tunafanyanao kazi wizarani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda vilevile kuishukuru taasisi moja ambayo sikuitaja wakati wa bajeti, ninasema kwa sauti kabisa, inaitwa *DVV* ya Ujerumani, ambayo inatusaidia sana katika kuwa na *alternative way* ya kutoa elimu, hasa kwa wale wengine ambao wameacha shule kwa sababu, mbalimbali. Rais wetu alipotoa maelekezo kwamba, tuwarudishe wote shuleni, tulikuwa tunahitaji mbinu nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema hivyo kwa sababu, siyo wote wako tayari kurudi darasani katika shule ya aina ileile na kukaa na wanafunzi. Wengine wanataka kuwa na utaratibu wao wapate elimu ileile, ambayo tumeagizwa na Rais wetu waweze kusoma au kusoma kwa vitendo, kupata ujuzi, kuhakikisha kwamba, azma ile ya Rais wetu tusimwache mtu nyuma katika elimu kwa sababu, elimu ni ufunguo wa maisha. Unamnyang'anyaje mtu ufunguo ule labda kwa sababu ya kosa moja alilofanya au kuteleza na kadhalika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuishukuru Taasisi ya *DVV* ya Ujerumani. Ahsanteni sana, *danke,* kwa Kijerumani, kwa kazi nzuri mnayofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda nishukuru sana sana sekta binafsi. Jana walitambulishwa wamiliki wa shule na vyuo vya kati, wanawake, walikuwa hapa walitambulishwa kwa jina, mmoja mmoja. Hii ni sehemu moja tu ya sekta binafsi, ambayo tunafanya nao kazi,

lakini hawa akina mama ninawazungumzia, walivyoona mwelekeo wa Serikali wa kutoa mafunzo ya amali waliamua kwa gharama zao, kwa fedha zao, kwenda China, walisema sisi kwa sababu, tunapeleka walimu India tuliwaambia China napo ni pazuri, walienda China.

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliomba tu Katibu Mkuu aweke *at least* maafisa wawili kwa gharama zetu, kwenda kuangalia utoaji wa mafunzo ya amali China ili na wenyewe waje wahakikishe kwamba, wanaiunga Serikali mkono katika utoaji wa elimu. Kwa kweli, sekta binafsi kwa ujumla wote tunawashukuru sana, tunaamini mazungumzo yetu ya *PPP* yataenda vizuri na tutaona namna gani tunashirikiana zaidi, hasa tunavyoenda katika utoaji wa elimu kwa miaka kumi, mazungumzo yanaendelea, ninaamini tutayamaliza vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuwapongeza na kuwashukuru walimu wote, wakufunzi wote na wahadhiri wote katika shule na vyuo vyote hapa nchini kwa sababu, kwa kweli katika utekelezaji wao ndiyo wako *front,* wao ndiyo wanafanya kazi kubwa na nzuri katika mazingira tofauti tofauti. Kwa kweli, Serikali inawashukuru na tunaona juhudi za Serikali kupitia Rais wetu kuhakikisha kwamba, baadhi ya vitu ambavyo vilikuwa vinaenda taratibu kwa mfano, upungufu wa ajira, sasa hivi tunaanza kuajiri kuhakikisha kwamba, wanapata *promotion.* Tunajenga nyumba na kadhalika, lakini hiyo ni ishara tu kwamba, Serikali inawathamini sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda sana kutoa shukrani za pekee kwa wenzetu wa TAMISEMI. Sisi tumeshikilia sera, mambo mengi ya mageuzi makubwa tunayofanya, yanafanyika chini ya TAMISEMI. Kwa hiyo, ninapenda sana kumshukuru, kwanza Waziri Mkuu; nitamzungumzia baadaye kidogo na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Profesa Shemdoe, ambaye tunafanya naye kazi. Mara nyingi mtatuona tupo pamoja katika majukumu ambayo tunayafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru vilevile Mawaziri wengine wote, kwanza ninaanza na *AG,* yupo hapa. Ninamkumbusha siku moja, ninadhani ametoka, wakati tunapambana kuhakikisha safari yetu ya kwenda Afrika Kusini kupeleka vijana wa *AI* tulivyokuwa tunakwama; anapigiwa simu usiku anafanyia kazi, asubuhi tumepata

majibu. Kwa kweli, huo ni utendaji mzuri kwa *AG* wetu na Mawaziri wenzetu wote ambao tunafanya nao kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Mambo ya Nje, ambaye kwa kweli, anatusaidia sana ku-*facilitate* mawasiliano yetu na nchi za nje, kwa ajili ya kupeleka wanafunzi na kwa ajili ya *exchange programs*. Waziri wa Fedha ni lazima nimseme, asije akanisahau na yeye katika ufalme wake, lakini Mawaziri wote tunashirikiana vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niishukuru vilevile kamati mbalimbali zinazotusaidia, hasa wale ambao wako nje ya Wizara, ambao hawalipwi na Serikali. Kwa mfano, Kamati ambayo inasimamia *Samia Scholarship Extended* inatushauri, kama siyo wao kwenda *Iceland* ku-*negotiate,* pengine tungeshindwa kulipa fedha zote ambazo tunatakiwa kulipa kule. Walijitolea, walienda, wanafanya kazi sana, Kamati hii sasa hivi ipo chini ya uongozi wa Profesa Yunus Mgaya na vilevile, Kamati inayosimamia Tuzo ya Taifa ya Mwalimu Nyerere ya Uandishi Bunifu, ambayo ipo chini ya uongozi wa Profesa Penina Mlama. Hawa wote, Profesa Penina Mlama, amestaafu, lakini anafanya kazi mpaka usiku wakati mwingine kuhakikisha kwamba, shughuli zinaenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, shukrani zetu ni nyingi na mimi binafsi ninapenda vilevile kuwashukuru ndugu zetu wa Rombo kwa sababu, wameniamini niko hapa na Rais akaniona. Ninamshukuru sana Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kuniamini katika Wizara hii. Ahadi yetu sisi ambao ametuweka hapa ni kwamba, tutajitahidi kadiri ya uwezo wetu na Mungu atusaidie tusimwangushe katika majukumu haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakishukuru Chama changu Cha Mapinduzi, na humu Mwenyekiti wa Chama wa Mkoa yupo; jana alikuwepo wa Wilaya, Ndugu Mneke, wa Mkoa yupo hapa na viongozi wengine wote. Tunawaita hapa waje waone kile ambacho wametutuma tunakitekeleza vipi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika michango ya Waheshimiwa Wabunge waliosimama, tumehesabu wote 45, wamemshukuru na

kumpongeza Rais wetu sana kwa kusimamia mageuzi makubwa ya elimu kupata kutokea hapa nchini. Nitaeleza ni kwa nini sifa hizi Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anastahili na pengine tunatakiwa tuongeze zaidi na kupaza sauti, lakini kabla sijaenda huko ninasema tu, sisi ambao ametukabidhi kufanya kazi hizi anatusimamia mwenyewe, anatufuatilia na anataka apate ripoti ya utendaji wetu wa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rauis ana wasaidizi wake; Makamu wa Rais, Mheshimiwa Balozi Dkt. Nchimbi, ambaye anamsaidia na yeye amekuwepo katika matukio mbalimbali katika Wizara ya Elimu, vilevile Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, Waziri Mkuu, ambaye ni msimamizi wa Shughuli za Serikali, anatufuatilia, anatuita kujua nini kinaendelea. Tunawashukuru sana viongozi wetu hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunafanya kazi vilevile kwa karibu na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar. Tunashirikiana hata katika yale mambo ambayo siyo ya Muungano. Elimu ya juu ni ya Muungano, tunashirikiana sana, lakini mambo mengine yote tunafanya kwa pamoja, tunaalikana, tunatembeleana, tunashauriana kwa hiyo, ninapenda sana kumshukuru Waziri mwenzangu kule Zanzibar, Mheshimiwa Lela Mohamed Mussa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee namshukuru Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kazi nzuri anayoifanya kwenye elimu kule Zanzibar na kwa jinsi ambavyo Serikali ya Mapinduzi inatoa ushirikianoo kwetu katika kufanya shughuli ambazo tunazifanya hapa nchini. Kwa hiyo, nimesema Waheshimiwa Wabunge wote wamempongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa mageuzi makubwa anayoyafanya katika elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba niwapitishe kwenye historia kidogo tu kwa sababu, wakati mwingine watu wanasema, aaah, si wamefanya wengine, sifa zinaenda kwa Rais tu? Lazima wasaidizi wake wakifanya kazi, sifa ziende kwake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hili ninaomba nitoe historia kidogo. Kumbukumbu zinaonesha Rais wetu ameapa kwa mara ya kwanza kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Tarehe 19 Machi, 2021. Ndani ya siku 14 baada ya kula kiapo alikuwa na kikao Ikulu Dar es Salaam, wakati huo Waziri wa Elimu alikuwa dada yangu na rafiki yangu sana, Mheshimiwa Profesa Ndalichako, alitoa maagizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninajiuliza, ndani ya siku 14 umechukua nchi katika hali ngumu, kuna *Covid,* kuna Msiba mkubwa wa Kitaifa na mambo chungu mzima, lakini akasema Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, ninapenda nione mtoto yeyote anapoingia katika mfumo wa elimu akitoka awe ameandaliwa vizuri zaidi, apate ujuzi, aweze kujiajiri na aweze kuajirika. Akasema, kama ambavyo hatimaye amekuja kuahidi kwa Watanzania kwenye Bunge hili kwamba, Serikali yake inataka kuhakikisha kwamba, tunapitia mitaala na tunapitia tena Sera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufanya mageuzi ili kuhakikisha kwamba, kweli elimu yetu sasa hivi inamwandaa Kijana na Mtoto wa Tanzania kwa namna inayostahili katika kipindi hiki. Hilo amelisema ndani ya siku 14 tangu aape kuwa Rais na ameendelea kutamka hadharani na wale waliokuwepo wanajua, Mheshimiwa Ndalichako anafahamu na sisi wengine tunafahamu. Tumekuwa tunaitwa na kutakiwa kutoa maelezo kadhaa kuhakikisha kwamba, tunatoa msukumo mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema mageuzi haya yalianza wakati Mheshimiwa Profesa Ndalichako akiwepo. Nimeingia Wizarani nimekuta kazi ya mitaala imeanza kwa hiyo, hata kama kuna maua kidogo yanakuja kwangu lazima nigawane naye kidogo kwa kazi ambayo tayari alikuwa ameianza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha muhimu sana ni kujiuliza na ninaomba Watanzania wote watakapokuwa wanasikiliza wajiulize, hivi mtu anachukua nchi, anaongoza katika kipindi cha msiba, kuna *Covid,* yaani kuna taharuki kubwa katika nchi; unakumbuka vijana, unakumbuka umuhimu wa elimu kwa vijana katika kipindi kile na ameendelea kusimamia jambo hili mpaka sasa hivi. Kwa hiyo, zile sifa

ambazo mnampa, ambazo wamesema Wabunge wote 45 walioongea hapa, wamesema anastahili na ziada. Kwa kweli, tumpe pongezi sana Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa haya mageuzi yana mambo mengi sana. Nitajaribu kwa muda nitakaopata hapa kuzungumzia maeneo mawili, elimu ya juu na vilevile haya mageuzi mengine kuanzia elimu ya awali mpaka vyuo vya ualimu kwa muhtasari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya juu. Ninataka nilizungumze hili kwa sababu, wakati mwingine tukiona tatizo mtu anaweza akalizungumza utadhani kwamba, hali imekuwa mbaya kuliko ilivyokuwa zamani. Waheshimiwa Wabunge, sasa hivi katika kipindi hiki cha uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan tumekuwa na uwekezaji mkubwa wa miundombinu katika elimu ya juu kuliko wakati mwingine wowote katika historia ya Tanzania na hilo siyo maneno linaonekana. Linaonekana kila mahali, ujenzi wa madarasa, kumbi za mikutano, ofisi, mabweni na nyumba za wahadhiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona Kamati yetu imetembelea na kwa kweli, nimeshangaa na kwenye ripoti wamezungumza. Wametembelea ujenzi wa Kampasi ya Chuo cha Mzumbe – Tanga, wameenda *DUCE* kuangalia ujenzi mkubwa unaofanyika katika Chuo Kishiriki cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, wameenda Mloganzila hiyo ni sehemu ya *MUHAS* ujenzi ambao unaendelea mle. Huo ni ujenzi mkubwa ambao unafanyika nchi nzima na ninasema kuna kampasi zinajengwa, tunafahamu, nitaje moja moja baadhi ya maeneo kwa sababu, haya si maneno, ni vitendo na vinaonekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa kampasi za vyuo vikuu unaoendelea hapa unafanyika Kigoma, unafanyika Kagera, unafanyika Rukwa, unafanyika Ruvuma, unafanyika Lindi, tumesema Tanga, tumezungumza Tabora, unafanyika Njombe, unafanyika Mwanza, unafanyika Shinyanga na mikoa mingine, ambayo ilikuwa haina kampasi ya chuo kikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huo ni uwekezaji mkubwa ambao haukupata kutokea katika historia yetu, kwa ujenzi huu tunatumia

takribani shilingi 1,000,000,000,000/= na haya ni maelekezo ya Rais wetu kwa sababu, mwanzoni fedha hizi zilipokuwa zinatafutwa dhana ilikuwa ni kuhakikisha tumeimarisha vile vyuo na kampasi zilizopo. Kasema imarisheni zilizopo, lakini hakikisheni kwamba na huku kwingine wanatawanya hizi fursa na tunaziona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa mfano Chuo Kikuu cha Dar es Salam, mimi huwa ninaenda sana pale na nikienda hata *Vice Chancellor* anashtukia ninaingia kwenye ofisi ya uchumi, wananiruhusu, ninakaa kaa pale na *computer* ninafanya shughuli zangu. Pale kwenye Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wamepata jumla ya shilingi 307,000,000,000 katika kipindi hiki cha Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuanzia mwaka 2021 mpaka sasa hivi katika ujenzi na unaonekana, nitatoa mfano. Kwa mfano, *School of Education,* wakati ninasoma pale majengo ya zamani sana yalikuwepo, sasa hivi wamehama, wana jengo jipya, ofisi mpya nzuri, kama unaenda Changanyikeni, mpya kabisa na ofisi za wahadhiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetoka Idara ya Uchumi pale, sasa hivi imekuwa *School of Economics,* kuna jengo kubwa linajengwa, kwa ajili ya kuhakikisha kwamba, walimu wana ofisi nzuri zaidi. Hizi zilizopo ni nzuri, lakini wanapata ofisi nzuri zaidi, kwa hiyo, ujenzi kule unaendelea. Tunaona kumbi zinajengwa, ukienda pale, ukiacha mataa pale, ukiangalia kuna *School of Agriculture* inajengwa kule na ukarabati mkubwa ambao unaendelea kuimarisha miundombinu katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na vyuo vingine vyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo kusema changamoto zimekwisha, lakini ukweli ni lazima tuuseme; hatua ambayo imepigwa hadi sasa hivi, mimi kwa sababu nimekaa pale chuo kikuu, kwa muda wote ambao nimesoma sikuona ujenzi wa ofisi unafanyika kwa miaka mitatu ambayo nimesoma pale. Halafu nimebaki nimefanya *masters* pale, baada ya kuondoka ndiyo ninaanza kukuta *Business School,* ndiyo wanaanza kujenga na kadhalika, kwa hiyo, hilo ni kubwa linafanyika. Ninapenda kuwaambia wahadhiri na wanafunzi, juhudi hizo za Rais wetu zinaendelea, hazijafika mwisho. Ukiangalia upande

mwingine kuna jengo ujue na kwako vilevile tunakuja kujenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukiangalia hata sehemu nyingine, kwa mfano Butiama, amezungumza Mheshimiwa Getere; kile Chuo cha Mwalimu Nyerere pale kaangalie sasa hivi, tayari kimechukua wanafunzi na ujenzi mkubwa sana umefanyika pale. Karibu tutakuwa na mahafali pale Butiama. Hayo yote yamefanyika kipindi hiki cha Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ujenzi wote umefanyika pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mtwara, amezungumza nakumbuka Mheshimiwa Arif. Pale Mtwara tulikuwa na vyuo vya ualimu viwili, Chuo cha Ualimu Mtwara kawaida na Chuo cha Ualimu Mtwara Ufundi. Kwa maelekezo ya Rais wetu vimeunganishwa vimefanywa kuwa Kampasi ya Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Mbeya. Katibu Mkuu akawa ananiambia, watu wa Mtwara wanasema kwa nini mkiite cha Mbeya? Haitakuwa ni Mtwara *College* kama ambavyo *MUCE* ni Mkoa *college*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, neno Mtwara halitapotea, pengine kama kutakuwa na maelekezo ya kubadilisha majina kwa namna nyingine. Kwa hiyo, watu wa Mtwara wajue kabisa kuna chuo, *university college,* inajengwa pale, itafanya kazi na Mtwara watakuwa na chuo. Kwa hiyo, kuna haya mambo makubwa yamefanyika, ninapenda waelewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niseme kitu kingine kuhusu elimu ya juu. Kuna uhuru wa kufundisha *(Academic freedom)* 100%. Mhadhiri ana haki na uhuru wa kufundisha chuo kikuu yale ambayo anatakiwa kufundisha, mhadhara ambao anatakiwa kuutoa kwa sababu, wahadhiri wetu wana weledi na kuzingatia maadili ya kazi na hawaendi kufanya jinai darasani. Ukifanya jinai hata ungekuwa Waziri, vyombo vitakuja kukushughulikia, lakini unafundisha kwa weledi, unafundisha *chemistry* pale kwa weledi na kuzingatia maadili, somo lolote unafundisha, hakuna kuingiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapokiuka weledi wa kazi yako, maana vyuo vikuu kuna taratibu za kuchukuliwa hatua; ukikiuka

weledi ni suala la ki-*administration.* Wako walimu huko nyuma nikiwa ninasoma walifukuzwa kazi kwa kukosa weledi tu, kwa masuala ya kukosa uadililfu uliopindukia. Ushahidi ulivyopatikana walifukuzwa wahadhiri wawili wakati ninasoma chuo kikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, uhuru wa kufundisha upo, tutausimamia, tutaulinda, tutautetea. Ninasema wahadhiri wetu wanafanya kazi kwa weledi, ndiyo maana huoni matatizo. Wanazingatia maadili ya kazi zao, ndiyo maana tunaona wanafunzi wetu wanasoma, likitokea tatizo lingine lolote linashughulikiwa na mamlaka ya vyuo vikuu kwa taratibu zinazotakiwa. Ukitoka nje ya chuo kufanya jinai, ni sawa na nitoke nje nifanye jinai, sijui kama nitakwepa vipi, kwa hiyo, hilo ni jambo moja ambalo ninapenda lifahamike vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa mikopo ya elimu ya juu, hili ninalisema vilevile. Rais wetu alipoingia alikuta mikopo ya elimu ya juu inazunguka mahali pamoja, imefika shilingi 464,000,000,000 hiyo ilikuwa inacheza hapo tu. Alipoingia mara ya kwanza akamwagiza Waziri wetu wa Fedha, akasema humuhumu Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, alisema sitaki nione fedha hazitoshi, ongezeni na nendeni mpaka vyuo vya kati. Kwa hiyo, kutoka shilingi 464,000,000,000 leo kwenye bajeti yetu tunayoomba watupitishie ni shilingi trilioni na kidogo. Hiyo ni zaidi ya mara mbili na nyongeza hii imekuwa ikienda mwaka hadi mwaka kwa sababu, yeye anasimamia na anafanya hili. Wakati miradi mikubwa ya nchi inatekelezwa, anataka wanafunzi waende vizuri, amewaongezea posho ya siku na ninajua mazungumzo yataenda kadri uchumi unavyokwenda, ataendelea kuangalia maslahi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wahadhiri, ninawakumbusha, Mheshimiwa Profesa Yanda amezungumza hapa ninamshukuru sana kwa sababu, mambo mengine makubwa tunayoyafanya tunasahau kuyasema. Kutoa tuzo kwa wahadhiri wa masomo ya sayansi na tiba na uhandisi, ambao wamechapisha katika yale majarida makubwa ya Kitaifa. Tuzo inatolewa, mhadhiri anapewa shilingi 50,000,000. Kazi hiyo inaendelea na karibu tutakuwa na hafla ya kuwakabidhi na

vilevile kuonesha Serikali inavyowathamini wahadhiri chuoni. Tuzo hii tunaangalia uwezekano wa kwenda katika *field* nyingine zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Profesa Yanda yeye ni mtaalam aliyebobea katika mambo yale, kwa hiyo anajua umuhimu wa jambo hili na sasa hivi Serikali inatoa *scholarship* kwa wahadhiri. Mradi wa *HEET* tuliambiwa tutenge fedha za *scholarship* kwa wahadhiri, wengi wamesoma kupitia *scholarship* hii, hata wahadhiri wa vyuo binafsi wamesomeshwa kupitia mradi wa *HEET*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika upande wa masomo ya sayansi kama *data science* na *nuclear*, kipaumbele kwa upande wa *masters* kwenda juu tunatoa kwa wahadhiri wa vyuo vikuu. Kwenye Samia *Scholarship Extended Nuclear Science,* tunatoa kipaumbele kwa wahadhiri wa chuo kikuu na Samia *Scholarship Extended Data Science Artificial Intelligence Plus* tunatoa kipaumbele kwa walimu wa vyuo vikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ningependa hili tuliweke vizuri na kusema hivi, siwezi kusema changamoto zimekwisha, ninataka kusema, jamani tumetoka mbali, tumefika mbali, yaliyobaki hatuyapuuzi, hatuyachukulii kwa urahisi, tutaendelea kupambana nayo kuyatatua. Ujenzi, ukarabati unaoendelea mpaka hosteli ya Magufuli, *University of* Dar es Salaam na sehemu nyingine utaendelea ni kazi ambayo tuna maelekezo nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahali ambapo pana changamoto moja isije tukasahu kila kitu, kwa kuzingatia kitu kidogo ambacho kwa kweli, sina uhakika sana vingine vinavyosemwa na nitajaribu kwenda kuangalia ni kiasi gani. Kwa hiyo, wanafunzi wa vyuo vikuu, wahadhiri wa vyuo vikuu, wajue kwa kweli kipaumbele hicho kipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mtu mmoja, Mheshimiwa mmoja alisema hapa, kuna matatizo shule za msingi, ni kweli Mheshimiwa Taska. Ni kweli kuna matatizo hapa na pale na wakati mwingine yanaripotiwa. Sasa mtu anaweza akasema, sasa ninyi mnaenda vyuo vikuu, kwani hamjamaliza *primary,* sasa mnapeleka watu, wanafunzi Ulaya kwa nini hamjamaliza kule, lazima twende na yote, ni vigumu

sana kusema tuache tu vyuo vikuu, tuache kupeleka watu nje, tushughulikie kwanza elimu ya msingi, kwa sababu hata hiyo elimu na ufundishaji unahitaji taaluma ambayo tunaitumia kupeleka watu kule. Kwa hiyo, hilo ni moja ambalo nilitaka nilieleze na ningeweza nikalielezea kwa saa zima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mageuzi katika elimu ya juu ambayo yanafanyika chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na maelekezo yake mahususi aliyoyatoa sasa hivi, na karibu kila Mkoa unaona wana furaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu twende katika haya mageuzi mengine. Hili suala la mageuzi ya elimu ni ajenda ya vijana. Hili suala la mageuzi katika elimu ni ajenda ya ajira. Hili suala la mageuzi katika elimu ni ajenda ya uchumi na kauli aliyotoa Mheshimiwa Rais wetu wakati ule, hizo siku 14 tu baada ya kuapa kuwa kuwa Mkuu wa nchi yetu, alizungumzia umuhimu wa ujuzi ili kuhakikisha kwamba, mtu akishamaliza shule, siyo anaanza kushangaa shangaa, aweze kuajirika na kuajiriwa mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni agenda ambazo hatuwezi kuzikwepa, tutazikwepa kwa madhara makubwa. Kwa upande wa elimu, tunavyoitoa vizuri kwa mfumo mzuri, ni sawa na kusema badala ya kumpa kijana wetu samaki, unamfundisha kuvua na unampa nyavu akavue, aweze kujiajiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ngoja nielezee kidogo inavyoenda. Kabla sijaenda huko, hebu nitoe mfano mmoja. Mheshimiwa Kija Yunus alitoa mfano na nilimpigia nikamuliza tena. Kule Ruangwa, jinsi ambavyo kulikuwa na ushuhuda wa waliosoma *VETA*, ambavyo wanaonyesha wameweza kufanikiwa vizuri na kuajiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nitatoa mfano mwingine, ninatoa mfano wa kijana, yeye ameshaniruhusu nitumie jina lake, anaitwa Oscar Mboya, sasa hivi yuko Guinea, Conakry, amesoma *VETA*, amesomea ufundi mitambo ya migodini, mimi ninakutana naye ninashangaa, Guinea Conakry wanaongea Kifaransa, siyo Kiingereza,

amefikaje huko? Ameniambia siyo mimi mwenyewe, tuliosomea *VETA* katika masuala haya, wako Congo, Mauritania, Ghana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yeye alianzia Tanzania, alivyopendwa sana akachukuliwa kama ambavyo wachezaji wazuri. Kama yule Chama ninadhani lile goli, alivyochukuliwa, wakapelekwa, Namibia, kutoka pale alipelekwa Mauritania, ameenda Senegal na sasa hivi yuko Guinea Conakry. Ujuzi, elimu hii mageuzi ni kuwawezesha vijana wetu, duniani yote iwe ni uwanja wa ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano mwingine, huu unaweza uka-*google* ukamwona Tim Cook, ambaye ni *CEO* wa *Apple*. Sasa hivi ana-*step down*, aliongea, alisema, ninashangaa watu wanasema sisi tunakimbilia kuwekeza China kwa sababu ya gharama ndogo ya rasilimali watu, yaani mishahara ni midogo. Anasema, sijui wanazungumzia China ipi! China tunayoijua sasa hivi mishahara ni mikubwa. Hatuendi kule kwa sababu eti kumwajiri mtu ni gharama ndogo, Hapana! tunaenda kwa sababu China imesheheni ujuzi kuliko nchi nyingine yoyote hapa duniani. Ninataka niwatumie hii *clip* tena, kwenye *group* la Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, anasema, wakati nchi nyingi ziliacha elimu ya *polytechnics*, ziliacha mafunzo ya amali, maana yake *technical and vocational training*, katika *secondary school* kwenda zaidi kwenye *theory*, China haikuacha. Anasema nchi yake, yeye ni Mmarekani, anasema; Kwangu mimi kwenda kutafuta *technicians* wa kufanya kazi kwa ajili ya simu za *Apple* na vitu vya *Apple* ni kazi kubwa sana, lakini China ni wengi wamejaa, wamesheheni, wanavutia uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana, nimesema mageuzi haya, vilevile yanabadilisha uchumi. Unaweza ukazungumzia uwekezaji sana, basi ukifanikiwa kwa misingi ya kodi na kadhalika, watakuja hapa na kuajiri wageni kuja kufanya kazi hapa. Kwa hiyo, manufaa yatakuwa si makubwa kiasi hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii kazungumzia Tim Cook kuhusu *Apple*, ni kampuni ya Marekani inakimbilia China kuwekeza kwa

sababu ya uwekezaji mkubwa wa mambo ya ujuzi. Ndiyo maana, hapa tunazungumzia na tutaendelea kuzungumzia suala la *polytechnics*, shule za amali na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mageuzi haya, suala kubwa ni ujuzi na ubora, muda sijui kama utaruhusu kuzungumzia suala la ubora. Ninajaribu kuzungumzia jinsi ambavyo, ujuzi na jinsi tunavyokwenda pamoja, itaweza kuhakikisha kwamba watu wanaweza kusoma vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, Mheshimiwa Profesa Muhongo alizungumza vizuri sana, ninashukuru, kwamba mageuzi haya yanaji-*align* zaidi na dunia inavyoenda. Sisi *actually* ni *six plus four, plus two, plus three plus*, kwa hiyo, ukienda chuo kikuu baada ya *form six,* miaka kumi na mbili ya shule. Alitoa mifano mingi hapa siwezi kurudia, lakini kubwa hili la kuondoka kutoka elimu ya lazima miaka saba, kwenda miaka kumi, ni mageuzi makubwa ya kimfumo katika elimu kupata kutokea tangu miaka ya 1960. Ambapo Mwalimu Nyerere, kwa miaka takriban mitatu kwa awamu kupitia mikoa aliamua kubadilisha mfumo ule wa darasa la nne na darasa la nane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *lower school, middle school* na *high school* akabadilisha na kuwa na darasa la saba, lengo lilikuwa Watanzania wengi walau wasiishie darasa la nne, waishie darasa la saba. Alitekeleza alijua nchi yetu bado ilikuwa maskini sana, alitekeleza kwa awamu. Ilichaguliwa mikoa kadhaa wakaanza, baadaye mikoa mingine, baada ya mikoa mingine, halafu tukamaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenda katika miaka kumi, hili wazo halikutokea katika toleo la 2023, lilikuwepo katika Sera ya Elimu na Mafunzo ya 2014. Suala kubwa na gumu, wakati mwingine unaweza ukasema tuahirishe kwa sababu nzuri tu, tujenge Bwawa la Mwalimu Nyerere, tuweke lami zaidi, tuhakikishe kwamba tuna Daraja la Busisi, tufanye mambo chungu mzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine ni rahisi kupata kigugumizi na kusema hebu tuahirishe jambo hili tusubiri kidogo muda

uende. Kwa sababu, sasa hivi *transition rate* kutoka darasa saba kwenda *form one* ni zaidi ya 70%, kwamba twende hivyo hivyo. Inahitaji ujasiri, inahitaji kiongozi ambaye haangalii mafanikio atakayeshangiliwa sasa hivi, inahitaji *a state's person, not a politician*, wanasema *a politician looks after the next election, a state's person, a statesman or a stateswoman for that matter, look after the next generation*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uamuzi wa kusema pamoja na changamoto na mahitaji makubwa ya nchi hii, twende miaka kumi ya elimu ya lazima hapa Tanzania, ni maamuzi alifanya Mheshimiwa Rais wetu na kwa ujasiri mkubwa. Hilo wala tusingeweza kulitamka hadharani, bila kwenda kupata kibali chake na wakati anatoa kibali alisema, hili litagharimu hela nyingi, hili litakuwa mzigo mkubwa, ninajua watakuja na bakuli kutafuta hela, litasaidia vizazi vya Watanzania, litasaidia ajira, twendeni tukatekeleze, ndiyo utekelezaji huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge, kila aliyesimama hapa na kumsifu Mheshimiwa Rais wetu, wanamsifu kwa haki sana, katika mageuzi, yeye ndiyo kinara, yeye ndiyo aliamua, yeye ndiyo ame-*take risk* na kusema *let's do it*. Kazi yetu sisi ni kuhakikisha kwamba linafanyika, linatekelezeka na tunaomba Mungu atusaidie tusimwangushe katika suala hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, faida yake mojawapo ya miaka 10 ni nini. Mtoto anaingia darasa la kwanza sasa hivi, akiwa na miaka sita ndiyo utaratibu uliopo, kwa hiyo elimu ya lazima miaka saba, maana yake akimaliza darasa la saba, anaweza akaacha shule, kuna amri, kuna *instrument* ya kumko-*coerce* kubaki shuleni. Ukifanya vile, ameondoka shuleni akiwa na miaka 13.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ajira tunaizungumzia wapi, au kujiajiri tunazungumzia wapi? Dunia nzima sehemu kubwa watu wameshaondoka huko, lakini akianza na miaka sita darasa la kwanza, akaenda mpaka *form four* kwa lazima, yaani mtoto asipokwenda, mzazi tuna wewe, tutahangaika na wewe. Akimaliza *form four,*

atakuwa na miaka 16, amekaribia umri ambao kabisa unaweza ukasema anaweza akaajiriwa na kujiajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ndiyo sababu mojawapo ya mageuzi, dunia nzima *Sustainable Development Goal*, inazungumzia masuala hayo na ile *Sustainable Development Goals,* Tanzania tuli-*sign*, tuliikubali kwa hiari yetu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Rais wetu amekuja ameamua kuhakikisha kwamba tunatekeleza. Kwa hiyo, hicho ni kipengele kimoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ni kuhakikisha kwamba tunaanzisha mkondo wa amali. Waheshimiwa Wabunge, tumeanza kidogo sana, makusudi, kwa sababu hatutaki mkondo wa amali uwe na elimu ambayo wananchi wanaipuuza, wananchi wanainyanyapaa, hapa tulipo sasa hivi, kuna vijana wanamaliza *form four,* wamefanya vizuri, wanataka kwenda kwenye vyuo vya kati vya amali. Huo utaratibu umeanza kwa muda kidogo na ninafahamu wengine wanasema: *Mimi naenda DIT kufanya diploma, sitaki kwenda form five na form six.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, tunataka tukitoa mkondo wa amali, wazazi na wanafunzi waseme, naam*!* Una-*choose* vizuri. Tumeweka unyumbulisho kwamba, ukienda mkondo wa amali, unaweza ukarudi elimu jumla. Kuna mikondo miwili, mkondo wa amali na mkondo wa elimu jumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetengeneza *pathway* kwamba, mtoto atakayeenda mkondo wa amali hafungiwi kurudi kuja kusoma sheria, kusoma masomo mengine. Tunahakikisha kwamba, hatufungi hivyo ili kuhakikisha kwamba tunavutia. Hatutachagua wanaoenda kusoma mkondo wa amali kwa sababu wamefeli. Tutachagua huyu anajua kucheza mpira sana, anafahamika, *AG* mshabiki wa mpira sana, sitazungumza zaidi hapo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mnaamua kwamba aende *sports academy,* lakini anasoma, amali yake ni *sports*! Huyu ni fundi anapenda sana mitambo, kufungua fungua, anaenda mkondo wa amali wa ufundi. Anasoma lakini masomo mengine atakayoyasoma, akifika *form four* akisema, sasa mimi bwana, ninataka nirudi *form six*,

tumeweka utaratibu anaweza akarudi akaendelea ili wazazi wasiogope kupeleka watoto wao katika mkondo wa amali na elimu jumla nao tumeweka dozi kidogo ya mkondo wa amali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo atakapomaliza mtoto, akimaliza *form four*, amemaliza na ufundi anapata na cheti, watu wanakiita cha *VETA* cha *NACTVET*, kama ni ufundi magari, ufundi umeme anapata cheti anaendelea na kadhalika. Kwa hiyo, hili suala la ujuzi linalomsaidia mwanafunzi anayesoma aende vizuri katika masuala ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kauli yetu ni kwamba, elimu ya msingi inakuwa miaka sita lakini elimu ya lazima ni miaka kumi kwa sababu kuna baadhi ya watu wanasema wamepunguza tena miaka kutoka miaka saba mpaka miaka sita, hapana! Tumeongeza miaka kutoka miaka saba mpaka miaka kumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulichofanya elimu ya msingi, tumeifanya miaka sita na utekelezaji umeanza. Sasa, katika hii hakuna kurudi nyuma na hatuwezi tena kurudi nyuma, kwa nini? Wakati Mwalimu Nyerere alitekeleza yale mageuzi yake makubwa kwa awamu na alitekeleza kuanzia mwaka gani, 1965 mpaka 1968, kwa Mkoa. Chagua seti ya mikoa hii, twende, badilisha mikoa hii, twende.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hii imeamua kutekeleza kwa awamu kwa madarasa, kwa hiyo tulianza na mitaala mpya darasa la tatu. Waliokuwa darasa la nne ni mtaala wa zamani mpaka la saba, hao watamaliza elimu ya msingi mwaka 2027 mwakani. Tulienda kwa awamu ili tusikurupuke sana na kuna *challenge* nyingi katika utekelezaji. Huo ndiyo ukweli wenyewe na zitakwepo, lakini tulienda kwa awamu kidogo. Halafu wa darasa la tatu, kwenye mtaala mpya wakifika la sita mwakani wamemaliza elimu ya msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kubadilisha, hatuwezi kuwaambia sasa tunawatafutia na masomo mengine ili mkae tena miaka saba, wazazi wanajua, wanategemea hakuna kurudi nyuma. Kwa hiyo, mwaka 2027, kila shule ya msingi itakuwa na mahafali ya darasa la sita wamemaliza shule ya msingi, mahafali ya darasa la

saba wamemaliza shule ya msingi, ilikuwa hivyo mwaka 1960 kipindi cha Mwalimu Nyerere.

Mheshimiwa Mwenyekiti, darasa la nane na darasa la saba walimaliza shule kwa pamoja na walichofanya, waliunganisha shule. Shule nyingine ambazo ilikuwa ni *lower school,* imeunganishwa na *middle school,* wakaunda darasa moja ikabaki madarasa mengine kuwa na shule saba. Kwa hiyo, utekelezaji unaenda, kutakuwa na changamoto kidogo ambayo na yenyewe ilikuwepo miaka ya 1960 ya kitu tunachoiita rika mbili, *double cohort*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wale wanaomaliza shule ya msingi madarasa mawili kwa pamoja, endapo kutakuwa hamna *dropout*, *dropout* sasa hivi karibu laki tano, wakati mwingine na tunajaribu kuipunguza. Wasipokuwa *dropout* ina maana wanafunzi milioni tatu wataendelea kidato cha kwanza, kwa sababu la sita na la saba wataendelea kwa pamoja. Wakienda *form two, form one* itakuwa *single cohort,* kwa hiyo hii *double cohort* itakuja a itamalizika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utaratibu huu, tunajua kwamba, kama *dropout* haitapungua sana, idadi itapungua kidogo. Sasa hapa niseme na nimshukuru sana Mheshimiwa mmoja hapa amezungumza kumshukuru sana Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Lameck Nchemba. Waziri wetu Mkuu, yeye ndiye anayesimamia TAMISEMI. Waziri Mkuu amechukua haraka ametuita, ametaka maelezo, ametuita mara ya pili na yeye ametutia moyo amesema, jamani tusiogope mageuzi, inawezekana, kauli ya Waziri wetu Mkuu, inawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ameshatoa maelekezo kwa Wakuu wa Mikoa na suala kubwa sasa hivi, lazima kuwe na sekondari inayofikika kwa miguu, nchi nzima. Kuna changamoto zipo, kauli kwamba kuna *primary school,* kuna umbali karibu kilomita kumi ipo. Huyu ni mtoto wa *primary school,* kuanzia darasa la kwanza mpaka la saba kilomita 10, basi atakuwa anaenda sekondari kilomita 10, lakini ninaamini tutaendelea kujenga shule kupunguza huo umbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ukisema kwamba tutaacha, kwa sababu wa sekondari ambaye sasa hivi amekomaa zaidi,

asiende kilomita kumi, kama kweli huyo mwingine alitembea kilomita 10, kwa kweli hilo suala tunaweza tukaenda nalo, tuhakikishe kwamba tunamaliza, tunavuka na tunaimarisha katika shule zetu zinavyokwenda kule. Kwa hiyo, hili linatekelezwa na TAMISEMI na mkakati umeshawekwa na bajeti imewekwa na mkakati unaendelea na tutakuwa tunatoa taarifa mara kwa mara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, TAMISEMI inatekeleza, lakini sisi tunashiriki, tunafuatilia kuhakikisha kwamba kweli ziko shule za msingi kwa mahali zilipo zitaongezewa madarasa. Ukumbuke kama kuna darasa la saba litaondoka kuna darasa moja litabaki halina mtu, halafu wataendelea hivyo, kwa hiyo mageuzi haya yanakwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa kuliko yote ni kuhakikisha kwamba zile shule za amali tunazikamalisha, tunaweka na vifaa. Wameona Naibu Waziri amezungumza na baadhi wamezungumzia hapa, tunapeleka walimu mara ya kwanza nchi hii walimu 150 wote wamepakiwa kwenye ndege, wamepelekwa India kutembelea sekondari za ufundi, wakaangalie nini kinaendelea kule wakaone, kwa sababu wakija hapa tunataka tuige.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliambiwa India ni kati ya nchi bora sana katika kutoa *technical secondary school*, siyo *vocational*, *technical secondary school*. Hivyo, 150 waliopo na wamechaguliwa kwa vigezo hivyo, warudi hapa walete mabadiliko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zimetengwa kwa ajili ya kununua vifaa kwa shule hizo na tunataka tununue vifaa vile wanavyotumia wenzetu wa China, wanavyotumia wenzetu wa India, kuhakikisha kwamba *technical education* inaenda katika kiwango ambacho kinahitajika, kwa hiyo, kazi kubwa sasa hivi itakuwa ni miaka kumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi kubwa itakayokuwa mbele yetu ni kuendelea kubadilisha sekondari nyingi zaidi ziwe za amali zifike nusu zizidi ili kuhakikisha kwamba tunatoa fursa kwa vijana ambao wanataka kuajiriwa mara moja wakitoka, lakini nitaomba uvumilivu, twende taratibu wakati tunaimarisha na kasi itaongezeka tunapokwenda mbele ya safari chini ya uongozi wetu wa Mheshimiwa

Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika elimu, katika haya ninasema ukweli, yajayo yanafurahisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna swali mtu anaweza akauliza, kwa hiyo, wanawapeleka hivyo, wanawapeleka sekondari za amali, maandalizi gani, wanawapeleka wapi? Tunajenga *polytechnics* na imezungumza hapa na Wabunge kadhaa. Rudisheni *polytechnics*, wanazungumzia kama *Dar Tech*, Dodoma tumekamilisha moja, itachukua wanafunzi. *Polytechnics* iko kwa Mheshimiwa Paschal pale anaifahamu, aliniambia pale Nala, lakini ameniambia panaitwaje pale eneo lile, tutazungumza. P*olytechnic* imekamilika, kuna masuala machache ya kumalizia, tutaanza kuchukua wanafunzi, tumeweka italelewa na *DIT*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutajenga nyingine Mwanza *polytechnic*, tutajenga nyingine Kigoma, tutajenga nyingine Mtwara, tutajenga nyingine Morogoro, tutajenga nyingine Zanzibar. Kwa hiyo, tunaongeza fursa za wale ambao wanasoma masomo ya amali, hasa *technical education* waweze kuhakikisha kwamba wana fursa za kwenda kuendelea na kusoma wasije wakabaki nyuma. Sasa kwenye mageuzi haya kuna mambo mengine, ambayo pengine siyo muda wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la ubora wa elimu. Mheshimiwa Rais wetu aliahidi wakati anazindua kampeni zake kwamba ndani ya siku 100, Serikali yake itaandaa mpango wa kuhakikisha kwamba tuna mpango wa kisayansi kuhakikisha kwamba watoto wakiingia darasa la tatu wanajua vizuri kusoma, kuandika na kuhesabu (KKK) na alikuonyesha umuhimu wa jambo hili kwake alikuja mwenyewe kuzindua ule mpango na kutoa maelekezo na anataka taarifa na kazi yetu sasa hivi ni kutekeleza kwamba wale ukisikia mtu anasema labda tujue kusoma na kuandika hilo tuna-*deal* nalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna lugha imezungumzwa Kiingereza kitafundishwa kuanzia darasa la kwanza na mfumo wa kufundisha Kiingereza umebadilika. Tumepunguza kanuni nyingi ambazo zinachosha anza tu kuongea, *communication* halafu *down the road* unaweka kanuni zaidi badala ya kuanza kumwambia *past tense,*

*present tense* na kadhalika unazungumza hivyo *verb, noun* na nini vitu ambavyo anakaa anavishanga shangaa wewe unamfundisha kuongea Kiingereza, akianza kuongea anakwenda vile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeongeza masomo ya hiari. *By the way* katika ufundishaji hata Kiswahili tunajaribu kuongeza ubora wa kufundisha Kiswahili; wala tusiwe tukadhani kwamba tuko vizuri sana kwenye Kiswahili, tukaona Kiswahili chenyewe lazima tuongeze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeongeza masomo ya hiari. Tutafundisha Kifaransa kwenye shule kwa wanafunzi walio tayari kusoma na walimu wapo. Tutafundisha Kiarabu kwenye shule za msingi kwa wanafunzi walio tayari kusoma na mwalimu atakuwepo. Tutafundisha Kichina shule za msingi; na kwa kufanya hivyo tunapitia *proposal* ya mageuzi makubwa sana kwenye vyuo vya ualimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimoja tumeki-*earmark* hiki cha Marangu, kilikuwa Chuo cha Lugha sasa wanataka kuja kufanya kila kitu; ninataka warudi kwenye lugha huko huko. Tuweke maaabara za Kiarabu, Kichina, Kifaransa; mwalimu akiingia kule ajifunze lugha tu. Tunafikiria vyuo vingine vinne, vitano, vya ualimu ili kuhakikisha kwamba wakisoma pale akimaliza ualimu, hata akiamua kuwa mkalimani anaweza akawa mkalimani; akiamua kuwa *tour guide* anaweza kuwa *tour guide*, lakini tupate walimu watakaokuja kutusaidia kusoma. Kwa hiyo kuna vitu vingi sana katika suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo limezungumzwa sana Mheshimiwa Regina na watu wengine suala la maadili. La maadili ni kubwa nitaeleza kidogo tunavyo-*deal* nalo; lakini labda niseme kwanza la ujasirimali, hili limezungumzwa sana, lipo. Kwa sababu mageuzi haya; na niwaambie wakati Mheshimiwa Rais anaagiza tufanye shughuli hizi alisema shirikisheni Watanzania; mtatumia wataalam, mtajifunza kwa watu wengine, lakini ninataka nihakikishe mnawasikiliza Watanzania na wenyewe wanataka nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nilikuwa ninamwambia Mheshimiwa Wanu hapa, mambo mengi tunayoyasikia humu yamo. Kwa nini? Kwa sababu tulikuwa tumekwishaanza kusikiliza wakati ule.

Somo la biashara limekuwa ni somo la lazima kuanzia *form one* hadi *form four;* linafundishwa kijasiriamali, halifundishwi *technical* sana. Linafundishwa kukuandaa wewe kama unamaliza unaanzisha biashara yako unafanya nini, vitu gani unatakiwa kufanya. Historia na maadili ya Tanzania. Somo lipo kwa watu ambao wanadhani wana maoni wanaweza wakatuambia tuongeze tubadilishe nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, njia nyingine katika elimu ni vitabu tunavyosoma shuleni. Kuna wakati fulani hapa tulipiga marufuku baadhi ya vitabu visiingie shuleni, kwa sababu bahati nzuri sheria inaruhusu, kuna watu wakalalamika; sasa mnaondoa vitabu viko wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo sasa hivi tuzo ya Taifa ya Mwalimu Nyerere ya uandishi bunifu; ina nyanja ya vitabu vya watoto na vinakuja vingi, vinapendwa na nyanja nyingine. Tukimaliza vitabu vile vya mshindi wa kwanza tunavichukua, tunavinunua *round* ya kwanza tunavigawa kwenye shule zetu ili watoto wetu waanze kuzisoma. Humo ndani kuna vitabu ambavyo vitakuja kuwa ni vitabu vya kiada, lakini tunataka kuwe na vitabu ambavyo vinaweza vikatumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumze sasa nitaendaje, kwa sababu muda unaenda hivi. Labda niseme mambo machache kuhusu sayansi. Mheshimiwa Getere amesema jambo zuri lakini tuliangalie kwa makini. Kuna masuala mengine ambayo tunasema tunataka ku-*invest* kwa Watanzania ambao hawa tukiwapeleka wanaenda vizuri, watatusaidia katika maeneo fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika masuala ya *artificial intelligence* sehemu mojawapo. Tuna-*pick the best of the best* na hakuna *room* ya kufanya chochote. Tulivyoangalia tulifurahi sana kupata wanafunzi ambao chimbuko lao ni shule za kata, nao wamepata nafasi hizo wameenda kusoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kazi kubwa tuliyonayo ni kujenga hizi shule na kuimarisha ufundishaji ili kweli isiwe ni *skewed* kwa watu ambao wana uwezo tu; lakini wale ambao tunawapeleka

tunawapeleka ni 50 tu tunapeleka na *next round* tunapeleka 50. Tunataka tuchukue wale *top* kabisa tuwaangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe taarifa kwa Waheshimiwa Wabunge; kule *Johannesburg feedback* ninayoipata inafurahisha. Walivyoenda kule baada ya muda fulani wanasema hawa wanafunzi kwa walivyofaulu hatukutakiwa tuwa-*charge* ada. Mheshimiwa Wanu alienda kuwatembelea kule, wanasema basi *next time,* sisi tuliona kwamba ni *full funded* hatukuwapa lakini kwa ufaulu mliowaleta hawa tunaweza tukasema wapeni hela za kuishi lakini ada hatuchukui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *the same Limerick* kule wanasema wameshangazwa na uwezo wa vijana wetu. Wengine wamefanya mitihani ya kimataifa; alizungumza Profesa Muhongo, utaratibu wa kurudi katika ile mitihani inaendelea na ni muhimu lazima twende tujilinganishe na wenzetu; lakini hawa vijana wamefanya mitihani. Wamefanya mitihani ya kimataifa kwa sababu huwezi kwenda sehemu nyingine bila kufanya mitihani mingine ambayo inafahamika. Tunaona tunaenda vizuri kwa kweli. Tunahitaji *exposure* nzuri zaidi ili kuhakikisha kwamba wanaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ni kweli kwamba kunaweza kukawa na *skewedness* kidogo kwa zile shule zile bora, sijui Ilboru na kadhalika, wakapatikana wengi, lakini tutaendelea kupambana kuhakikisha kwamba hata wengine huku wanaweza wakajajiunga na huku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefurahi, shule za Serikali wapo wengi ambao wameingia mle; shule za binafsi wameingia hatuwezi kuwanyanyapa lakini ninadhani shule moja ya Sengerema na nyingine ya Tanga, shule za kata kabisa, wameweza kufaulu wakaenda huko na tunadhani twende huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mambo ya sayansi na teknolojia ninakubaliana na Waheshimiwa Wabunge, haya masuala ni muhimu sana, dunia inakokwenda hakuna namna. Kwa hiyo hizi *scholarship* mojawapo ni kivutio kwa mtoto anaposoma; na nimewasikia, yuko darasa la saba anaenda *form one* anasema mimi

bwana ninataka wazazi wangu niwapunguzie mzigo mimi nitasoma sayansi kwa bidii ili nipate *Samia Scholarship*. Ukizungumza utakuta wanafunzi wanasema hivyo; kwamba mimi nitasoma kwa bidii nipate *Samia scholarship*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo lake lilikuwa ni hilo ku-*create an incentive* ya kuwavutia badala ya kusema ninakwenda kusoma *commerce*, *law* au *economics* waende wakasome. Kwa sababu, wakifanya *degree* ya kwanza *science* wakitaka kurudi huku kwingine watarudi ila wakija kusoma *economics* unataka kwenda kusoma *engineering* huwezi tena. Mlango umeshafungwa. Kwa hiyo bora tuwavutie wengi wasome *science* halafu baadaye wakiamua kutokwenda huko wataendelea; lakini hawa watatusaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakuwa na maonyesho hapa ya kazi inayofanywa kati yetu sisi Wizara, *COSTECH* na *CRDB* kitu kinaitwa *IMBEJU*. Juzi hapa niliondoka niliomba ruhusa nikaenda kuzindua utaratibu wao. baadhi ya uvumbuzi, ninafurahi na nitaomba Waheshimiwa Wabunge wote waende wakaangalie, unafurahisha. Mtu anayevumbua vile anasaidiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisikia kauli ilisema fedha si tatizo, tatizo ni uvumbuzi ambao unaweza ukaingia katika soko. Ukishaonekana unaingia katika soko, *CRDB* wako pale watasaidia. Vilevile kuna kitu tunachoita *Samia Innovation Commercialization Fund,* kuna fedha ziko pale kwa anayefanya vizuri; na hii ni ajenda ya vijana vile vile, labda niseme vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu wavumbuzi wengi, ukiacha wachache maprofesa ambao wamezindua hadi maabara *mobile,* watakuja kuiona hapa; na namna ya kutengeneza *flasks* ngumu ambazo hazivunjiki; wanazitengeneza idara ya *chemistry* pale Chuo cha Dar es Salaam. Hizo ninaamini kabisa kwamba watakapoanza kuzizalisha *on commercial basis* ni *cheaper* na *stronger*, ninaamini tutakuwa tunazinunua kupeleka katika shule zetu. Kwa hiyo tunajaribu kuwekeza kule kwa sababu Wizara hii kama ilivyosemwa hapa, si Wizara ya Elimu tu; kuna sayansi na teknolojia, kuna mambo mengi tunayafanya kwa ajili ya shughuli hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nijaribu kumalizia vitu vingine vichache ambavyo ningependa vizungumzwe. Kwa upande wa elimu ya walimu. Uboreshaji wa vyuo vya ualimu ni mkubwa sana; wengi wanafahamu. Vingine vimeachwa; Kasulu kimeachwa chuo kimeonekana. Kwanza ile ardhi yenyewe si Serikali iliyokuwa inakimiliki; kimejengwa chuo kipya kabisa na alikuja Mheshimiwa Rais mwenyewe kukizindua. Sumbawanga kilikuwepo kimechakaa na ardhi ilikuwa si ya Serikali; kimejengwa Chuo cha Ualimu kipya kabisa kimehamishwa na Mheshimiwa Rais wetu mwenyewe alikuja kuzindua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tabora tutaangalia alichozungumza Mheshimiwa Hawa ni nini kinachoendelea kwa sababu tunavyojua ukarabati ulifanyika mkubwa sana na Vyuo vingi vya Ualimu vimefanyika. Kama nilivyosema tutavi-*organize* kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunatoa elimu vya biashara kama nilivyosema, ufundi kuhakikisha kwamba tunatoa nafasi ya ufundi lakini na *language* na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, baada ya hapo walimu wanaomaliza tumetenga bajeti, tunataka tuwape fursa wakafanye *internship* kwa mwaka, waende wakafundishe lakini siyo kwa gharama zao kwa gharama zetu; waende wakafundishe wakapate kazi na wakati mwingine hata mtu akiwa anasubiri ajira anakwenda ana-*practice* kidogo, anapata shughuli, anaongeza ujuzi na anaongeza maarifa. Ninadhani hiyo itatusaidia sana katika kuhakikisha kwamba tunaenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo ni mengi, mageuzi ni makubwa na kazi ni kubwa mbele yetu. Changamoto zitakuwepo; za vitabu zimesemwa hapa. Ninaamini sasa hivi tunaongeza fedha, *ratio* ya kitabu kimoja mtu mmoja inaongezeka ili kuhakikisha kwamba baadaye kila mtu anakuwa na kitabu chake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kutumia maktaba mtandao limezungumzwa hapa, tayari tumekwishaanza kutumia, kazi yetu ni kusambaza fursa hiyo ili iweze kuwafikia wanafunzi wengi zaidi na vilevile uboreshaji wa shule, kama wanavyofahamu, unafanyika. Kwa

hiyo, ningeomba wote tuendelee kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu kwa jambo hili. Ni jambo kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kusema; nilishangaa kuna nchi mbili zimewahi kuja hapa, waliambiwa na Benki ya Dunia, kwamba, wanataka kuanzisha mageuzi ya elimu, kaangalieni Tanzania. Sisi tunasema mbona ndiyo tunaanza jamani? Wanasema tumeambiwa ninyi mlivyojipanga mnaenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hizi shukrani na pongezi za Mheshimiwa Rais wetu ni jambo kubwa na kazi yetu labda ni kulisemea zaidi. Kwa sababu ni rahisi sana kufurahia ukiona daraja kubwa, kuona barabara ya lami, lakini watu wanaweza wakasahau kwamba uwekezaji wa namna hii wa kimfumo ambao unachukua muda wa kuleta matunda ni uwekezaji ambao unakuja kubadilisha kabisa sura ya nchi yetu na kusukuma mbele katika maendeleo. Tuendelee kumuunga mkono Mheshimiwa Rais wetu na ninaomba wote wamuunge mkono ili bajeti yetu iweze kupita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kubwa ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Hoja imeungwa mkono.

Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae. Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge linakaa kama Kamati ya Matumizi ili kuipitisha bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Tunaanza na Fungu 46, ukurasa 442 kwenye vishikwambi na kwenye kitabu ni ukurasa 392.

**KITABU CHA PILI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 46 – Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resource Management*…………….....…Sh. 8,250,027,145

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa hiki ndicho kifungu ambacho kina mshahara wa Waziri. Kwa hiyo kwa mujibu wa kanuni zetu 123(2) na (3) tafsiri ya pili na ya tatu tumepokea ombi la kupata maelezo au ufafanuzi. Nimwite Mheshimiwa Kenneth Nollo.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nipate maelezo kuhusu utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu. Kwanza ninataka Mheshimiwa Waziri atupe maelezo. Sawa, Serikali inatoa fedha nyingi kwa ajili ya mikopo, lakini mfumo huu bado una *digital discrimination*. Kwa maana gani? Maana moja ni kwamba kama mtoto alisoma *private form four* au *form six* tayari yuko *penalized* asipate mkopo. Sasa inawezekana mwingine alisomeshwa na wafadhili au alisomeshwa na wazazi wake, wazazi wamefariki, kwa hiyo *automatically* iko *penalized*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, kuna mtoto anapata 30% mwingine anapata 70%; kwa hiyo haiko *rational.* Sisi tunaona namna ambavyo watoto hawa wengi hawapati fedha ya mkopo; unaona kabisa *the same*. Mwingine ni yatima lakini hapati. Vilevile tunasema tunatumia mfumo wa kielektroniki, *digital something,* kwenye kutoa mkopo huo, lakini mkopo ule mtoto wa aki-*appeal* inamwambia hujapata. *The reason behind* haipo, haionekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Mheshimiwa Waziri atupe maelezo, je, kwa nini wasiweke *a threshold* kwamba wale wote wanaoomba mikopo angalau waanze na 70%, halafu kama kuna mahitaji ya wengine kuongezeka zaidi, kama wale wanafunzi wa sayansi, tutakuwa tumeondoa ahueni. *Otherwise* tatizo la watoto, hasa wengi ambao wanatoka familia duni, wako mitaani, wako

*stranded,* wamekosa mikopo na mfumo haujakaa sawasawa. Ninaomba hilo Mheshimiwa Waziri atupe maelezo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri Profesa Adolf Mkenda nikwite kwa kutoa maelezo na ufafanuzi.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *Concern* ya Mheshimiwa Mbunge ni ya msingi sana. Ni kweli katika taarifa ambazo zinatumika kufanya maamuzi kama mwombaji wa mkopo apate mkopo ama asipate katika taarifa zote ambazo zinatumika mojawapo ni historia yake na alikosoma. Ziko shule ambazo ada yake ni kubwa kabisa kuliko ada ya chuo kikuu ya miaka yote mitatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, ni kweli kwamba kunatokea wakati mwingine familia ya mtu inasaidiwa labda, mjomba akasema mimi mwanao ninampeleka hapa *form six* baada ya hapo nakuachia mwenyewe. Sasa, baada ya hapo anabaki kwa wazazi na wazazi hawawezi kumsomesha kwa sababu alipokwenda kusomeshwa kasomeshwa na ndugu au mfadhilii au kitu kingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunachofanya sasa hivi tuna ofisi za kanda na *hotline* na lazima tuboreshe zaidi, kwamba mtu anaweza akajitetea na Bodi ya Mikopo ina maelekezo kwa kutumia viongozi, kuanzia viongozi wa mtaa na kadhalika kuhakiki kwamba huyu, pamoja na kwamba alisoma katika shule ambayo ni ghali sana; wengine wanalipa karibu shilingi milioni tano katika shule hizo anazosoma kwa mwaka; kwamba pamoja na hivyo lakini kwa kweli familia yake haiwezi kusoma, kwa hiyo asije akakosa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ni lazima tuendelee na kila siku tukifungua dirisha tunajaribu kutoa elimu labda kazi yetu ni kutoa elimu kubwa zaidi. Taarifa hii ni ya kwa kuanzia, Kwa kiasi fulani wengi ambao wanaondolewa kwa msingi huo ni kweli wana uwezo wa kujisomesha. Kwa sababu ukienda vyuo vikuu vya Serikali kwa Tanzania vinaonekana ndivyo bora, ndivyo watu wanavyovikimbilia zaidi kuliko vyuo vikuu vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mtu aliyesoma shule ya *private* huko anapotaka kuingia chuo kikuu anataka kuingia chuo kwenda kusoma. Ni *conern* ya kweli na kwa kweli kazi ni kuendelea kutoa *information* na kuelimisha na kuhakikisha kwamba hicho kikwazo ambacho wengine wanakipata hakipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, nimeona kesi nyingine ambazo zinapopelekwa na ushahidi na watu wakaenda waka-*check* wanapewa mkopo pamoja na historia hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli vile vile, kwamba kuna utofauti wa asilimia; na hivyo uwezo wa familia; unapimwa na vigezo. Juzi hapa tulikuwa na kikao Wizarani na Bodi ya Mikopo na niseme tena wakati Waheshimiwa Wabunge wengi walisema hapa tubadilishe Bodi ya Mikopo iwe ni Mfuko; sisi vilevile tuna maelekezo ya Mheshimiwa Rais, kwamba tufanye *reforms* kubwa katika Bodi ya Mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo maoni ya Waheshimiwa Wabunge tunayachukua vilevile. Kazi ilikwishaanza, tumeshaangalia na juzi hapa tuliletewa taarifa na tumeipitia tena; kati ya vitu ambavyo kuangalia ni vile vigezo jinsi vinavyotumika; kuhakikisha kwamba vinachukua watu vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli vilevile, kwamba utumiaji wa *electronics* kuna baadhi ya watu wanaweza wakapata shida kidogo, hasa katika *communication.* Tungependa sana kupata *feedback.* Hili tunalichukua na tutajaribu kuona. Kama mtu ame-*apply* halafu hakupata tusikie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kwamba bahati nzuri kuna watu wako *very aggressive*, mtu wa kawaida kabisa huko vijijini, akienda Bodi ya Mikopo hakupata zinapigwa simu mpaka zinapigwa nyingine kwangu, zinapigwa kwa Katibu Mkuu na kwa Naibu Waziri. Sisi tunawaambia Bodi ya Mikopo tuleteeni ushahidi *what happen* hapa. Unakuta mtu anasema kwamba mimi ni yatima; halafu anatakiwa aweke vyeti vya vifo, halafu havipo. *Automatically* wakati unapojaza hupati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kwa kweli kuna haja ya kupanua wigo wa taarifa anazopata mwombaji na majibu anayoyapata mwombaji ili kuhakikisha kwamba tunaendelea kutoa mikopo hii kwa namna ambayo ni ya haki zaidi.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Profesa kwa maelezo. Waheshimiwa kifungu hiki kinaafikiwa?

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*......................Sh. 1,305,364,501
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit*…........................Sh. 2,198,025,000
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit*……...............................Sh. 1,132,475,200
Kifungu 1005 – *Procurement Management Unit*................Sh. 821,692,000
Kifungu 1006 – *Government Communication Unit*……......Sh. 600,719,000
Kifungu 1007 – *Legal Unit*……............………………….Sh. 588,997,000
Kifungu 1008 – *Information, Communication, Technology and E-Learning*…...................Sh. 924,906,000
Kifungu 1009 – *Monitoring and Evaluation Unit*………......Sh. 1,031,917,499

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2001 – *Basic Education Development Office*..Sh. 97,771,532,500

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Kifungu 2002 – *School Quality Assurance*...................…....Sh. 56,179,333,659
Kifungu 7001 – *Higher Education*…………………...….....Sh. 378,992,451,000
Kifungu 7002 – *Technical and Vocational Training Division*……………………………….……..Sh. 81,025,990,491
Kifungu 8001 – *Science, Technology and Innovation*…………………………………Sh. 67,018,450,005

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

## Fungu 18 – Tume ya Taifa ya *UNESCO*

Kifungu 1001 –*Corporate Services Unit*............................Sh. 2,512,250,500
Kifungu 1002 –*Legal Services Unit*.........................................Sh. 69,400,000
Kifungu 1003 – *Internal Audit Unit*.........................................Sh. 94,240,000
Kifungu 1004 – *Monitoring and Evaluation Unit*...................Sh. 25,862,500
Kifungu 1005 – *Procurement and Supplies Management Unit*.......................................Sh. 58,430,000
Kifungu 1006 – *Information and Communication Technology Unit*..........................................Sh. 61,300,000
Kifungu 1007 – *Public Relations and Communication Unit*....................................Sh. 22,550,000
Kifungu 2001 – *Programme Management Unit*..............Sh. 1,022,960,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

## KITABU CHA NNE

## MIPANGO YA MAENDELEO

## Fungu 46 – Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*…………………..Sh. 5,465,841,800
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*……………....Sh. 2,420,900,000
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit*……………..........Sh. 71,360,732,738
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit*…..................................Sh. 1,434,494,905
Kifungu 1005 – *Procurement Management Unit*................Sh. 379,000,000
Kifungu 1006 – *Government Communication Unit*..........Sh. 1,101,548,000
Kifungu 1007 – *Legal Unit*……………………..……………..Sh. 563,800,000
Kifungu 1009 – *Monitoring and Evaluation Unit*………..Sh. 15,181,363,297

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2001 – *Basic Education Development Office*……………………………………...Sh. 208,597,846,884

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Kifungu 2002 – *School Quality Assurance*………………....Sh. 4,244,763,200
Kifungu 5001 – *Teacher Education*..................................................…......Sh. 0
Kifungu 7001 – *Higher Education*……………….…....Sh. 1,197,580,804,243
Kifungu 7002 – *Technical and Vocational Training Division*……………………….............Sh. 163,744,666,544
Kifungu 8001 – *Science, Technology and Innovation*………………………..…...Sh. 23,506,186,389

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae. Mtoa Hoja, Taarifa.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa taarifa kuwa, Bunge lako lilikaa kama Kamati ya Matumizi na limekamilisha kazi zake. Ninaomba taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaafiki.

**MWENYEKITI:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Waheshimiwa tukae.

Kwa mujibu wa Kanuni ya 126(4) sasa nitawahoji kwamba Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka wa fedha 2026/2027. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 Yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo basi sasa ninatangaza rasmi kwamba Bunge hili limepitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka wa fedha 2026/2027. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo nichukue nafasi hii kukupongeza sana Mheshimiwa Waziri, Profesa Adolf Faustine Mkenda, kwa kazi nzuri ya kuongoza Wizara hii mpaka kufika hatua hii.

Pia, niwapongeze sana wasaidizi wake tukianza na msaidizi namba moja Mheshimiwa Wanu Hafidh Ameir kwa kumsaidia vizuri Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Niwapongeze vilevile Katibu Mkuu, Profesa Carolyne Nombo kwa kazi nzuri ya kuongoza Wizara hii akisaidiwa na wasaidizi wake tukianza na Naibu Katibu Mkuu, Profesa Daniel Mushi lakini vilevile Naibu Katibu Mkuu Dkt. Hussein Mohamed Omar na watendaji wote wa Wizara hii na Wakuu wa Taasisi mbalimbali ambao tulikuwa nao kwa siku mbili hizi hapa, tunawapongeza sana kwa kazi nzuri.

Kwa ujumla ninadhani Wabunge mmewasikia asilimia kubwa kama mlivyosema wamepongeza sana Wizara hii. Wamempongeza sana Mheshimiwa Rais kwa mageuzi makubwa ambayo ameyafanya kwenye sekta ya elimu. Kwa hiyo Wizara yenu inabeba maono

makubwa hasa ni mhimili mkubwa kwenye Dira yetu ya 2025. Kwa hiyo, tunawapongeza sana na Bunge litakuwa nanyi.

Nisiwasahau pia Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo, mmefanya kazi nzuri na uchambuzi mzuri. Tunawashukuru sana kwa kufanya kazi yenu hiyo ya kikatiba.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, kabla hatujafunga kuna wageni ambao tulikuwa nao jioni ya leo tuweze kuwatambua kabla hatujamaliza.

Kwanza kabisa ni Mheshimiwa Patrick Boisafi, huyu ni Mwenyekiti wa CCM, Mkoa wa Kilimanjaro; Ndugu Suleiman Mfinanga huyu ni *MNEC* Kilimanjaro; Ndugu Daudi Mrindoko, huyu ni Mwenyekiti Jumuiya ya Wazazi CCM, Mkoa wa Kilimanjaro; Ndugu Pai Ureta, yeye ni Mkurugenzi wa *Makoni Printing Press* yuko pale; na Mheshimiwa Diwani Erasmus Kiwango, yeye ni Mkurugenzi vilevile wa *ECOS Builders Limited*. Tunawashukuru sana kwa kuwa nasi jioni hii. *(Makofi)*

Tunao vilevile wageni wa Waheshimiwa Wabunge: tuna wageni tisa wa Mheshimiwa Onesmo Merdson Mnkondya, hawa ni marafiki zake kutoka Mkoani Songwe. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni ambao wametembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; hawa ni wanachama 70 wa Shirika Lisilo la Kiserikali la *Mutual Generation International* ambao ni Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma, Chuo cha *St. John* na Chuo Kikuu cha Ufundi Stadi *VETA* kutoka Jijini Dodoma. Karibuni sana na tunawashukuru kwa kututembelea. *(Makofi)*

Tangazo la mwisho, Waheshimiwa Wabunge mnakumbushwa kuwa kesho Jumamosi tarehe 9 Mei, 2026 kutakuwa na semina itakayotolewa na Wizara ya Afya kuhusu utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote. Semina hii itafanyika Ukumbi wa Pius Msekwa, saa tano asubuhi. Waheshimiwa Wabunge mnasisitizwa sana kufika kwa wakati ili tuanze kwa wakati.

Baada ya matangazo haya machache, ninaomba sasa niahirishe Bunge hili mpaka Jumatatu tarehe 11 Mei, 2026, saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.30 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatatu, Tarehe 11 Mei, 2026, Saa Tatu Asubuhi)*